# Nipashe

Alhamisi Machi 28, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579877

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper





## Madai ya kutekwa m'biashara yazua taharuki mpakani Namanga

UKURASA 3


ama

ALHAMISI MACHI 28, 2019

AFYA NA MAZINGIRA

Watoto Kagera katika hali mbaya, wenye utapiamlo idadi inatisha

Ukurasa 14

Skauti wahamia ufukweni kukabili uchafu uliokithiri

Ukurasa 18

UNAIJUA NAWEZA? Mkakati unaosuka upya mwelekeo kukabili magonjwa hatari nchini

Ukurasa 19

Wanaunguzwa matiti wasivutie wanaume

Ukurasa 20

Waziri Hasunga: Sumu kuvu yatafuna mazao na uhai wetu

UKURASA 13

# Mahakama ya Mafisadi yaanza kazi kwa kishindo

**Yawatupa** miaka 315 jela wawili kwa makosa 105... *Uk. 3*



Polisi wakiweka ulinzi karibu na mlango wa kuingia katika Hoteli ya PR Stadium, katika Manispaa ya Temeke, jijini Dar es Salaam jana, ambapo viongozi wa kitaifa wa chama cha ACT -Wazalendo walikuwa na mkutano wa ndani. **PICHA: HALIMA KAMBI**

## Dola yawazuia Maalim Seif, Zitto

UKURASA 2

### YALIYOMO

UKURASA WA 2

**DC ANUSURU WANAFUNZI 300 KUFUKUZWA CHUO**

MKUU wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, amezuia jaribio la wanafunzi zaidi ya 300 wa Chuo cha Ualimu Moshi kilichopo Kata ya Bondeni wilayani humo, kufukuzwa kuendelea na masomo au wakubali kulipishwa ada ya masomo mara mbili, baada ya kutapeliwa zaidi ya Sh. milioni 60...

## Mawakili wa Nassari, Jamhuri wapambana vikali kwa saa nne

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA, TUYISENGE WAMALIZANA RASMI UK.32

MAONI, KATUNI UK.6




XXXXXX

# DC anusuru wanafunzi 300 kufukuzwa chuoni

**Na Waandishi Wetu,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, amezuia jaribio la wanafunzi zaidi ya 300 wa Chuo cha Ualimu Moshi kilichopo Kata ya Bondeni wilayani humo kufukuzwa kuendelea na masomo au wakubali kulipishwa ada ya masomo mara mbili, baada ya kutapeliwa zaidi ya Sh. milioni 60.

Wanafunzi wanaodaiwa kulizwa fedha hizo na Mhasibu wa chuo hicho, wamo wale wanaotarajia kufanya mitihani ya taifa ya kada hiyo ngazi ya cheti ya 'Grade IIIA' Mei mwaka huu.

Ole Sabaya alizima mpango huo jana, baada ya kwenda katika chuo hicho akiwa ameongozana na kamati yake ya ulinzi na usalama kisha kuzungumza na wanafunzi hao pamoja na menejimenti ya chuo.

"Mkuu wa chuo nakuelekeza usithubutu kufukuza mwananchuo hata mmoja na wasilipe fedha mara mbili kwa sababu muundo wa uongozi wa chuo chenu una kasoro na ndio maana wizi huu umetokea mchana kweupe,"

Zaidi aliongeza "Huo wizi wa fedha za hawa wanafunzi mmegundua baada ya miezi 15 kupita, huyo mhasibu na mwenzake ambaye ni wakala wa Benki moja wako wapi OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) tutahakikisha haki ya chuo inapatikana na haki ya hawa wanafunzi wanaoendelea na maandalizi ya mitihani yao ya taifa nayo inapatikana."

Akitoa maelezo, Mkuu wa chuo hicho, Fedrick Akyoo alimweleza Ole Sabaya kuwa wanafunzi hao ni kweli walimpa fedha mkononi mhasibu wao Septemba 2018 na baadae waligundua kutokuwapo kwa fedha hizo katika akaunti ya chuo Desemba mwaka jana.

Alisema kiasi cha fedha ambazo wanachuo hao wametapeliwa ni zaidi ya Sh.milioni 60.2

Wiki iliyopita, Mkuu wa chuo hicho alisema walikuwa wanajiandaa kuwarejesha nyumbani wanafunzi hao wakatafute ada upya kwa kuwa hawana uwezo wa kuwahudumia kwenye mahitaji mbali mbali hapa chuoni.

Alisema wanafunzi hao wana makosa kwa vile wao walitapeliwa na mhasibu kwa kukubali kumkabidhi pesa kinyume cha sheria na taratibu za chuo hicho.

Kwa mujibu wa Akyoo, walifikia uamuzi huo baada ya wakaguzi wa ndani wa mahesabu pamoja na wakaguzi wa nje kugundua kuwa mhasibu huyo alikula njama na wakala wa taasisi moja ya fedha kuingiza fedha hewa kwenye akaunti ya chuo kwa mwaka 2017/2018.

Akyoo alisema mhasibu huyo aliweza kutengeneza risiti hewa 380 kwa utaratibu anaoujua na kwamba taarifa ya wakaguzi wa ndani na nje zinaonyesha chuo kiliiingiziwa milioni tano pekee kati ya zaidi ya Sh.milioni 60.2

Baadhi ya wanachuo wanaodai kutapeliwa fedha hizo akiwamo Chacha Nyagana alisema kuwa mhasibu huyo alikuwa akichukua fedha za wanafunzi mkononi na kuahidi kuwaletea risiti za benki. Alipotafutwa Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Hamis Issah kutoa ufafanuzi kuhusiana na madai hayo, alieleza taarifa hizo ndio zinamfikia, lakini akaahidi kulifanyia kazi na atatoa taarifa zake baadae.

**Imeandikwa na Mary Mosha na Godfrey Mushi**

# Dola yawazuia Maalim Seif, Zitto

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Polisi Mkoa wa Temeke, jijini Dar es Salaam, limezuia mkutano wa Chama cha ACT-Wazalendo uliokuwa umepangwa kufanyika katika ukumbi wa mikutano wa PR Stadium, Wilaya ya Temeke.

Mkutano huo ulitarajiwa kufanywa jana na viongozi wakuu wa chama hicho pamoja na wanachama wake wa Mkoa wa Dar es Salaam, lakini ilishindikana baada ya polisi kufika na kuuzuia kwa madai ya kiusalama.

Viongozi waliotarajiwa kuongoza mkutano huo ni pamoja na Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe, Naibu Kiongozi wa chama hicho, Juma Duni Haji na mwanachama mpya wa chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad.

Kwenye maeneo jirani na ambako mkutano huo ulipangwa kufanyika, yalionekana magari ya askari wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) yakiranda randa na askari wenye silaha. Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, Kaimu Kamanda wa Polisi Temeke, Kamishna Awadhi Haji, alikiri Jeshi la Polisi kuzuia mkutano huo kwa sababu alizosema kuwa ni za kiusalama.

"Ni kweli tulilazimika kuzuia mkutano wa ndani uliokuwa umepangwa kufanywa na Chama cha ACT-Wazalendo na ilikuwa kwa sababu za kiusalama," alisema Awadhi na kuongeza: "Tunajua kwamba wana haki kufanya mikutano yao ya ndani, lakini sisi kama chombo cha dola tunawajibu wa kulinda usalama wa raia wetu hasa tunapobaini kuwapo kwa viashiria vya uvunjifu wa amani."

Baada ya kuzuiwa kufanya mkutano huo, viongozi wa chama hicho walikwenda kwenye ofisi za chama Kijitonyama kuzungumza na waandishi wa habari kuhusu tukio hilo.

Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto, alisema walipanga kugawa kadi zaidi ya 9,000 kwa wanachama wapya wanaotaka kujiunga na chama hicho.

Zitto alisema pamoja na kuzuiwa kufanya mkutano huo, lakini wataendelea kufanya shughuli zao za kukijenga chama hicho bila kuvunja sheria.

"Nawaagiza viongozi wote wa kata katika maeneo yote mhakikishe mnafanya ziara za kwenda kuwaandikisha wanachama hao wapya, naomba muwaorodheshe wote, kazi lazima iendelee hatukati tamaa na haturudi nyuma, lazima tusonge mbele," alisema Zitto.

Zitto alionyesha bendera na kadi za wanachama wa Chama cha Wananchi (CUF) ambao wameamua kujiunga na chama hicho ambazo zilikuwa zimewekwa katika mabegi na mifuko.

Alisema wanatarajia kuzirudisha kadi na bendera hizo katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa wakati wowote kuanzia sasa.

Akizungumza katika mkutano huo, mwanachama mpya wa chama hicho, Maalim Seif, aliwataka wanachama wa chama hicho kutokata tamaa.

"Mimi mwenzenu haya mambo nimeyazoea sana, siyo mara ya kwanza kunitokea na niwaambie kwamba hii ni dalili ya kutukomaza, ACT-Wazalendo ni chama kichanga, lakini ni chama kinachoonekana kuwa tishio kwa sasa. Safari hii ndiyo kwanza imeanza upya, hatukati tamaa, tumeshusha tanga na tumepandisha tanga," alisema Maalim Seif.




Aliyekuwa Mbunge wa Arumeru Mashariki, Joshua Nassari (kulia), akitoka nje ya viwanja vya Mahakama Kuu ya Dodoma jana, huku akiongozana na mawakili wake pamoja na wasindikizaji, alipofika kusikiliza ombi la kufungua kesi ya kupinga kuvuliwa ubunge wake na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Saa 4 mvutano kesi ya Nassari

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MVUTANO mkali wa kisheria uliibuka katika Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma jana, kati ya mawakili wa pande mbili katika shauri la kuomba kufungua kesi kupinga uamuzi wa Spika Job Ndugai kumvua ubunge Joshua Nassari.

Mawakili wa Utetezi na Upande wa Jamhuri walivutana kuhusu Kifungu cha 146(3) cha Kanuni za Kudumu za Bunge kilichotumiwa na Spika Ndugai kumvua Nassari ubunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki (Chadema).

Mvutano huo ulidumu kwa takribani saa nne wakati mahakama hiyo ilipoketi kusikiliza shauri hilo la kuomba kufungua kesi ya msingi ili kutengua uamuzi wa Spika Ndugai.

Ombi hilo linasikilizwa na Jaji wa mahakama hiyo, Latifa Mansour, upande wa Jamhuri ukiwakilishwa na mawakili watatu; Alesia Mbuya na Masunga Kawahanga kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Pius Mboya kutoka Ofisi ya Bunge, huku upande wa utetezi ukiwa na mawakili wawili; Hekima Mwasipu na Fred Kalonga.

Shauri hilo namba 22/2019 lilianza kusikilizwa saa 3:15 asubuhi hadi saa 7:15 mchana, Upande wa Jamhuri ulidai Spika Ndugai yuko sahihi kumvua ubunge Nassari huku upande wa utetezi ukidai kuwa Kanuni za Bunge zimekiukwa.

Mawakili wa pande zote walifanya rejea za kesi mbalimbali za aina hiyo, huku Wakili Mbuya akidai spika yuko sahihi katika uamuzi wake kwa kuwa kanuni inasema mbunge atakoma ubunge endapo hatahudhuria mikutano mitatu ya Bunge mfululizo bila taarifa.

Upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili Kalonga ulidai kabla ya kufikia uamuzi huo, Spika alipaswa kutoa onyo kama kanuni inavyoelekeza, lakini hakufanya hivyo na kudai kwa kutoa uamuzi huo, amekiuka kanuni. Baada ya mvutano huo, Jaji Mansour alisema mahakama hiyo imesikiliza pande zote mbili na itatoa uamuzi wa shauri hilo Machi 29, mwaka huu (kesho).

Alisema uamuzi huo pia atautoa baada ya kupitia mapingamizi matatu yaliyowasilishwa na upande wa Jamhuri.

Machi 20, mwaka huu, mahakama hiyo ilisitisha mchakato wa uchaguzi mdogo wa ubunge katika Jimbo la Arumeru Mashariki hadi shauri la kutoridhishwa na uamuzi wa Spika wa kumvua ubunge Nassari litakapotolewa uamuzi.

Mahakama Kuu pia ilitoa siku saba kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwasilisha majibu ya madai ya Nassari. Katika shauri hilo, Nassari aliomba kibali cha kufungua kesi ya msingi ili kutengua uamuzi wa Spika Ndugai kumvua ubunge.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Rais mstaafu, Jakaya Kikwete na viongozi wengine wakiangalia moja ya maabara inayotumiwa na wanafunzi wa Chuo cha Udaktari Ndaki ya Mbeya, kilichopo katika Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya, katika ziara yake mkoani humo jana, kukagua eneo la ekari 3,000 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa chuo kikubwa cha udaktari na kiwanda cha dawa. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mahakama ya Mafisadi yahukumu 2 miaka 315

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, imewahukumu wafanyakazi wawili wa zamani wa Bandari Kavu ya Azam ICD, kutumikia kifungo cha miaka 315 jela, baada ya kupatikana na hatia ya makosa ya kughushi 105 na moja la kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 12.7 na kuachiwa kwa makosa ya kutakatisha fedha na kukwepa kodi.

Kadhalika mahakama hiyo imemhukumu mfanyakazi wa Region Cargo Service, Benson Malembo, kutumikia kifungo cha miaka miwili gerezani kwa kukutwa na hatia ya kuisababishia serikali hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 12.

Mbali na kifungo, mahakama imewaamuru washtakiwa hao baada ya kumaliza kifungo chao kulipa fidia ya Sh. bilioni 6.35 sawa na nusu ya fedha waliyoisababishia hasara Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ya Sh. bilioni 12.7.

Hukumu hiyo ilitolewa na Jaji Winfrida Korosso na kuwataja washtakiwa waliotiwa hatiani kuwa ni Malembo, Meneja wa Operesheni za Usalama Azam, Raymond Louis na mfanyakazi wa Azam, Khalid Yusufu Louis.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa walikuwa wakikabiliwa na mashtaka 110 ikiwamo ya kula njama, utakatishaji wa fedha na kukwepa kodi.

Jaji Korosso alisema washtakiwa Raymond na Khalid wametiwa hatiani kwa mashtaka ya kughushi la pili hadi la 106.

"Mahakama yangu inawatia hatiani na kuwahukumu Raymond na Khalid kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka mitatu kila kosa kwa kosa la pili mpaka la 106, pia watatumikia kifungo cha miaka miwili kwa kosa la kuisababishia hasara TRA pamoja na Malembo," Jaji Korosso alisema.

Alisema baada ya kupitia ushahidi wa mashahidi 34 bila kuacha

INAENDELEA UK. 8

## Wafugaji wavamia kambi hifadhini, wajeruhi askari

**Na Ashton Balaigwa,** MVOMERO

KUNDI la vijana wa jamii ya wafugaji wakiwa na silaha za jadi, wamevamia kambi ya Msitu wa Hifadhi ya Pagale wilayani Mvomero Mkoa wa Morogoro na kujeruhi askari wa hifadhi hiyo na wa Suma JKT na kuharibu mali mbalimbali.

Mbali na kuharibu mali na kujeruhi, pia wanadaiwa kupora ng'ombe 300 waliokuwa wamekamatwa na askari hao baada ya kuharibu shamba la miti lenye ukubwa wa hekta 400 kati ya 500 zilizopandwa katika hifadhi hiyo.

Mmoja wa askari hao aliyekuwa katika kambi hiyo, Athuman Mkopi, alisema wafugaji hao walivamia kambi hiyo juzi, majira ya usiku na kuvunja milango na madirisha kwa kutumia silaha na kuanza kuharibu mali nyingine ikiwamo gari, pikipiki na baiskeli zilizokuwa nje ya jengo hilo.

Alisema yeye ambaye alikuwa nje ya jengo hilo kwa ajili ya kulinda mifugo iliyokamatwa na kuhifadhiwa katika zizi, alijeruhiwa kwa kupigwa na kitu kizito kisha wakapora ng'ombe wote waliohifadhiwa katika zizi hilo na kuondokana nao.

"Mimi nilikuwa nje ya jengo la kambi yetu ambako kuna zizi kama mlinzi wa zamu, na wenzangu walikuwa ndani, hivyo walivyovamia na silaha, walinipiga na kitu kizito na nikapoteza fahamu kisha wakachukua mifugo yote niliokuwa nikilinda na kuondoka nayo," alisema Mkopi.

Askari mwingine, Junie Eliudi, alisema wakati wa uvamizi, alikuwa ndani na wenzake wakiwa la silaha za moto, lakini waliamua kutulia kwa kuwa wangeamua kuzitumia wanadhani wangesababisha maafa.

"Sisi tuliokuwa ndani sio

INAENDELEA UK. 8

## Taharuki mpaka wa Namanga

**Na Zanura Mollel,** NAMANGA

TAHARUKI imezuka katika mpaka wa Kenya na Tanzania (Namanga), baada ya wakazi wa upande wa Kenya kuzuia magari ya Tanzania kuingia upande wao kwa madai ya kutekwa kwa mfanyabiashara wa kubadilisha fedha za kigeni upande wa Kenya, juzi majira ya saa tatu usiku.

Mmoja wa wananchi wa eneo hilo upande wa Kenya, Odinga Nguduu, adai kuwa, majira ya saa tatu ilikuja gari yenye namba za usajili wa Tanzania kwenye ofisi ya mfanyabiashara huyo na kuondoka naye kuelekea Namanga ya Tanzania.

"Tangu achukuliwe jana usiku (juzi), hajarudishwa na hadi sasa haonekani mtu wetu, wakimrejesha Moha wetu tutaacha vurugu na tutaruhusu magari haya ya abiria na mizigo kuingia Kenya," mwananchi huyo alidai.

"Anaitwa Moha, ni raia wa Kenya mwenye asili ya Kisomali," alidai.

Simon Ledupa mkazi wa Namanga upande wa Tanzania, alisema kuwa Namanga ni mpaka mkubwa na kuna watu wengi kutoka mataifa mbalimbali wanapita na kwamba madai ya kutekwa kwa mtu huyo sio ya kweli.

Alisema, wanapodai kuwa gari iliyomchukua mtu huyo ni yenye namba ya Tanzania wanauhakika gani kwa sababu mpakani biashara za magendo ni nyingi na watu kutumia plate number (kibao cha namba) za nchi kwa nchi kwa biashara haramu inatumika.

INAENDELEA UK. 8


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 27/03/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumapili tarehe **31/03/2019** kampuni ya **S.S.F Co.LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **MTIBWA kuelekea DAR ES SALAAM** gari hilo lenye namba za usajili:
   **T785 CAD/T 166 ADN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **21.80** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.85** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.60** |

3. NJia itakayotumika **MTIBWA hadi DAR kupitia MZANI WA MIKESE** gari litasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215143402

HABARI KITAIFA

# Wizara zaagizwa kuhusu ushirika

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA zote zinazohusika na Vyama vya Ushirika kwa Akiba na Mikopo (SCCULT) zimetakiwa kuhakikisha zinakuwa na Dawati la Ushirika na taarifa zake kuwasilishwa kwa Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Tanzania.

Pia, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imetakiwa kuhakikisha kuwa inasimamia, kudhibiti na kuhamasisha vyama vya ushirika viweze kufanya kazi kikamilifu na kwa wakati kwa kuzingatia Sheria ya Ushirika Namba 6 ya Mwaka 2013 na kanuni zake za mwaka 2015; na kanuni za Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo ya 2014.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, ndiye aliyetoa maelekezo hayo alipomwakilisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwenye kongamano la Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo Afrika linalofanyika jijini Mwanza.

Hasunga alisema mamlaka zote zinazohusika na Maendeleo ya Sekta ya Ushirika nchini zijiwekee malengo yanayotekelezeka ya kusukuma gurudumu la maendeleo ya ushirika na kujipima kila mara.

Kadhalika, serikali imesema itaendelea kuwachukulia hatua kali za kisheria kwa wote wanaobainika kuhujumu dhamira njema ya maendeleo ya ushirika kwa kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha matarajio ya kuanzishwa kwa vyama hivyo. Alisema serikali imeendelea kuweka mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa sekta ya ushirika inakua na kujisimamia vema katika utekelezaji wa majukumu yake japo bado kuna wabadhirifu wachache wanaoendelea kubainika.

Alisema ushirika wa akiba na mikopo una umuhimu mkubwa katika jamii kwa sababu unajenga jamii yenye utamaduni wa kuweka akiba ya fedha mara kwa mara na kuwa na matumizi bora ya fedha zao kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya siku za usoni, kuanzishwa kwa Saccos nyingi katika maeneo mengi ya vijijini, ambazo zimesogeza karibu huduma za kifedha kwa wananchi wa kawaida.

Pia kuwawezesha kumiliki na kuendesha taasisi yao wenyewe ya fedha na kutoa mikopo kwa wanachama wake kwa masharti na riba nafuu wanayojiwekea wao wenyewe kwa mujibu wa sheria na kanuni lengo likiwa kuboresha maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii.

Alisema SCCULT imejiendesha kwa udhaifu kwa kutotoa huduma stahiki kwa wanachama wake kwa muda mrefu takribani miaka 10, ambapo kipindi hicho ikiwa na wanachama 1,247, na kwamba hadi Januari, 2019 zoezi la uhakiki juu ya uwapo wa wanachama hao kama wapo hai na wanafanya shughuli zao umebaini takribani vyama vina wanachama 500 tu ambavyo vipo hai na vinafanya kazi.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (wa tatu kushoto), akikagua miundombinu ya umeme katika Kijiji cha Kazuramimba, wilayani Uvinza, Mkoa wa Kigoma juzi. Habari Uk. 9. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfanyabiashara matatani shehena ya nyavu haramu

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MFANYABIASHARA wa zana za uvuvi mkoani Mwanza, Jeremia Assama, anashikiliwa na maofisa wafawidhi wa rasilimali za uvuvi Kanda ya Ziwa Victoria, kwa kosa la kuingiza na kuuza nyavu haramu zenye macho ya nchi mbili.

Kukamatwa kwa mfanyabiashara huyo kunatokana na operesheni ya kukamata wavuvi haramu wanaovua sangara wenye uzito wa sentimita 85 katika Ziwa Victoria kutokana na uvuvi wa baadhi ya wavuvi kuwadanganya wenzao kuwa Waziri wa Uvuvi Luhaga Mpina ameruhusu kuvua samaki hao.

Samaki wenye uzito huo walizuiwa kuvuliwa kwa sababu ndio wazazi wa samaki wengine aina ya sangara.

Akizungumza katika eneo la tukio ambalo Assama alikuwa na ghala lililokuwa likihifadhi marobota 67 ambayo yalikuwa na nyavu 13,400 zenye macho ya nchi mbili, Ofisa Mfawidhi wa Rasilimali za Uvuvi mkoani Mwanza, Masui Munda, alisema walimtafuta kwa muda mrefu mfanyabiashara huyo.

"Katika mitego yetu tuliweza kujua zana hizo ziko wapi na tukatengeneza mazingira ya kumpata mhusika, tulifanikiwa kwa hilo kwa kumkuta dukani kwake tulimhoji kuwa ana gowdown (maghala) mangapi na yako wapi, alichokifanya ni kutupeleka katika gowdown (ghala) lililo na zana halali lililo karibu na nyumbani kwake, jambo ambalo halikuwa makusudio yetu," alisema Munda.

Aidha, Munda alisema baada ya kufika katika ghala hilo walimuuliza kama ana ghala lingine liliko, lakini Assama alikataa ndipo walipoamua kumpeleka wenyewe katika ghala ambalo alikuwa ameficha marobota hayo ya nyavu haramu na walipomuuliza tena alikiri kuwa ni mali zake.

Ofisa Mfawidhi wa Rasilimali za Uvuvi Kanda ya Ziwa Victoria, Didas Mtambalike, alisema mtuhumiwa Assama anatuhumiwa na makosa ya kutengeneza, kuhifadhi vyavu haramu.

"Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 Namba 69 F, inasema nyavu zote zilizo chini ya milimita tatu haziruhusiwi katika maji yoyote yale Tanzania," alisema Mtambalike.

Aidha, mtuhumiwa alijitetea kuwa nyavu hizo hakuagiza kwa kipindi cha sasa, aliingiza kabla serikali haijazuia nyavu, na kwamba walipoanza kuzuia na kuzikamata, aliamua kuzitunza nyavu hizo.

# Wakurugenzi waagizwa kujibu hoja za CAG

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imewataka Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha kuwa hoja zote zilizoibuliwa kwenye taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), zinajibiwa na kufanyia kazi mapendekezo ya wakaguzi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Mhandisi Joseph Nyamhanga, katika kikao kazi cha upokeaji na uhakiki wa taarifa za majibu na mipango kazi ya utekelezaji wa hoja na mapendekezo ya CAG kwa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa za mwaka 2017/18, jijini hapa.

Nyamhanga alisema kuwa ni muhimu hoja zote zikafanyiwa kazi haraka na kwa ufasaha ili kunusuru upotevu wa fedha, kuboresha utendaji na kuimarisha utawala bora, jambo ambalo ndio msingi wa ukaguzi.

"Kila mtumishi afanye kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni, miongozo, taratibu na kuwajibika bila kuoneana haya, tukifanya hivyo, hoja zisizo za lazima zitaondoka na hata wakaguzi hawatatumia muda mwingi katika kufuatilia mambo ya msingi zaidi katika kuboresha utendaji," alisema.

Alieleza kuwa katika kujibu hoja za CAG na kuandaa mpango kazi wa utekelezaji wa maagizo ya CAG ya hesabu za mwaka 2016/17, imeonekana kuwa kufikia mwezi Januari 2019, jumla ya hoja asilimia 47 zilifungwa wakati asilimia 53 zilikuwa bado hazijajibiwa.

Aidha, aliwataka Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha kuwa hoja na mapendekezo ya taarifa ya CAG wanayafanyia kazi ili kuboresha utendaji wa kazi na kuimarisha uwajibikaji. "Kwa kufanya hivyo tutakuwa tunatekeleza maagizo ya rais kuhusu kufanyia kazi maagizo ya CAG na kuchukua hatua stahiki kwa watumishi na inaelekeza kuwa, watendaji wakaendelee kufanyia kazi hoja na mapendekezo ya CAG na kuwasilisha kwa wakaguzi wa CAG," alisema.

Katibu Mkuu aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kuhakikisha kuwa baada ya taarifa ya CAG kuwasilishwa bungeni majibu na vielelezo viwasilishwe kwa wakaguzi wa CAG ndani ya siku 21 kwa mujibu wa sheria. "Sitegemei kuona majibu ya awali yasiyojitosheleza ilhali mmekutana Dodoma kwa ajili ya kuyaboresha majibu yenu," alisema.

## HABARI KITAIFA

# WFP yaahidi kuisaidia Tanzania uhaba chakula

**Na Gwamaka Alipipi**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula (WFP) limesema lipo tayari kuisaidia Tanzania muda wowote endapo itakumbwa na ukame au uhaba wa chakula,kama ilivyo sasa kwa nchi ya Kenya.

Mwakilishi mkazi wa WFP Tanzania, Michael Dunford, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipokutana na waandishi wa habari kuzungumzia upatikanaji wa lishe bora katika wilaya za Chamwino, Bahi, Ikungi, baada ya kuzitembelea na kufanya utafiti.

Alisema WFP wana utaratibu wa kusaidia linapotokea tatizo la ukame au janga la njaa katika nchi husika, kama ilivyo sasa katika nchi za Msumbiji, Malawi na Zimbabwe ambazo zimekumbwa na mafuriko.

"Tumeshatoa msaada Msumbiji, Malawi na Zimbabwe, kuna timu yetu ambayo imeondoka hapa kwenda huko kusaidia, WFP itasaidia maeneo yoyote yenye ukame Afrika Mashariki kama vile eneo la Turkana Kenya ambalo kwa sasa limekumbwa na ukame mkubwa," alisema Dunford.

Dunford alisema WFP imekuwa ikifanya kazi na Tanzania kwa muda mrefu katika kusaidia chakula, hivyo itaendelea kushirikiana nayo katika kila jambo litakalotokea.

**"Tumeshatoa msaada Msumbiji, Malawi na Zimbabwe, kuna timu yetu ambayo imeondoka kutoka hapa kwenda huko kusaidia, WFP itasaidia maeneo yoyote yenye ukame Afrika ..."**

Kwa upande wake Ofisa lishe wa WFP Tanzania, Neema Shosho, alisema WFP kupitia programu ya boresha lishe imekuwa ikishirikiana na ngazi za juu kitaifa kama vile Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), katika kuhakikisha wananchi hususani kinamama na watoto wanapata lishe bora.

"Pia tunashirikiana na ngazi za mikoa, wilaya pamoja na jamii ambapo wamekuwa wakiunda kamati zinazotekeleza mipango ya lishe bora, na hadi sasa tumeshawafikia wanawake 43,800, vikundi 50 na tumewajengea uwezo wa kutoa elimu kuhusu lishe," alisema Shosho.

Naye mtoto wa mfalme wa Jordan, Princess Sarah Zaid, ambaye ni mshauri wa lishe ya mama na mtoto WFP, alisema alifanya ziara katika wilaya za Chamwino na Bahi mkoani Dodoma na kukuta idadi kubwa ya watoto chini ya miaka mitano wanakosa lishe bora.

Alisema mtoto asipopata lishe bora humsababishia kutokukua vizuri, pia huchangia kutokufanya vizuri katika masomo shuleni.

# Korti Kuu yatengua hukumu ya Kisutu

**Na Enock Charles**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imetengua hukumu ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam dhidi ya Bob Chacha Wangwe kulipa faini ya Sh. 500,000 au kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela.

Akisoma hukumu ya rufaa dhidi ya hukumu hiyo jijini jana, Jaji Seif Mwishehe Kulita, alisema Bob Wangwe alihukumiwa kimakosa kwa kuwa hapakuwa na ushahidi wa kutosha kumtia hatiani ikiwa ni pamoja na kutokuitwa mahakamani kwa mashahidi muhimu waliotajwa katika shauri hilo kutoka mamlaka ya mawasiliano nchini (TCRA) kuthibitisha madai dhidi yake.

Akitaja mambo muhimu ya kuzingatia kabla ya kutoa hukumu katika kesi ya makosa ya mtandaoni, Jaji Kulita alisema ni lazima mtuhumiwa awe ametoa taarifa hiyo yeye mwenyewe, iwe imethibitishwa kuwa ni taarifa ya uongo na pia kama imelenga kuleta taharuki.

Rufaa hiyo namba 370 ya mwaka 2018 ilitokana na hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu dhidi ya mshtakiwa huyo aliyekuwa anakabiliwa na mashtaka ya kusambaza ujumbe uliodaiwa kwenda kinyume cha Kifungu cha 16 cha Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2015.

Katika kesi hiyo iliyofunguliwa na Jamhuri dhidi ya Bob Wangwe, mahakama hiyo ilimtia hatiani na kuamuru alipe faini ya Sh. 5,000,000 au kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya hukumu ya jana, Bob aliishukuru Mahakama Kuu kwa kutenda haki katika kesi hiyo na kuwashauri Watanzania kutokata tamaa na kuridhika pale wanapohisi kuwa wameonewa katika hukumu zinazotolewa na mahakama za chini dhidi yao.

"Maamuzi haya yanaweka msingi muhimu kwa kesi nyingine za aina hii kwa kuwa yatatumika kama rejea, naishukuru mahakama kwa kutenda haki na ninawasihi Watanzania wasiwe watu wa kukata tamaa na kuridhika pindi wanapohisi kuonewa na mahakama za chini," Bob alishauri.

Wakili wa utetezi katika kesi hiyo, Jebra Kambole na Bob walisema watafuatilia katika utawala wa Mahakama ya Hakimu Kisutu kurejeshewa Sh. 500,000 ambazo Bob alilipa baada ya kutiwa hatiani.


RADIO One

POPOTE ULIPO SIKILIZA RADIO ONE KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.radioone.co.tz /RadioOneStereo /RadioOneStereo /radioonetz



ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http://www.ewura.go.tz

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya kifungu Na.19 cha sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni Na. 17 (4) ya Kanuni za Mafuta (Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Reja Reja na Matumizi Binafsi), Gazeti la Serikali Toleo Na. 380 la 2018)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya kubadili umiliki wa leseni na jina la kituo cha mafuta kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| **Jina la awali la kituo** | : | State Oil Tanzania limited-Majengo Road Station |
| **Nambari ya Leseni** | : | PRL-2016-151 |
| **Mahali Kituo kilipo** | : | Kiwanja Namba 463, Kitalu "V" Majengo, Manispaa ya Songea, Mkoani Ruvuma |
| **Jina linalopendekezwa** | : | Refuelling Solution(T)Ltd-Majengo Road Petrol Station |
| **Mmiliki wa awali** | : | State Oil Tanzania Limited |
| **Mmiliki mpya** | : | Refuelling Solutions (T) Ltd |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA,**

215143702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maofisa elimu wafanyie kazi kauli ya Majaliwa

**KAULI** iliyotolewa juzi jijini Dodoma na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kuhusu vitendo vya wizi wa mitihani, ina ukweli na ni ya msingi.

Majaliwa aliamua kuirudia kauli hiyo pengine kutokana na kutaka viongozi wanaosimamia elimu aliokutana nao waelewe athari zake kwa taifa, hivyo wachukue hatua za kukomesha hujuma hizo.

Kutokana na kuonekana kukerwa na kuendelea kushamiri kwa vitendo vya wizi wa mitihani Majaliwa alitoa onyo kali kwa baadhi ya maofisa elimu wa mikoa na wilaya wanaoshirikiana na walimu kujihusisha na wizi, udanganyifu na uvunjaji wa mitihani na kuwataka waache mara moja tabia hiyo kwa sababu unalivunjia heshima na hadhi taifa.

Waziri Mkuu alisema kamati za mitihani za mikoa na wilaya ziendelee kusimamia sheria, kanuni na taratibu bila ya woga, upendeleo na ziyumbishwe na hatua za kinidhamu na kiutumishi kwa mujibu wa sheria, na kwamba hatua ziendelee kuchukuliwa dhidi ya wote wanaobainika kukiuka sheria, taratibu na miongozo inayotolewa.

Waziri Mkuu alitoa onyo hilo juzi wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa sita wa Umoja wa Maofisa Elimu Mikoa na Wilaya (REDEOA).

Waziri Mkuu alisema Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) ni chombo ambacho kwa muda mrefu kimejijengea sifa nchini na barani Afrika, na serikali imewekeza kiasi kikubwa cha rasilimali ili kukifanya chombo hiko kuwa imara na cha kisasa.

Alisema hali hiyo imezifanya nchi mbalimbali kuja nchini kujifunza masuala ya upimaji na uendeshaji wa mitihani, na kwamba amejulishwa pia hivi sasa nchini wapo viongozi wa mabaraza ya mitihani kutoka nchi za Afrika Mashariki.

Matukio ya udanganyifu wa mitihani yamekuwa yakiongezeka na kuripotiwa kila mwaka pale NECTA inapokuwa inatangaza matokeo ya mitihani ya taifa ya darasa la saba, kidato cha nne na kidato cha sita.

Kinachobainika kila mwaka ni kuwa udanganyifu huo unafanyika kwa kupangwa na walimu wa shule husika ili kufahaulisha idadi kubwa ya wanafunzi, hivyo shule zao kupata sifa.

Matokeo ya udanganyifu huo ni baadhi ya wanafunzi kufutiwa matokeo, baadhi ya vituo vya mitihani kufungiwa pamoja na walimu kuchukuliwa hatua za kisheria na za kinidamu.

Athari kubwa kuliko zote ni kuwa udangantifu huo unasababisha kuzalisha watu ambao hawana uwezo wa kuisaidia kulipatia maendeleo taifa letu, ambalo linahitaji wataalamu katika sekta mbalimbali. Kwa ligha nyingine ni kuwa tunatengeneza mazongira wenyewe ya kuzalisha wajinga.

Itakumbukwa kuwa mpango wa taifa kwa sasa ni kuelekea katika uchumi wa kati kupitia ujenzi wa viwanda, ambao unahitaji nguvukazi ya wasomi na hususan wanasayansi, na ndiyo maana Kaulimbiu ya mkutano huo ilisema "Elimu bora itatufikisha katika uchumi wa kati ifikapo 2025".

Tunaamini kuwa wote wenye dhamana na elimu wenye masikio wamemsikia na kumuelewa Waziri Mkuu kuhusiana na mchezo wa udanganyifu wa mitihani.

Kutokana na uzito wa suala hilo, bila shaka REDEOA watalitolea tamko kabla ya kikao chao, ili hatua madhubuti zianze kuchukuliwa kwa lengo la kutokomeza kabisa vitendo hivyo ambavyo ni hujuma kwa maendeleo ya taifa.

Kila kila mmoja kwa nafasi yake atimize wajibu wake kwa kupinga vitendo vya udanganyifu wa mitihani, na baadaye kuzalisha taifa la wajinga.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Makondakta wababmbika tiketi, wenzetu wa Sumatra mnayajua?

Na Beatrice Shayo

**DALADALA** ni usafiri unaotumiwa na umekuwa ukitumiwa na watu wa makundi mbalimbali, kwa kuwavisha kutoka sehemu moja, kuwapeleka sehemu nyingine.

Ndio tegemeo rahisi linalowezesha shughuli na mizunguko ndani ya miji mikubwa, ikifuatiwa na usafiri wa pikipiki maarufu kama bodaboda na bajaji, achilia mbali nia kongwe ya kuchapa mguu.

Lakini usafiri huo bado unakabiliwa na changamoto kubwa, kutokana na mambo ambayo yamekuwa yakitokea katika uendeshaji wa huduma hizo za daladala.

Unapotaja wahudumiaji daladala mijini, kama yalivyo mabasi ya safari zingine, yana madereva na makondata. Ila kuna watu watu wa ziada ambao hawajazoeleka sana, hawa ni wapiga debe vituoni, ambao jukumu lao kubwa ni kuhamasisha kujaza magari.

Nikirejea tiketi ambayo ni kigezo cha kuhalalisha malipo, zinauzwa katika maeneo mbalimbali.

Zipo baadhi ya daladala ambazo wamiliki wake wamezichapisha kwa kuziandika namba za magari na majina yao, ambayo ndiyo iko rasmi kisheria.

Wapo wamiliki wa daladala wanaonunua tiketi na wanatumia kalamu kuandika namba za magari yao.

Sasa hao ambao wanajiandikia namba za magari, wamekuwa sio waaminifu, kwa kutoa tiketi zilizo na namba za magari mengine. Unakuta gari uliopanda lina namba tofauti na tiketi waliyotoa.

Kama mtu akipata ajali au kusahau mzigo katika gari anaweza kuhangaika mno na huenda asifanikiwe. Ni vigumu kumchukulia hatua mmiliki wa gari, ambalo limebambikwa namba ya tiketi.

> **Changamoto nyingine, ipo katika usafiri wa daladala ni kipindi cha usiku na mchana. Baadhi ya daladala zinakatisha 'ruti' mchana na usiku, hazifiki kituo cha mwisho.**

Kuna kila sababu ya kuwa makini na tiketi hizo na ikiwezekana namba za magari zibandikwe mbele kwa dereva, pia pande za kushoto na kulia, ili mtu anapopewa risiti, aweze kuangalia kama ipo sawa na namba alizokabidhiwa.

Kwa mfano, inapotokea abiria umepata ajari unaenda na tiketi kudai haki zao, kumbe gari unayoidai sio iliokusababishia ajali. Hapa kuna jambo jamani!

Pia, changamoto nyingine katika daladala ni madereva kutokuwa na kauli nzuri katika vyombo vyao, kwa kuwajibu watu waliowazidi umri na wengi wasi na makosa. Tunayashuhudia sana haya.

Kuna majibu ambayo makondakta wanayatoa kwa watu waliowazidi umri, utadhani wanalingana nao.

Changamoto nyingine, ipo katika usafiri wa daladala ni kipindi cha usiku na mchana. Baadhi ya daladala zinakatisha 'ruti' mchana na usiku, hazifiki kituo cha mwisho.Mfano, unakuta gari za Makumbusho kupitia Sinza Mabibo hadi Kariakoo, zinaishia Mabibo hazifiki Makumbusho nyakati za mchana na usiku.

Hali hiyo inasababisha abiria kuingia gharama mara mbili ili uweze kufika Makumbusho au Mwenge.

Ndugu zangu wa Mamlaka ya Usafiri Majini na Nchi Kavu (Sumatra), tuwafungua macho, kama ambavyo vyombo vya habari tumefanya kwa mengi. Chukueni hatua.

BARUA/MJADALA

## Jangwani tunasubiri jiwe la uwekezaji

**Mhariri,**

*MHESHIMIWA Rais wetu kwa heshima na taadhima, kwa niaba ya wakazi waishio Bonde la Msimbazi wanaoguswa na mradi huo, tunapenda kukupongeza kwa kazi ngumu unazofanya, pia tunakupa pole kwa uzito wa majukumu yako.*

*Sisi wakazi wa Bonde la Msimbazi, tulifarijika sana tuliposikia na kuona unapotembelea mradi wa ujenzi wa nyumba katika eneo la Magomeni Kota, mwezi huu.*

*Siku hiyo tulishuhudia jinsi ulivyo karibu na wanyonge wanaotegemea kuingia kwenye nyumba hizo, mara zikatapokamilika. Hakuna shaka wewe ni Rais mtetezi wa wanyoge na sisi tulio wanyonge tutaendelea kumwomba Mwenyezi Mungu akulinde siku zote.*

*Pongezi zetu zingine kwako ni jinsi serikali ya awamu ya tano, ilivyotushirikisha wananchi wa Bonde la Msimbazi kupitia ofisi yako; Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), kubuni na kupanga uendelezaji wa bonde hilo.*

*Dhana iliyopo kitaalamu ni kwamba inahamishwa kutoka mtazamo hatarishi hadi kwenye uwekezaji, makazi, biashara, kuongeza ajira na kipato cha wananchi wa manispaa hadi taifa.*

*Pia, tunaipongeza Benki ya Dunia na asasi ya DFID ya Uingereza, kukubali kufadhili mradi huo na tulishirikiana vizuri katika warsha ya wiki moja.*

*Niseme kwa unyeyekevu mkubwa, Rais wetu kwa niaba ya wakazi wenzangu wa Bonde la Msimbazi ambako mradi unatekelezwa, tuna shauku kubwa kuona siku unatuwekea jiwe la msingi, sote tukipigia makofi ya tukio hilo.*


*Hadi sasa ratiba tuliyoahidiwa imeshapita na mvua za masika zinakuja, bila ya kujua tarehe kamili ya utekelezaji. Tunatanguliza shukurani zetu na Mungu akulinde katika majukumu yako.*

**Wakazi wa Jangwani,**
**Habiba Mondoma (Katibu); 0717303660 na Godwin Cathbert (Mratibu); 0712 104242.**

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Trafiki Ubungo, mzunguko umeyeyushaje ile foleni?




**Na Mwandishi Wetu**

MALALAMIKO ya muda mrefu ya watumiaji wa barabara zinazopita katika makutano ya Ubungo, wamekuwa yanaelekezwa kwa askari wa usalama barabarani, kuwa wanachangia.

Kwa muda mrefu watumiaji wa barabara hizo wamekuwa wakilalamikia, hatua ya baadhi ya askari hao kukaa kati na kuita magari ya upande mmoja kwa muda mrefu, imesababisha misururu mirefu ya magari kwa pande zote.

Licha ya malalamiko hayo ya muda mrefu, hakuna hatua za kina zilizochukuliwa. Ni sura ya machozi ya samaki kuishia kwenye maji.

Uitaji magari ya upande mmoja kwa muda mrefu, licha ya pande zote kuwa magari mengi, ulituumiza sisi wa barabara za Sam Nujoma na Mandela.

Tulishashuhudia mkwaruzano usioopendeza dhidi ya aliyekuwa akiongoza magari kutoka kwa 'watemi' dai lao ni yanapendelewa magari yaliyotokea Kimara kwenda mjini. Kilichotokea sasa katika mzunguko wa barabarani uliojengwa katika 'Interchange' au mapishanao ya barabara Ubungo, umethibitisha kuwapo nafuu mkubwa, kwa kuwa umeondoa kabisa foleni na magari ya pande zote yanapita haraka, kwa mtazamo wangu, kulikuwapo na upunguful wa tatizo.

Kila mtu ameangukia katika mshangao wa, hii ikoje jamani kufikia hali hii? Huko nyuma tulishuhudia malalamiko si yangu tu, bali kwa magari yanayotoka Kimara yanavutwa zaidi, kuliko pande nyinginezo za barabara na nini sababu?

Mfano wa kuakisi hilo, ni jambo linalowezekana gari lilikuwa Mbezi Mwisho kupita Ubungo na yule aliye Sam Nujoma au Mandela akiwa anasubiri.

Nikiwa mtumiaji wa gari, sijafurahia hali ya awali, kwani wananchi wote bila ya kujali upande wa barabara waliko, wana haki sawa ya kuwahi kwenye shughuli zao.

Mkuu wa Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani, Fortunatus Muslim, nakushauri ukinge sikio kutoka malalamiko ya umma na kuyafanyia kazi, badala ya kuyapuuza.

Watu wamelalamika sana kuhusu foleni kubwa, lakini kulitawaliwa na ukimya. Huenda kwingineko nako kuna wezekana kukawa na vilio kama hivyo. Leo hii watu wahoji kwa nini sasa hawaoni ile foleni ya barabara ya Mandela iliyokuwa ikianzia eneo la External?

Ule msusuru wa magari ya Barabara ya Sam Nujoma, iliyokuwa ikianzia kule Ubungo Mawasiliano, mbona umetoweka ghafla? Jibu ninalopata kutoka mtazamo wa haraka, kulikuwapo tatizo la uongozaji magari.

Nashauri, askari wawe na kawaida ya kusikiliza kero za wananchi na kuzifanyia kazi. Nakumbuka baadhi yetu walithubutu kuhoji walishakutana na majibu yasiyopendeza, ya kutotaka kuingiliwa katika majukumu.

Mimi nayaona haya ni majibu mepesi, kutoka kwenye maswali magumu na ninabaki na maswali, kwanini yapatikane majibu ya sampuli hiyo?

**KABWELA** — **NA FADHIL MOHAMMED**



## Mahakama ya Mafisadi yahukumu 2 miaka 315

INATOKA UK. 3

shaka, mahakama imewakuta na hatia na kuwahukumu adhabu hiyo.

Hata hivyo, mahakama hiyo imewaachia huru washtakiwa wawili waliokuwa wanakabiliwa na mashtaka hayo baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha mashtaka dhidi yao.

Washtakiwa walioachiwa ni, Mchambuzi Mwandamizi wa Masuala ya Biashara TRA, Hamis Omary, Haroun Mpande wa kitengo cha mawasiliano na kompyuta ICT TRA.

Jaji Korosso alisema amepitia maelezo ya upande wa mashtaka na yale ya washtakiwa pamoja na mawakili wa utetezi na kusema washtakiwa ni wakosaji wa kwanza na kwamba wanafamilia zinazowategemea kwa kuwa wote wana wake na watoto ambao wanawategemea.

Alisema, amezingatia maombi yote ya washtakiwa kuwa wanajutia makosa yao na pia mshtakiwa Raymond na Khalid, wameiomba mahakama iangalie kipindi cha zaidi ya miaka mitatu walichokaa gerezani.

Aidha, katika utetezi wao waliiomba mahakama kizingatia kuwa katika kipindi chote wakiwa waajiriwa wa Azam hakukuwahi kutokea upotevu wowote na mara zote walikuwa wakionyesha nidhamu na kufika mahakamani bila kukosa.

Katika kesi ya msingi Raymond na Khalid wanadaiwa kutoa makontena kwenye Bandari Kavu ya Azam ICD iliyopo maeneo Sokota na kujaribu kuonyesha yalitolewa kihalali na TRA Dar es Salaam huku wakijua walighushi.

Shtaka lingine wanadaiwa walisababisha hasara ya Sh. 12, 618,970,229 kwa kutoa makontena 329 bila ya kulipia ushuru na malipo mengine.

# Ujenzi mji wa serikali wakamilika 99%

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, (pichani) amesema nia ya Rais Dk. John Magufuli ya kujenga upya mji wa serikali imetekelezwa kwa asilimia 99. Alisema hayo jana alipotembelea mji mpya wa serikali unaojengwa katika eneo la Mtumba, jijini Dodoma kwa kukamilika majengo 20 ya wizara.

Waziri Mkuu alitembelea na kukagua majengo ya wizara 13 na kuridhishwa na hatua za ujenzi zilizofikiwa katika maeneo mengi.

Hata hivyo, alibaini kasoro kwenye mlango wa kuingilia katika Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira na kumwagiza mkandarasi anayejenga jengo hilo auondoe kutokana na kuwa chini ya kiwango.

Kuhusu ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ambayo bado haijamilika, Waziri Mkuu amemwongezea siku 10 mkandarasi na kumtaka akamilishe.

Wakati huo huo, amewaagiza mawaziri na makatibu wakuu kuhakikishe kazi iliyosalia ambayo ni ya kuboresha mazingira ya nje ya ofisi hizo iwe imekamilika ifikapo Aprili 15, mwaka huu. Mji huo unatarajiwa kuzinduliwa na Rais Magufuli.

Awali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema ujenzi wa mji huo ulianza Desemba mwaka jana na ulitarajiwa ukamilike Februari mwaka huu, badala yake utakamilika Mei mwaka huu.

Waziri Jenista alisema ujenzi wa majengo ya wizara tatu ambayo hayajakamilika ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Rais (Tamisemi) na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi na Wenye Ulemavu yatakamilika Mei, mwaka huu.






Meneja Mwandamizi wa Biashara ya Kilimo wa Benki ya NMB, Carol Nyangaro (kushoto), akitoa mada wakati wa ufunguzi wa Jukwaa la tisa la fursa za biashara na uwekezaji, mkoani Lindi juzi. Benki ya NMB ni mdhamini wa jukwaa hilo. **PICHA: NMB**

# Taharuki mpaka wa Namanga

INATOKA UK. 3

"Wasichafue hali ya amani kwa kuwa mtu huyu ni mfanyabiashara mkubwa wa kubadili fedha eneo lao, wanaoneana wivu wenyewe kwa wenyewe, wasituingize Watanzania," alidai Ledupa.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kudai kuwa hadi sasa hakuna athari za kibindamu zilizotokea.

"Ni kweli jambo hili lipo, lakini hakuna kifo wala ulemavu, watu wangu wako salama na tunajadiliana na viongozi wa upande wa Kenya namna ya kutatua taharuki hii," Mwaisumbe alisema.

Menenja wa TRA (Forodha) Namanga ya Tanzania, Godfrey Kitundu, alisema hali hiyo inaathiri mwingiliano wa kibiashara baina ya nchi zote. "Watu hawa wa Kenya wamefunga barabara na kuchoma matairi, magari yetu hayawezi kuingia huko na wala yao hayaingii, mapato yatashuka," Kitundu alisema. Aidha, alieleza kuwa tukio hilo la kufunga barabara linakwamisha pia wafanyabiashara watembea kwa miguu kufanya shughuli zao na kuwatia hofu watalii.

"Kitendo hicho kina ashiria ukosefu wa amani eneo la mpakani, ila kwa kuwa viongozi wameshafika tunasubiri maamuzi yatakayotolewa," alisema Kitundu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, na kwamba walikuwa kwenye kikao kulijadili, na kuahidu kutoa taarifa badaye.

# Wafugaji wavamia kambi hifadhini, wajeruhi askari

INATOKA UK. 3

kwamba tuliwaogopa, tulikuwa na silaha za moto zaidi ya tatu, lakini tuliamua kufanya busara ili kuepusha kutokea kwa maafa zaidi," alisema Eliudi.

Ofisa Msitu wa Hifadhi ya Pagale, Dk. Hamza Kateti, alisema uharibifu wote uliofanywa na wafugaji hao umeisababishia serikali hasara ya shilingi milioni 100 zikijumuisha kisima kilichokuwa kimechimbwa ambacho nacho kilifanyiwa uharibifu.

"Hawa wafugaji wamekuwa wakifanya uharibifu ndani ya Hifadhi ya Pagale. Licha ya kutoa elimu mara kwa mara juu ya umuhimu wa hifadhi hiyo, lakini wanakaidi na kutusababishia hasara, hivi sasa tumeamua kukamata hiyo mifugo na kuipiga faini kubwa," alisema Dk. Kateti.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Mwalimu Mohamed Utari, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kwamba ameshamwagiza Mkuu wa Polisi Wilaya hiyo, kuhakikisha anawasaka na kuwakamata wafugaji hao na kuwafikisha mahakamani ili liwe fundisho kwa wengine.

HABARI KITAIFA

# Mhasibu hospitali kortini kwa tuhuma za ubadhirifu

**Na Boniface Gideon,** TANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Tanga imemfikisha katika Mahakama ya Wilaya ya Handeni, aliyekuwa Mhasibu wa Hospitali ya Wilaya ya Handeni, Stephen Isaya Sanga, na kumfungulia kesi Namba 45/2019 kwa makosa ya ubadhirifu wa fedha.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Tanga, Christopher Mariba, alisema Sanga anashtakiwa kwa jumla ya makosa tisa ambapo manne kati ya hayo yanapatikana ndani ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu sura 16 R.E.2002 na makosa matano yaliyobaki ni ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007. Mariba aliongeza kuwa mhasibu huyo alipaswa kufikishwa mahakamani Novemba mwaka jana, lakini mtuhumiwa huyo alitoweka wilayani Handeni na kutokomea kusikojulikana.

Aliongeza kuwa baada ya kumtafuta kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, alipatikana Machi 24 na Machi 26 alifikishwa mahakamani.

Aliongeza kuwa mhasibu huyo kwa nyakati tofauti Oktoba 2014, alitengeneza na kuwasilisha stakabadhi za uongo kuwa amefanya malipo ya jumla ya shilingi 9,861,000 kwa huduma mbalimbali zilizotolewa katika mkutano wa wadau wa mradi wa chanjo ya surua, henia na matende ulioandaliwa na kuratibiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

Kwa mujibu wa Mariba, malipo yote aliyofanya Sanga hayakuwa ya kweli, na kwamba alitenda kosa la kughushi kinyume cha kifungu cha 333,335(a) na 337 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu sura ya 16 R.E.2002.

Aliongeza kuwa Sanga alitengeneza stakabadhi hizo na kuziwasilisha kwa mwajiri wake na kwamba alikuwa anatenda kosa chini ya kifungu cha 22 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007.

Kwamba kitendo cha kumdanganya mwajiri kwa stakabadhi zenye maelezo ya uongo, mhasibu huyo alifanikiwa kufanya ubadhirifu wa kiasi cha shilingi 9,861,900 kati ya shilingi 151,948,900 ambazo aliaminiwa na kukabidhiwa na halmashauri, na kwamba kwa kufanya hivyo alitenda kosa kinyume cha kifungu cha 28 (1) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

Kesi hiyo ipo chini ya Hakimu Anord Kileo na kuendeshwa na Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Anifa Kapinga, na iliahirishwa juzi Mei 2, mwaka huu, huku mtuhumiwa akiwa nje kwa dhamana.



Wanawake wakipepeta mahindi kabla ya kuyasaga kuwa unga katika mashine iliyopo eneo la Manzese, jijini Dar es Salaam juzi.
**PICHA: HALIMA KAMBI**

# Neema ya fidia kupisha umeme

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amesema wananchi waliopisha mradi wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme katika Kijiji cha Kidahwe wilayani Kigoma, watalipwa fidia kabla ya ujenzi kuanza.

Alisema hayo jana wakati za ziara ya kikazi wilayani Kigoma na Uvinza, ambapo alikagua eneo kutakapojengwa kituo cha kupoza umeme wa gridi ambao utatoka Tabora- Kigoma kwa msongo wa kV 132.

"Tunawapongeza wananchi kwa kupokea mradi huu kwa mikono miwili, lakini tunajua kuna wanaopaswa kulipwa fidia, ni haki yao ya msingi, hivyo hatutaanza ujenzi mpaka mtakapolipwa kwanza," alisema Dk. Kalemani.

Aliongeza serikali imetenga shilingi milioni 722 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi, na makadirio yameshafanyika na taratibu za uhakiki zinaendelea ili wananchi wapate kile wanachostahili.

Alisema wananchi watakaopisha njia hiyo ya umeme pia watalipwa fidia, na kwamba ujenzi utaanza wakati wowote baada ya malipo hayo kukamilika.

Akiwa wilayani Uvinza, Waziri wa Nishati alikagua kazi ya usambazaji umeme vijijini katika vijiji vya Kazuramimba na Nyanganga, mkandarasi kampuni ya CCCE Etern anaendelea na kazi.

Katika Kijiji cha Kazuramimba alikuta mafundi wakiendelea na kazi ya ufungaji wa transfoma, msimamizi wa mradi huo kutoka Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) alimweleza kuwa kazi hiyo ilitarajiwa kukamilika jana, na baada ya hapo wataanza kuunganishia umeme wananchi.

Akiwa katika Kijiji cha Nyanganga, Dk. Kalemani alimwagiza mkandarasi kuhakikisha kijiji hicho kinapata umeme Jumapili.

# Shule zapewa mil. 197/- kwa madarasa, samani

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imetoa Sh. milioni 197.5, kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, mabweni na samani katika shule za sekondari zilizopo wilayani Musoma.

Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vencent Anney, ameteja samani zitakazonunuliwa ni viti na meza kwa idadi ya 120 kila moja, pia vitanda 80 kwa ajili ya Shule ya Sekondari Mtiro iliyoko katika Kata ya Bukumi. Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, Dk. Anney alifafanua kuwa katika kiasi hicho cha fedha, Sh. milioni 135 zimetolewa kwa ajili ya Shule ya Sekondari Mtiro na Sh. 62.5 kwa ajili ya Sekondari ya Bugoji.

"Ufyatuaji matofali na uchimbaji wa msingi unaendelea katika Sekondari ya Mtiro kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 80," alisema.

Alisema wananchi wa Kata ya Bukumi wanajitolea kuhakikisha ujenzi wa sekondari unakamilika, na kila mmoja amekubali kuchangia shilingi 2,000 ili kugharimia usombaji wa maji na kulipa vibarua.

"Wameamua kushirikiana na serikali, hamasa ni kubwa kwa kuwa wanataka kuwaondolea watoto wao kero ya kutembea umbali mrefu kufuata elimu, bweni litasaidia wanafunzi wa kike kuepuka changamoto za mimba," alisema.

Aidha, alisema Kata ya Bugoji ambayo imepata Sh. milioni 62.5, wakazi wake wanaendelea na ujenzi wa sekondari yao kuhakikisha inaanza kupokea wanafunzi mwakani.

"Kwa sasa wanafunzi wa kata hiyo yenye vijiji vitatu vya Kaburabura, Kanderema na Bugoji wanasoma katika sekondari ya kata jirani ya Nyambono," alisema.

Alisema ujenzi wa sekondari hiyo ulianza Desemba 2018, unafanywa kwa nguvu za wananchi, serikali na wadau wa elimu na kwamba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) imetoa Sh. milioni 62.5, ambazo zitakamilisha ujenzi wa madarasa matano.

Alisema boma la vyumba viwili limekamilika na kinachofuata ni kupaua baada ya kukamilisha ujenzi wa ofisi ya mkuu wa shule na makamu wake.

"Boma lingine la vyumba viwili na ofisi moja, wanafunga renta, huku wakiendelea na ufyatuaji wa matofali ili kuanza ujenzi wa vyumba vingine vya madarasa na nyumba ya kuishi walimu," alisema.

# Huduma kidigitali sasa asilimia 90

**Na Salome Kitomari**

ASILIMIA 90 ya huduma za afya kwa mfumo wa kielektroniki (E-health) zimekubalika kwa watoa huduma za afya na kurahisisha utoaji na ufikishaji wa taarifa kwa wananchi.

Akiwasilisha mada jijini Dar es Salaam juu ya matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama) kwenye huduma za afya Tanzania, Ofisa Tehama wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Sultana Seif, alisema wamekamilisha miongozo iliyowezesha matumizi ya teknolojia kwenye huduma za afya.

Alisema mwaka 2015 watumishi wengi wa huduma za afya hawakukubali utoaji huduma kwa 'E-health', lakini baada ya kupewa mafunzo na kuelewa faida walikubali na kuwezesha kusambaa nchi nzima.

Miongozo hiyo, alisema imekuja ili kutoa mwelekeo wa pamoja wa matumizi ya teknolojia kwenye huduma za afya, kuliko kuacha kila mtu kufanya anavyoweza na mwishowe kuiweka nchi uchi kwa kutoa data mbalimbali ambazo haziruhusiwi.

"Kwa ujumla vitu vingi vinavyoendelea katika kusaidia utekelezaji wa sera ya afya, vinafanywa kwa njia ya teknolojia mfano elimu ya afya tunafanya kwa kutumia mitandao ya kijamii, hali ya huduma za afya kielektroniki ipo katika asilimia 70 kwa sasa," alisema.

Alisema awali watoa hudumu waliona shida kutumia kompyuta kutokana na mazoea ya kutumia karatasi, na kwamba kwa sasa wanajivunia kwa kuwa imewezesha ufuatiliaji wa karibu wa huduma za afya nchini.

"Kwa sasa ni rahisi kufuatilia masuala ya dawa, wafanyakazi, mfano unaweza kusikia wananchi wanalalamika hakuna dawa sehemu fulani ni rahisi kuangalia kwenye mfumo kiasi cha dawa kilichopelekwa kwenye eneo husika," alisema Seif.

Alisema kuna maeneo ilikuwa ni ngumu huduma kufika, lakini kupitia teknolojia wamewafikia wananchi kiurahisi na sasa wanapata taarifa za afya kupitia simu za mkononi.

"Kijiji cha Ololosokwani wanatumia mfumo wa digitali kwenye huduma za afya, pia hivi karibuni eneo la Mafia mama mjamzito alipata tatizo wakati wa kujifungua na daktari aliwasiliana kwa simu na daktari mwingine aliyepo Muhimbili na walifanikiwa kuokoa maisha ya mama yule," alibainisha.

Naye Mkurugenzi wa Ufundi wa Mfuko wa Ubunifu kwa Maendeleo ya Binadamu (HDIF), Muzafar Kaembil, alisema wamewaleta pamoja serikali na watekelezaji kujadili namna wanavyoweza kushirikiana kuwa na huduma bora za afya kwa kutumia Tehama. "Serikali tayari ina 'E Health' ya kuweka mifumo ya habari kwa ajili ya sekta ya afya, lakini changamoto ni wadau zaidi ya mmoja kufanya kitu kimoja kwenye maeneo tofauti, inahitajika kuwa na eneo linalowakusanya pamoja ili kuondoa mkanganyiko," alisema.

Awali, Meneja Programu wa Shirika lisilo la kiserikali la Amref, Serafina Mkuwa, alisema ndani ya serikali kuna mabadiliko makubwa kwenye E health kwa kuondoka kwenye kutumia karatasi na kutumia simu na kompyuta jambo ambalo litawezesha huduma kuwafikia wananchi kirahisi.

Alisema Amref inatekeleza shughuli za utoaji huduma kwa afya ya uzazi kwa mama, watoto na vijana kwenye mikoa ya Shinyanga na Geita, na kwamba uwepo wa miongozo ya utoaji huduma kwa kutumia mfumo wa kidijitali utasaidia.



Mchuuzi wa maembe akiwa kwenye harakati za kutafuta wateja katika Barabara ya Nyerere, akielekea katikati ya Jiji la Dar es Salaam jana.
**PICHA: JOHN BADI**

## Mitambo kubaini wahalifu JNIA mbioni kukamilika

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

MITAMBO ya kubaini wahalifu katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam inakaribia kukamilika ili ikabidhiwe.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mhandisi Isaack Kamwele, wakati akifungua Baraza la Wafanyakazi wa wizara hiyo.

Kamwele alisema mitambo hiyo inatarajia kukabidhiwa wakati wowote kabla ya kuanza kutumika. Aidha, alisema mitambo hiyo itasaidia kukamata wahalifu ambao watabainika wanafanya uhalifu ndani ya uwanja.

Alifafanua zaidi kuwa lengo la kufunga mitambo ni kutaka kuweka usalama katika uwanja huo.

Katika hatua nyingine, alilitaka baraza hilo kuchapa kazi ili kufika mbali katika utendaji.

Alisema yeye kama waziri anafurahi kuona wafanyakazi wanajituma badala ya kukaa na kubweteka.

Aliongeza kuwa mtu atakayekuwa mtendaji mzuri na mbunifu, basi atakuwa rafiki yake kutokana kwa kuwa wanahitaji watu wabunifu. Alisema lengo ni kuona kila mmoja anawajibika na si kusubiri posho ya ofisini. Mwenyekiti wa Baraza hilo, Erick Mwakalinga, aliwataka washiriki kuwa makini na kile wanachojadili na kutobweteka.

Alifafanua kuwa kila mfanyakazi alitendee haki baraza hilo kutokana na kujadili mambo muhimu. Kadhalika, walifanya uchaguzi wa viongozi na kupata wapya.

Alisema wafanyakazi wanapaswa kushirikiana na si kila mmoja kufanya kazi kivyake, kitu ambacho hakileti maana.

## Mapya yabainishwa ukatili watoto wa kike

**Na Consolata Evarist,** GEITA

WATOTO wa kike mkoani Geita, wameendelea kukumbana na changamoto nyingi katika jitihada za kufikia ndoto zao ikiwamo kukosa fursa ya masomo kutokana na kuwapo kwa vitendo vya ubaguzi wa kijinsia.

Hayo yalibainishwa jana na Meneja wa Shirika lisilo la kiserikali la Plan International, Marcely Madubi, alipokuwa akitoa taarifa ya vitendo vya ukatili kwenye kikao cha wadau wa kujadili mkakati shirikishi wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Kwamba imebainika bado watoto wa kike wanakumbwa na adha hiyo kutokana na uelewa mdogo wa wazazi na walezi na kwamba pia kumekuwa na mimba nyingi za utotoni ambazo ni tatizo kubwa, kwa kipindi cha mwaka jana, zaidi ya mimba 300 zimeripotiwa kutokea.

Alisema mkoa wa Geita umeendelea kukumbwa na tatizo kubwa la kuwapo kwa mimba za utotoni ambazo zimekuwa zikichochea kwa kiasi kikubwa wanafunzi wa kike kushindwa kufikia malengo.

Alisema wazazi wengi wamekuwa wakiwaacha wanafunzi wa kike kuishi kwenye nyumba za kupanga kwa madai ya kukaa karibu na mazingira ya shule wakati watoto hao bado wanahitaji uangalizi wa karibu kutoka kwa mzazi.

"Watoto wengi ambao tumeshawahi kuzungumza nao na kuona mazingira wanayotoka wengi wao wanasema ni ugumu wa maisha ya familia ndio chanzo kikubwa kinachowapelekea kujikuta wakiingia kwenye uhusiano na mwisho wa siku kupatiwa ujauzito," alisema Madubi.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita, Elikana Haruni, aliwasihi viongozi wa dini kutoa elimu juu ya vitendo vya ukatili kwa waumini wao.

"Tunaamini viongozi wa dini wakisimama kwa pamoja na serikali kutoa elimu juu ya vitendo hivi vya ukatili watakuwa wamesaidia kwa nafasi kubwa kupunguza matukio ambayo yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara na kusababisha kuwanyima haki wanawake na watoto,"

# Wafanyabiashara wa madini watamani wataalamu wa nje

**Na Novatus Makunga,**
ARUSHA

MWENYEKITI wa Chama cha Wafanyabiashara, Wanunuzi na Wauzaji wa Madini nchini (Tamida), Sammy Mollel, amesema Tanzania haina wataalamu wa kutosha wa kusanifu madini.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake jana, Mollel aliiomba serikali kuondoa urasimu katika utoaji wa vibali vya ajira pale wanapotaka kuleta wataalamu wa kigeni wa kusanifu madini. Alisema hivi sasa taratibu za kuomba vibali vya kuajiri wataalamu wa kigeni zinachukuwa mpaka miaka miwili kuweza kupata vibali.

Aliongeza nchi inahitaji wataalamu wa hali ya juu katika ukataji, ung'arishaji na usanifu wa madini kutoka nchi zenye wabobezi hususani Sri-Lanka ili wasaidie kuleta teknolojia na kuacha ujuzi kwa Watanzania.

"Sisi kama Tamida tuna ushirikiano na wenzetu wa Sri-Lanka Gem and Security Authority tangu mwaka 1996 wenye lengo la kukuza sekta ya madini ya vito na tumekuwa tukifanya maonyesho mbalimbali hivyo ni rahisi kupata wataalamu wabobezi," alisema.

Alisema suala la utaalamu wa kukata, kung'arisha na kusanifu madini ya vito halihitaji kuwa na shahada bali ni suala linalohitaji kipaji cha mtu mwenyewe katika kazi hiyo.

"Ni sawa na uchongaji wa vinyago, ambapo kila mtu hapa nchini anafahamu wenye kipaji hicho ni Wamakonde, lakini ukienda nchi jirani ya Kenya wakataji, wang'arishaji na wasanifu wa madini ni Wakamba, lakini duniani Sri-Lanka ndiyo wapo juu zaidi," alifafanua.

Alitaja madini kama rubi na sapphire kuwa yanahitaji utaalamu wa hali ya juu na mashine za kipekee hasa katika uchomaji, ambapo alieleza kwa hapa nchini utaalamu wake haupo.

"Uchomaji wake unahitaji nyuzi joto zaidi ya 1,000 na umeme wa uhakika, kitendo chochote cha kukosea ni moja kwa moja unaingia katika hasara kwa madini kuharibika na kutokuuzika tena," alifafanua Mollel.

Alisema hivi sasa nchi nzima ina mashine za kukata na kusanifu madini zisiozidi 300 ambazo kwa wastani zinauwezo wa kusanifu madini yasiozidi kilo moja kwa siku.

"Mfano uzalishaji wa madini ya tanzanite pale Mirerani kwa siku ni zaidi ya kilo tatu, huku madini ya rhodolite ikiwa ni zaidi ya tani moja kule Tanga, sasa kwa hizi mashine na wakataji waliopo unadhani unaweza kumaliza kwa siku ngapi ukichanganya na madini mengine yanayopatikana maeneo mbalimbali nchini," alifafanua.

Aidha, aliomba serikali iondoe Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na ushuru wa forodha kwa mashine za kusanifu, kung'arisha na kukata madini ya vito. Mollel alisema kwa mashine zinazoagizwa kutoka nchini Thailand huuzwa kwa dola za Marekani kati ya 300 na 500 na zile kutoka Marekani ni dola kati ya 3000 na 6000.

Alisema katika kuunga mkono mkakati wa Rais John Magufuli wa Tanzania ya viwanda, nchi haina budi kuleta wataalamu kutoka nchi zilizoendelea kwa teknolojia na baadaye waweze kuwaachia Watanzania utaalamu katika usanifu wa madini ya vito. "Ni lazima tumsaidie Rais kwa jitihada zake na kamwe zisikwamishwe ili tuweze kufikia uchumi wa kati ifikapo 2025, ambapo mkazo mkubwa na kuwa na viwanda vya kutosha," alisema.

Mollel alipongeza hatua ya Rais Magufuli ya kukutana na wadau wa madini Januari 21 na 22 mwaka huu, jijini Dar es Salaam na hatimaye kuwakubalia kilio chao cha muda mrefu cha kusafirisha nje ya nchi madini ghafi ya tanzanite yenye uzito wa chini ya gramu moja kutokana na kukosekana kwa teknolojia ya kuyasanifu na kuyaongezea thamani hapa nchini.

Aidha, Mollel alipongeza hatua ya Rais Magufuli kuridhia na kuupeleka kwa hati ya dharura muswaada wa marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, (VAT), ya asilimia 18 na sheria ya zuio ya asilimia 5 (Witholding Tax) ambapo tayari zilishapitishwa na bunge na kusainiwa kuwa sheria.

Sheria ya Madini Namba 14 ya Mwaka 2010 inasisitiza kwamba madini yote yanayopatikana nchini ni lazima yasanifiwe kabla ya kusafirishwa na kuuzwa nje ya nchi.

Baadhi ya madini ya vito yanayopatikana hapa nchini ni pamoja na tanzanite, sapphire, emarald, tourmaline, aguamarine, zircon, garnet, aqrnethyst, rhodolite na alexandrite.



Mwenyekiti wa chama cha wachimbaji madini Mkoa wa Manyara (Marema), Justin Nyari, akifunga mafunzo ya siku mbili ya wadau wa madini yaliyofanyika Mji Mdogo wa Mirerani na kuandaliwa na Tume ya Madini jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mkandarasi aomba kulipwa madeni miradi

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

MKANDARASI anayetekeleza ujenzi wa miradi wa maji mkoani hapo, ameiomba serikali kulipa madeni ili aweze kukamilisha miradi ambayo inatakiwa kukamilishwa kwa wakati ili wananchi wapate maji.

Mkandarasi huyo wa kampuni ya Black Lion Investmest, John Festo Makune, alitoa ombi hilo wakati akizungumza na Nipashe kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji.

Alisema kuchelewa kupata fedha kunasababisha kukwama kwa utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati.

Aliongeza kuwa miongoni mwa miradi ambayo ameingia mkataba na serikali ni mradi wa maji wa Kijiji cha Imbilili uliopo Halmashauri ya Mji wa Babati ambao una thamani ya shilingi milioni 487 na ameshalipwa shilingi milioni 30.

Alisema fedha hizo alilipwa mwaka jana, lakini mradi huo bado haujakamilika kutokana na kusuasua kwa malipo.

Licha ya ucheleweshaji wa malipo, mkandarasi hiyo alisema mradi huo umetekelezwa kwa asilimia 75, hivyo ameomba alipwe ili akamilishe kazi yake.

Mradi mwingine ni wa Mwankoko B uliopo Manispaa ya Singida uliotekelezwa na kampuni yake ya Kwirasa Investment, wenye thamani ya shilingi milioni 702 bila kodi ya ongezeko la thamani (Vat), ambapo alisema alilipwa shilingi milioni 650 na bado anadai Sh. milioni 46 na mifereji Sh. milioni 15, ambapo alijenga pia tangi na dip 12.

Alisema mradi huo ulikuwa wa mwaka wa fedha 2014/15 mpaka 2015/16.

Mradi mwingine tena wa maji ni ule uliopo Kijiji cha Kazi Ngumu katika Halmashauri ya Kiteto ambao mkandarasi ni kampuni ya Kwilasa Investment wenye thamani ya shilingi milioni 176.

Aliiomba serikali kumlipa fedha ili aweze kukamilisha ujenzi wa miradi hiyo ya maji ambayo ikikamilika itakuwa mkombozi kwa wananchi wanaoishi maeneo hayo.

Kilio cha makandarasi hao kimekuja siku moja baada ya Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda ambaye ni mlezi wa CCM Mkoa wa Manyara, kuwa katika ziara ya siku nane kukagua utekelezaji wa ilani ya chama hicho, ambapo alibaini kukwama kwa miradi ya maji kutokana na ukosefu wa fedha.

# DC 'awapa vidonge' wachimbaji madini

**Na Mwandishi Wetu,** SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, amesema pamoja na Rais John Magufuli kuondoa kodi na kero zote za sekta ya madini bado baadhi ya wachimbaji madini wanashindwa kutimiza wajibu wao na wanataka kusukumwa na serikali.

Alisema hayo juzi kwenye semina ya siku mbili ya wadau wa madini wilayani hapa ambayo ilizinduliwa na Tume ya Madini na kufanyika Mji Mdogo wa Mirerani.

Alisema baadhi ya wachimbaji madini hawatunzi taarifa za ufanyaji kazi na uzalishaji kwenye migodi yao, hivyo kuwapo na sintofahamu juu ya malengo yao.

Chaula alisema anataka siku moja wachimbaji wa wilaya hiyo wapewe sifa kwa kufanya mambo mazuri ikiwamo kuchimba kwa usalama na kulipa kodi inayostahili.

"Rais Magufuli ataendelea kuwasaidia mengi zaidi, lakini tuonyeshe mfano kwa hayo machache aliyoanza nayo kwenye sekta ya madini ili muwe mfano bora tofauti na wachimbaji wengine nchini," alisema.

Kwa upande wake, Mhandisi wa Migodi wa Tume ya Madini, Laurent Mayala, alisema mafunzo hayo yanahusisha uchimbaji salama wa kuepuka ajali na vifo migodini.

Alisema wachimbaji hao wameelezwa kufahamu namna bora ya kufikisha hewa safi mgodini na utoaji wa udongo migodini.

Alitaja nyingine ni namna bora ya kuchoronga bila kudhuru afya kwa kuzuia na kupunguza vumbi ikiwamo kuepuka ugonjwa wa kifua kikuu na silikosis, ulipuaji baruti wenye tija na kuzuia ngema.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa kimadini wa Simanjiro, Daudi Ntalima, alisema mafunzo hayo yamefanyika kupitia mpango wa Tume ya Madini ya kuwezesha mafunzo ya wachimbaji kupitia ofisi za mikoani.

Alisema faida ya mafunzo hayo ni kupunguza vifo migodini kwa uzembe, usalama migodini kwenye magonjwa na kufuata sheria za uchimbaji madini.

Mchimbaji wa madini ya green kwenye machimbo ya Lemshuku, Bernald Kasanu, alisema mafunzo hayo yamewajengea uwezo zaidi wachimbaji katika kuchimba madini kwa usalama.

Naye mchimbaji wa madini ya tanzanite, Rachel Njau, alipongeza serikali kwa kufanikisha mafunzo hayo na kushauri yawe yanafanyika kila mara ili kuwakumbusha wachimbaji.



Wananchi wa Machame ambao ni wanachama wa Chama cha Ushirika wa Mazao cha Lyamungo Amcos, wakimsindikiza Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, kwa majani maalumu yanayoheshimika kwa mila za Wachaga 'masale', baada ya kutatua mgogoro wa ardhi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Serikali yashauriwa kutenga bajeti kusaidia wanaopokwa haki zao

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

IDADI ya wakulima na wafugaji walioko vijiji vya pembezoni katika eneo la Moshi Vijijini ambao hawajafikiwa lakini wanapitia aina nyingi za ukatili ikiwamo kupokwa haki zao na wajanja kwa sababu ya kukosa uelewa wa sheria mbalimbali zinazowalinda, imetajwa kuwa bado ni changamoto.

Kutokana na changamoto hiyo, msaidizi wa kisheria eneo hilo la Moshi Vijijini, Quider Mwanga, ameishauri Wizara ya Katiba na Sheria kutenga ruzuku maalum katika bajeti yake ya mwaka 2019/2020 kwa ajili ya kuwezesha kada hiyo kuwafikia wananchi wengi zaidi ambao wanapitia aina zote za uminywaji wa haki katika ngazi ya kaya na kutoa ushauri wa kuvifikia vyombo vingine vya maamuzi.

"Wachache waliosikia kuna watu wanaitwa wasaidizi wa kisheria na wanasaidia watu, wapo wananchi hasa kinamama wanaotoka TPC na Arusha Chini umbali wa zaidi ya kilomita 30 wanakuja kutafuta huduma Moshi. Hatujaweza kusogea huko pembezoni kwa sababu kipato chetu ni kidogo na tunahitaji fungu kwa ajili ya kufanya kazi hiyo," alisema. Wasaidizi wa kisheria maana yake ni watu wanatoa huduma ya msaada wa kisheria kupitia mtoa huduma ya msaada wa kisheria.

Wakili maarufu na Mkurugenzi wa Shirika la Kilimanjaro Women Information Exchange and Community Organization (Kwieco), Elizabeth Minde, ameeleza kuwa wameanza kuchukua hatua zinazofaa kuhamasisha elimu ya sheria na kuongeza uelewa katika jamii na hasa kuelimisha makundi maalumu katika jamii kuhusu haki na wajibu wao kwa mujibu wa katiba na sheria nyingine.

Akizungumzia umuhimu wa kutumika kwa wasaidizi hao wa kisheria, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Arusha Chini (WEO), Emmanuel Mosha, alisema: "Kinachotusumbua hasa vijijini ni migogoro ya ardhi inayoanzishwa na baadhi ya wachochezi, sasa kupitia elimu hii nadhani tutafanikiwa kuimaliza migogoro ya ardhi, ndoa, mirathi, umiliki wa mali kwa kufanya usuluhishi huko walipo wananchi."

Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, alisema kuwatumia wasaidizi wa sheria kutapunguza muda unaotumika mahakamani na watu wengi hasa wanasheria na mawakili wamekuwa na mtizamo hasi na hata kufikia kuwapiga vita.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa kusogeza huduma karibu na wananchi, sheria imeweka wasajili wasaidizi katika ngazi za halmashauri ambao watakuwa wakishirikiana na wasaidizi wa kisheria maeneo hayo.

# Halmashauri yadaiwa kukiuka agizo la Lukuvi

**Na Mary Mosha,** SAME

WENYEVITI wa Serikali za Vijiji vya Ndungu, Msufini na Mpirani katika Wilaya ya Same wameitupia lawama Halmashauri ya Wilaya hiyo kwa kushindwa kutekeleza agizo la Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wiliam Lukuvi, la kuwapatia eneo la ekari 100.

Ardhi hiyo ilipaswa kumegwa katika shamba la katani la Kampuni ya L.M Investment, kwa mujibu wa wenyeviti hao.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ndungu, Paul Gilbert, akitoa malalamiko hayo jana, alisema licha ya wao kwa umoja wao kufuatilia suala hilo katika ngazi ya wilaya, hakuna jitihada zozote zilizochukuliwa hadi sasa.

"Agizo hilo la Waziri Lukuvi lilitakiwa kutekelezwa ndani ya siku 60 na lilitolewa Oktoba mwaka jana, lakini hakuna kilichotekelezeka na wala hakuna mrejesho tuliopewa, siku 60 zimepita na leo ni zaidi ya siku ya 150," alisema.

Alisema hali hii inaonyesha kuwa wananchi hawawezi kupata haki zao, kwa kuwa watendaji wamekuwa wakitupiana mpira, licha ya kuwa ni agizo la waziri.

"Kucheleweshwa kutekeleza kwa agizo hili kunachelewesha maendeleo, msimu wa kilimo wa masika unaendelea wakati wananchi wameweza kuchukuwa maeneo hayo na kulima ili kujiepusha na hatari ya baa la njaa," alisema Juma Hemed ambaye ni mwakilishi kutoka Kijiji cha Mpirani.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alipotafutwa kuzungumzia malalamiko hayo alieleza; "Hili ni suala la kutekeleza agizo la Waziri Lukuvi na si kurushiana mpira, nitalifuatilia kwa ukaribu kujua kwa nini miezi yote mitano imepita."

Kamisha wa Ardhi, Kanda ya Kaskazini, Leo Komba, alipoulizwa alikiri kusuasua kwa utekelezaji wa agizo la Waziri Lukuvi, akisema, "Tunaendelea na ufuatiliaji katika kuhakikisha tunamaliza kuzungumkuti kilichopo kwa kufuatilia wapi agizo hilo limekwamia."

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa shamba hilo, Alan Abas, aliimbia Nipashe kuwa anasikitika kuwa tayari walishalipa gharama za upimaji wa shamba hilo lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea.

"Waziri Lukuvi alitoa miezi miwili shamba hilo liweze kupimwa na sisi tuliandikiwa barua ya kututaka tulipie fedha kiasi cha milioni 4.9 kwa ajili ya upimaji, lakini hadi sasa hakuna kinachoendelea na kinatuadhiri kwa kuwa hakuna uzalishaji unaoendelea, hivyo tunaomba mamlaka husika kuharakisha zoezi hilo la upimaji," alisema.

# Mhagama atoa angalizo kwa vijana

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KUMBUKIZI ya miaka 20 ya kifo cha Rais wa kwanza wa Tanzania, hayati Mwalimu Julius Nyerere imemwibua Waziri wa Nchi, Ofsi ya Waziri Mkuu, (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, kuanza kuhubiri juu ya vijana kuacha kutumiwa vibaya na watu wasio na mapenzi mema ambao wanalipaka matope taifa.

Waziri Mhagama ametoa onyo hilo jana, alipokuwa akikabidhi bendera ya taifa kwa vijana 16 wanaopanda kilele cha Uhuru cha Mlima Kilimanjaro, kusimika bendera hiyo wakati Mwenge wa Uhuru utakapowashwa rasmi Aprili 2, mwaka huu, katika Mkoa wa Songwe.

"Vijana acheni kutumiwa na watu wasio na mapenzi mwema na taifa hili, maadili yamepungua katika jamii hasa kwa vijana kumekuwapo na wengi wanaotumia dawa za kulevya, hatutawavumilia vijana wa namna hiyo kwa sababu wapo tayari kurubuniwa ili kulichafua taifa," alisema waziri huyo.

Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, huhitimishwa Oktoba 14 kila mwaka kwa ajili ya kumuenzi Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Julius Nyerere aliyefariki dunia mwaka 1999 katika Hospitali ya St. Thomas nchini Uingereza.

Alisema wameanza kumbukizi hiyo kwa kuwahamasisha vijana kuacha kutumika kulibomoa taifa na kuwa mstari wa mbele kulipigania taifa.

Awali, Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Kippi Warioba, akizungumza kabla ya waziri huyo, aliwataka vijana kuanza kupekua vitabu vya kihistoria ili kufahamu baba wa taifa na nini alichokifanya katika taifa linalomuenzi leo na kuiga matendo yake.

Mkurugenzi wa Maendeleo wa Vijana kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, James Kajugusi, alisema wamejipanga kuhakikisha wanawafanya vijana kuwa chachu ya mabadiliko katika kulipigania taifa.

Alisema imefika wakati vijana kujitambua, kufanya kazi kwa kujituma, kuacha matumizi ya dawa za kulevya pamoja na kuilinda nchi kwa matendo, huku wakiipeleka kwenye uchumi wa viwanda.

Akipokea bendera hiyo, kiongozi wa vijana hao Musa Mwanja alisema, "Tumepokea bendera hii vijana 16 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Visiwani, tutatanguliza Tanzania kwanza bila kujali, dini zetu, kabila zetu na afya zetu... kwa mbinu mbalimbali lengo likiwa ni kuhakikisha bendera inafika kileleni kama Watanzania walivyotupa dhamana."

# ama

ALHAMISI MACHI 28, 2019

AFYA NA MAZINGIRA



Watoto Kagera katika hali mbaya, wenye utapiamlo idadi inatisha

Ukurasa 14



Skauti wahamia ufukweni kukabili uchafu uliokithiri

Ukurasa 18



**UNAIJUA NAWEZA?** Mkakati unaosuka upya mwelekeo kukabili magonjwa hatari nchini

Ukurasa 19



**Wanaunguzwa matiti wasivutie wanaume**

Ukurasa 20



# Waziri Hasunga: Sumu kuvu yatafuna mazao na uhai wetu

Ukurasa 16



Tohara ikifanyika. **PICHA: MTANDAO.**

## Aliyetahiriwa nyumbani afa, serikali yachachamaa

**ROMA,** Italia

MTOTO wa miezi mitano aliyefanyiwa tohara nyumbani kwao amefariki, serikali nchini imetangaza, huku ikicharukia tukio hilo.

Sasa imeamua kulishikia 'bango' suala hilo, baada ya mtoto kufikishwa hospitali na kufariki muda mfupi baadaye akiwa na hali mbaya sana, Ijumaa iliyopita .

Hata hivyo, inaelezwa nchini Italia kunaendekezwa tabia za kienyeji majumbani, kufikia idadi ya 5,000 kwa mwaka, mamlaka za afya zimeeleza.

Kiafya inaelezwa kuwa tendo hilo ni muhimu kufanyika hospitali, kwani daktari ana nafasi yake katika kutoa ridhaa na usimamizi wa utelelezwaji wake wa kurejea vigezo vya kitaalamu kiafya.

Nchini Uingereza kunakadiriwa kwamba tohara za kienyeji zinafanyika katika wastani wa asilimia 10 ya watoto wote.

Katika nchi nyingi za Kiafrika na hata kwingineko, tendo hilo kinafanywa na baadhi ya njia za kieyeji kutumia makundi na miongozo za kimila, ikisimamiwa na wanaoaminika wataalamu wa jadi wa kutahiri

Nchini Ujerumani mwaka 2012, Mahakama katika hukumu yake ilitangaza marufuku ya kisheria, tendo hilo kufanyika, baada ya kijana wa miaka minne kuhudhuriwa vibaya kiafya, katika tohara iliyosimamiwa na miongozo ya kidini..

**BBC.**

AFYA

# Watoto Kagera katika hali mbaya, wenye utapiamlo idadi inatisha

## • Asasi Ima World Health yajitosa kuwanusuru

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA



Kinamama wakiwalisha watoto, baada ya kufundishwa namna ya kuandaa chakula cha watoto. **PICHA: LILIAN LUGAKINGIRA.**

MKOA wa Kagera unatajwa kuwa na watoto umri wa chini ya miaka mitano waliodumaa asilimia 41.7, kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2016, uliofanywa na taasisi ya Tanzania Demographic Survey (TDS).

Kagera inaundwa na wilaya saba, ikiwamo Missenyi, ambako katika vijiji viwili; Buchurago na Bugorora, kulifanyika upimaji na wakagundulika watoto 535, ambao ni asilimia 16 wana utapiamlo. Kati yao 51 wana utapiamlo wa kadri na 35 mkali.

Pia, katika kijiji cha Kashaba wilayani Kyaka, walipimwa watoto 250 na 81(asilimia 36) waliogundulika kuwa na utapiamlo wa kadri na tisa utapiamlo mkali.

**Kwanini hivyo?**

Sababu zinazochangia, zinatajwa kuwa ni wazazi kutokujua kuandaa chakula cha watoto wao na Dk. Mussa Abdallah, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Missenyi, anasema kuna maeneo walikobaini lishe duni na anafafanua:

"Kuanzia zile siku 1,000 (miezi mitatu na siku 10) tangu mimba inapotungwa, hadi mtoto anapofikisha miaka miwili, ni siku muhimu sana kwa afya ya mtoto, kwa sababu ni kipindi ambacho ubongo unatengenezwa na kuna virutubisho ambavyo vinahitajika, ili kuweka ubongo imara kwa ajili ya baadaye."

Dk. Abdallah, anasema uelewa wa mtoto shuleni hutegemea kiwango chake cha lishe katika kipindi hicho na kinga ya mwili dhidi ya magonjwa.

Anasema Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi, ilichukua hatua kuhakikisha elimu inaifikia jamii kwa njia mbalimbali, ikiwamo kuwekeza wahudumu wa afya ya jamii wawili katika kila kijiji. Wilayani wapo 154.

Mganga huyo anasisitiza umuhimu wa mtoto kunyonyeshwa maziwa ya mama pekee kwa kipindi cha miezi sita bila kuchanganyiwa vyakula vingine, huku akitaja vijiji vya Buchurago na Bugorora, ndiyo vina hali mbaya zaidi.

"Wanafundishwa namna ya kutumia vyakula ambavyo vinapatikana kwenye jamii husika, ambavyo vikichanganywa inavyotakiwa, akapewa mtoto vinaweza kuimarisha lishe," anasema.

> "Watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano waliobainika kuwa na upungufu wa damu ni 99 sawa na asilimia 0.6 ya watoto 14,750 waliofika kutibiwa katika vituo vya kutolea huduma za afya, lakini watoto waliolazwa kutokana na tatizo la upungufu wa damu ni 57,"

Pia, wanawapima watoto kupitia vituo vya huduma za afya, ikiendana na kufanyika vikao vya kamati za lishe za wilaya

Dk. Abdallah anavitaja vyakula muhimu ni mchanganyiko wa karanga, mchicha, ndizi, maharage na dagaa na kwenye wenye uwezo kununua samaki, nyama hasa maini, mayai na maziwa wanashirikiana na Idara ya Kilimo kutoa mafunzo ya ulimaji viazi na maharage lishe.

Pia, anawashukuru wadau, wakiwamo shirika la IMA World Health kupitia Mradi wa Mtoto Mwerevu, kwa ufadhili wa mradi kwa Shilingi milioni 77.

Pia, Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi, katika bajeti yake kila mtoto anatengewa Sh. 1000 na Dk. Abdallah anafafanua: "Ni kwa ajili ya kusimamia masuala ya utoaji wa elimu ya mambo ya lishe kwa watoto kwenye jamii."

DK. Abdallah analalamika kwamba bado elimu haitoi matunda stahiki, kwa sababu bado wataalamu wa afya ndio wanawaibua watoto wenye utapiamlo kliniki

Gratian Kajuna, ni Mhudumu Afya Ngazi ya Jamii kijijini Kilimilile, anasema baada ya elimu kupitia mashirika mbalimbalii, walianza kijijini hapo na kinamama. Anafafanua:

"Tulianza kuwafundisha wananchi kwa nadharia na baadaye vitendo, tukiwaonyesha namna wanavyoweza kuandaa na kuchanganya vyakula vinavyojenga lishe ya watoto, huku wananchi wanaoshindwa kupata vyakula hivyo wakichangiwa na wenzao."

Anasema, wanawapima watoto na wenye uzito pungufu, pamoja na wazazi wao wanatengwa na kupewa elimu, wanaofunzwa uandaaji chakula cha watoto kuhakikisha afya inaimarika.

"Gharama za wahudumu wa afya ngazi ya jamii za kuzunguka katika vitongoji na vijiji kutoa elimu kwa jamii, hutolewa na (taasisi) ya World Vision na wananchi wameonekana kuwa na mwamko mkubwa wa kujifunza hasa wanawake," anasema Kajuna.

Huku akirejea mwaka 2017, ukame uliteteresha afya ya wengi waliojikimu na njaa kwa kula maembe na anasema vituo vya kuhamasisha wananchi kupima watoto na wajawazito ndiko kunakotolewa dawa za minyoo na vitamin, chini ya usimamizi wa serikali.

**Ofisa Ustawi Jamii**

Ofisa Ustawi wa Jamii katika Wilaya ya Missenyi, Anord Nkongoki,

Inaendelea Uk.15

AFYA



**JUU NA CHINI:** Kinamama wakifundishwa kupika chakula cha watoto. **PICHA ZOTE: LILIAN LUGAKINGIRA.**

# Watoto Kagera katika hali mbaya

**Inaendelea Uk.14**

anasema kati ya Januari na Oktoba mwaka jana, kulikuwapo watoto wanaonyonya maziwa ya mama ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa; 5,505 au asilimia 89 ya watoto hao, ikiashiria dalili njema.

Anataja kiashiria kingine ni watoto wanaozaliwa chini ya uzito kilo 2.5 wako 214 au asilimia 3.4 na wajawazito waliobainika kuwa na upungufu wa damu chini ya gramu nane ni asilimia 1.2 ya wanawake 5,374.

"Watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano waliobainika kuwa na upungufu wa damu ni 99 sawa na asilimia 0.6 ya watoto 14,750 waliofika kutibiwa katika vituo vya kutolea huduma za afya, lakini watoto waliolazwa kutokana na tatizo la upungufu wa damu ni 57," anasema Nkongoki.

Aidha, anasema watoto wenye umri kuanzia miezi sita hadi 56 waliopatiwa matone ya vitamin A katika wilaya hiyo ni 34,094 sawa na asilimia 94 ya watoto 36,216 waliolengwa.

"Watoto waliolazwa katika Hospitali ya Mugana ambayo ni Hospitali Teule ya Wilaya ya Missenyi wakisumbuliwa na tatizo la utapiamlo ni 499 na kati ya hawa waliokuwa wakitibiwa utapiamlo mkali ni 13 ambao ni sawa na asilimia 2.6," anafafanua.

Anataja mipango mingine ni kuweka kambi ya wiki tatu katika maeneo yatakayobainika kuwa na watoto wengi wenye utapiamlo na kumazishwa wodi maalumu katika Kituo cha Afya Bunazi.

### Ofisa Fao

Julius Sonoko, ni Mwakilishi wa Shirika la Chakula Duniani (FAO) mkaoni Kagera, anayesema kuna mradi wa ndizi wa mkoa unaofanyiwa kazi wenye viini lishe zaidi, ikilinganishwa na ndizi nyingine na zenye kiwango kikubwa cha Vitamin A.

"Tatizo la upungufu au ukosefu wa vitamin A ni kubwa na linaathiri watoto na kinamama ambao wako katika umri wa kujifungua," anasema Sonoko, akifafanua ni lishe rahisi kufikia raia wengi na sasa wanatumia wilaya za Kyerwa na Muleba, walikozalisha mbegu na kuwapatia raia mbegu (miche) 3,500.



Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef), nchini kuna asilimia 34 ya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano waliodumaa.

### Wakazi

Bibi Veneranda Clemence, ni mkazi wa Kijijini Kilimilile, anayelea mjukuu kumsaidia bintiye, ambaye sasa ana mtoto mchanga.

Anasema alikabidhiwa mtoto huyo akiwa na umri wa miaka miwili na uzito wa kilo 7.5 na aliendelea kuishi naye bila ya kumpeleka kliniki katika zahanati jirani ya Kilimilile.

"Nilifundishwa kutumia vyakula vinavyopatikana kwa urahisi katika maeneo tunayoishi vikiwamo ndizi, karanga, mchicha, dagaa, maparachichi na maembe na katika muda wa mwezi mmoja na wiki mbili, uzito wake ulipanda na kilo 9.5," anasema.

Anasema kutokana na elimu aliyoipata, ameelimika na sasa amekuwa mwelekezaji wa kinamama wenye watoto wenye uzito pungufu, uandaaji wa lishe bora kunusuru afya zao.

### IMA World Health

Sista Margaret Ishengoma, ni mtaalamu wa Mabadiliko ya Tabia katika Lishe kutoka shirika la IMA World Health, anasema mradi unalenga kupunguza udumavu kwa watoto na utoaji huduma zao wanashirikiana na serikali na vituo vya huduma za afya vya Kagera.

Sista Ishengoma, anakumbusha kumlundikia mama kazi nyingi kunamkosesha muda wa kupumzika na kunachangia mtoto kudumaa. Anafafanua:

"Kawaida ya mtoto huwa ananyonya, anaacha na kuanza kucheza halafu anaendelea kunyonya. Kwa hiyo, kama mama ana shughuli nyingi, akinyonyesha kidogo mtoto akaanza kucheza anaachana naye mtoto hawezi kunyonya vizur."

> "Baada ya siku 12 tunawapima tena watoto na cha kushangaza chakula hiki kinatenda maajabu. Watoto uzito unaongezeka hata kwa kilo mbili katika kipindi hicho na kuwashangaza wazazi,"

"Wahudumu wa afya ngazi ya jamii wanakwenda kwenye nyumba za walengwa wetu ambao ni wajawazito na watoto wenye umri wa chini ya miaka miwili, kuangalia hali ikoje, kuhimiza na kujadiliana ni kitu gani wanaweza kufanya ili kupunguza udumavu kwa watoto," anaongeza Sista Ishengoma.

"Baada ya siku 12 tunawapima tena watoto na cha kushangaza chakula hiki kinatenda maajabu. Watoto uzito unaongezeka hata kwa kilo mbili katika kipindi hicho na kuwashangaza wazazi," anasema.

Ofisa Lishe wa asasi hiyo, Idda Katigula, anasema ni mradi ulioanza mwaka 2016 na katika mwaka wa fedha 2018/2019, wamepanga kutoa ruzuku ya Sh. milioni 800 kwa halmashauri zote nane za Kagera.

"Tuko katika wilaya zote saba za Mkoa wa Kagera, na wakati tunaanza mradi huu, tulitumia takwimu za serikali za Tanzania Demographic Survey (TDS) ambazo kwa wakati huo zilionyesha mkoa kuwa na udumavu kwa asilimia 41.7 kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano," anasema.

Kuhusu upungufu wa damu, walikuta asilimia 57.2 na kinamama wa umri wa kuzaa, asilimia 39.1. Mradi umepanga kufikia watu zaidi ya 900,000 kwa mkoani Kagera na hadi sasa wameshafikia walengwa 769,886, ambao ni zaidi ya asilimia 80.

# WAZIRI HASUNGA:
## Sumu kuvu yatafuna mazao na uhai wetu

- Imeshaua 19, chanzo robo ya kansa
- Karanga, mahindi katika hali mbaya
- Bn 60/- kunusuru, AU yaingilia kati

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KWA wakulima wengi, mwezi Julai ni wa mavuno ya mpunga, mahindi, karanga, maharage na mtama.

Japo mavuno ni neema, kwa wakulima wengi wa Tanzania ni maumivu kwa sababu huumizwa na kile kinachoitwa hasara zinazotokea baada ya kuvuna mazao mashambani.

Ni hasara zinazoambatana na kupoteza mazao yanayobakia shambani, yakiwapo baadhi yanaharibika, mazao yanayovunda kutokana na kuvunwa mapema, kabla hayajakauka ipasavyo.

Mengine yanaliwa na mchwa, pia wanyama aina ya panya wanashambulia mimea baada ya kukomaa.

Lakini, kubwa ni tatizo linalotishia afya na uhai wa wakulima na walaji, hii ndiyo changamoto kubwa inayotokea wakati wa kuvuna kwani yanachafuliwa na sumu kuvu.

**SUMU KUVU NI NINI?**

Sumu kuvu inatajwa kuwa hatari kwa afya ya binadamu na inapenda kujihifadhi kwenye mahindi na karanga.

Kwa mujibu wa Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Kilimo katika Ukanda wa Kitropiki (IITA), mazao hayo yanatunza wadudu jamii ya kuvu, ambao kitaalamu wanatokana na fangasi au kuvu wanaojulikana kama 'Aspergillus flavus'.

Inadaiwa, kuvu hao wanaishi kwenye udongo na mabaki ya vitu vilivyooza shambani, hawaonekani kwa macho, hivyo si rahisi mkulima kuwabaini.

Mazao yanaweza kushambuliwa na sumu hiyo yakiwa shambani, iwapo yataanguka chini na kugusana na wadudu hao walioko ardhini au kwenye masalia ya mazao yaliyooza.

Asasi hiyo inaitaja kuwa ni sumu hatari na inayosafiri kutoka kwa mama anayenyonyesha, iwapo anakula chakula chenye sumu kuvu na atampa mtoto wake maziwa, sumu hiyo inamdhuru.

**MRADI SUMU KUVU**

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga,anasema tatizo la sumu kuvu nchini ni kubwa na inakadiriwa kukabili asilimia 25 ya mazao nchini.

Hivyo, anasema kumezinduliwa Mradi wa Kudhibiti Sumu kuvu Tanzania (Tanipac) utakaogharimu takribani Sh. bilioni 80 na lengo la mpango huo ni kupunguza sumu kuvu katika mahindi na karanga na umekuja wakati muafaka.

"Ina maana kwa namna moja au nyingine, sisi wote hapa imetugusa au umekutana nao kwa namna nyingine,"anasema Waziri Hasunga .

Anafafanua kuwa tafiti za kiafya zinabainisha kwamba sumu kuvu inachangia zaidi ya aina 25 za saratani, huku kipekee ikichangia asilimia 30 ya saratani ya ini.

Waziri Hasunga anasema, pamoja na kuchangia saratani, kuna ushahidi wa kisayansi unaoonyesha kwamba sumu kuvu inachangia kudumaa watoto na akili zao.

"Kwa hiyo, katika maeneo mengi ambayo tumeona watoto, hata wamezaliwa wamedumaa inawezekana, ni kwa sababu ya sumu kuvu kwahiyo ndio maana tunasema hili tatizo ni kubwa linahitaji kuwekewa nguvu ya kutosha,"anasema.



Mahindi yaliyoathiriwa na sumu kuvu.




Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akipokea maandiko yanayohusu sumu kuvu. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> "Hili ni tatizo, idadi ya vifo na watu walioathirika kwa tatizo hilo ni wengi, inawezekana hawa waliogundulika ni wale waliopima tu, ambao hawajapima huenda tatizo likawa kubwa,"




Mtaalamu akiwa katika maabara inayohudumia kukabili sumu kuvu.

Vilevile, anasema tatizo la sumu kuvu kwa kiasi kikubwa huathiri mazao ya biashara na chakula katika soko la kimataifa, bara la Afrika likipoteza zaidi ya Dola za Marekani milioni 670 (Sh. trilioni 1.494) ambazo ni sawa na asilimia 40 ya mauzo yote nje yanayokataliwa kila mwaka.

"Sisi sote ni mashahidi, tunaona kwamba kwa mfano ukipeleka mazao yako Marekani, kuna masharti magumu sana wanakuambia kuwa, ile fursa ina masharti mengi. Maana wamekuwa wakiamini kuwa sisi uwezo wetu wa kutunza ni hafifu

"Nilikuwa nateta na mwakilishi wa Benki ya Maendeleo Afrika(AFDB) anatoka Gambia na kule kihistoria ni wazalishaji wa karanga na wengi wameathirika, kwa sababu wanazalisha, lakini hawawezi kupeleka nje ya jiji na nchi zote zinakataa kununua zinasema zina sumu.

"Sasa fikiria nchi inayotegemea karanga halafu inaambiwa zote zina sumu kwahiyo ina maana nchi kama inaathirika kimapato kwahiyo hili suala ni la msingi ni muhimu tukaliangalia kwa mapana,"anasisitiza Waziri Hasunga .

Anasema tatizo si geni Afrika Mashariki, kwa sababu limekuwa lilijitokeza nchini Kenya mwaka 2014, watu zaidi ya 300 walipatwa na ugonjwa unaotokana na sumu na kusababisha vifo vya watu 125, baada ya kula kilichokumbwa na kiwango kikubwa cha sumu kuvu.

Anafafanua, tatizo kama hilo liliwahi kutokea nchini mwaka 2016, zaidi ya watu 60 katika Halmashauri za Wilaya za Bahi, Chemba, Kiteto na Kondoa, waliugua kutokana na chakula chenye sumu kuvu, kati yao19 wakifariki.

"Hili ni tatizo, idadi ya vifo na watu walioathirika kwa tatizo hilo ni wengi, inawezekana hawa waliogundulika ni wale waliopima tu, ambao hawajapima huenda tatizo likawa kubwa," anasema, huku akitaja namna nyingine ya maambukizi ni kupitia wadudu aina ya fangasi.

Anatoa wito kwa wadau wote kushirikiana kupambana na tatizo hilo, akieleza kwamba juhudi zinahitajika kutatua changamoto kwenye kilimo, hususan kwa walaji na wazalishaji.

**DIRA YA MRADI**

Waziri Hasunga, anasema mradi unalenga mazao ya mahindi na karanga, yanayoshambuliwa zaidi na utafiti unaelekeza tatizo lipo kwenye Ukanda wa Mashariki, hususani mikoa ya Morogoro (Asilimia 25 hadi 43), Tabora (asilimia 34), Geita (asilimia 40).

Aidha, kwenye zao la Karanga tatizo lipo Ukanda wa Kusini mkoa wa Mtwara, kunakoguswa kwa asilimia 18 hadi 20; Kaskazini mkoa wa Manyara (asilimia 18) .

Kwa mujibu wa Hasunga, athari hiyo iko pia katika mikoa mingine nchini.

Rai yake kwa taasisi zinazojishughulisha na usalama wa chakula, kutimiza wajibu wao, ili taifa libaki salama kutokana na changamoto ya sumu kuvu.

"Hatuwezi kuacha mazao yenye sumu kuvu yakauzwa kwa walaji, kwani madhara ni makubwa kijamii na kiuchumi. Hivyo, tunahitaji kukinga mazao haya kabla hayajamfikia mlaji," anasisitiza Hasunga.

**AU YAZUNGUMZIA CHANGAMOTO**

Mwakilishi wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika(AUC-PACA), Dk.Happy Magoha, anasema jitihada za kukabiliana na sumu kuvu Afrika ni zinakwamshwa na uelewa mdogo wa jamii.

"Kamisheni ya Afrika kwa kushirikiana na jumuiya za kiuchumi za kikanda walipendekeza nchi sita ziingie kwenye programu hii, ambapo ni Gambia, Malawi, Nigeria, Senegal, Uganda na Tanzania,"anasema

Katika mpango huo, nchi hizo zitajengewa uwezo katika sekta zote na Tanzania ilishawasilisha maombi hayo ya kujengewa uwezo kitaalamu, kuzuia mlipuko wa sumu kuvu. Anabainisha kuwa, Tanzania ni nchi ya kwanza kupata ufadhili wa mradi mkubwa wa kudhibiti sumu kuvu.

**BENKU YA AFRIKA**

Meneja wa Benki ya Maendeleo ya Afrika(AfDB-TZ),Johm Ken, anasema zaidi ya kaya 60,000 zitanufaika na utekelezaji wa mradi huo na anafafanua:

"Kwa Benki ya Afrika, huu mradi ni muhimu sana, kwa sababu ni mradi wa aina yake kufadhiliwa, tunaamini utafanikiwa na nchi zingine zitakuja kujifunza kutokana na utekelezaji wenu,"anasema.

AFYA



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akimpatia dawa ya kifua kikuu Abas Sudi, katika hospital ya Mbagala, Dar es Salaam. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

# Waziri wa Afya alipotia mguu hospitali Mbagala

- Aaanika picha nzima ya TB
- Aelezwa kulivyo ziarani

**Na Yasmine Protace**

KIFUA Kikuu kimo katika orodha ya magonjwa hatari ya kuambukiza, zaidi ikienezwa kwa njia ya hewa na katika taratibu za kiserikali, unatibiwa bure, huku ikiendelea na jitihada za kuboresha matibabu.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, siku chache zilizopita, alifanya ziara kukagua hali ya utoaji huduma katika Hospitali ya Mbagala jijini Dar es Salaam.

"Huduma za matibabu ya kifua kikuu sugu zimesogezwa karibu kwa wananchi. Kwa sasa tunazo hospitali 93 za kutibu Kifua Kikuu Sugu, ikilinganishwa na mwaka 2015, huduma za matibabu zilikuwa zinapatikana katika Hospitali ya Kibong'oto pekee "anasema.

Ummy anasema, hivi sasa katika kila Watanzania 100,000, wapo 269 wanaohisiwa kuwa na TB na anafafanua: "Watu 70 kila siku wanakufa kutokana na ugonjwa wa kifua kikuu. Kwa, hiyo kila saa ni sawa na watu watatu wanafariki kutokana na ugonjwa wa kifua kikuu ambao unatibika."

Waziri Ummy anasema takribani wagonjwa 154,000 wanaokadiriwa kuugua kifua kikuu, wanapaswa kufikiwa na kuingizwa katika mpango wa matibabu kila mwaka, ili kuutokomeza nchini.

Anasema, Tanzania ni miongoni mwa nchi 30 duniani zenye kiwango kikubwa cha wagonjwa wa TB. Inakadiriwa kuwapo wagonjwa 154,000 kila mwaka.

Waziri Ummy anasema, mgonjwa wa kifua kikuu ambaye hajaanza matibabu, anaweza kuambkiza kati ya watu 10 hadi 20 kwa mwaka, hivyo jitihada za makusudi zinatakiwa kuendelea kutokomeza maradhi hayo.

"Hivyo, tunalo jukumu kubwa la kuhakikisha tunawafikia wote wanaougua, ili tuweze kuzuia maambukizi mapya," anasema.

Kuhusu wagonjwa sugu, Ummy anasema kitaifa kunakadiriwa takribani kuna wagonjwa 200, kati yao 167 sawa na asilimia 84, walianzishiwa matibabu. Wito wake ni wagonjwa wengine wajitokeze kutibiwa.

**KUTOKA HOSPITALINI**

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Felix Lyaviva, amemuomba Waziri Ummy, aangalie uwezekano wa kuipanua Hospitali ya Mbagala, ili kurahisisha utoaji huduma za afya, kwani kuna takribani wanawake 67 mpaka 70 wanaojifungua kwa siku.

" Kinamama wanaojifungua hapa ni wengi sana. Kwa mfano jana tu , kinamama 67 walijifungua, siku nyingine wanafika 70 mpaka 80. Hivyo, tunahitaji ipanuliwe," anasisitiza.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk Ally Mussa, anasema kutokana na maboresho makubwa ya hospitali hiyo, sasa kuna ongezeko kubwa la wagonjwa hadi kufikia wagonjwa 1,700 kwa siku.

Pia, anasema kuna maboresho makubwa ya huduma za mama na mtoto na uchunguzi kimaabara kwa wagonjwa.

MAZINGIRA



**JUU NA CHINI:** Kampeni ya usafishaji ufukwe wa Coco, jijini Dar es Salaam, ambayo si mbali na Msasani, kulikofanyiwa usafi na vijana wa Skauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# Skauti wahamia ufukweni kukabili uchafu uliokithiri

## • Waanzia Msasani kwa Nyerere

**Na Beatrice Philemon**

KATIKA kusimamia hatima ya mazingira nchini na kimataifa, moja ya mambo muhimu wanayohimiza vizazi vya vijana na watoto kutunza mazingira yasiwe na madhara, hasa kutetea viumbe baharini.

Hivi sasa fukwe nyingi nchini zimesheheni uchafu na hasa mifuko na chupa za plastiki, kopo na taka za vyakula, ambazo ni hatari kwa samaki na viumbe baharini.

Tanzania imeazimia kuwa na utalii wa fukwe, ambao moja ya vigezo vya ufanisi wake ni uadhifu, ili watalii wakae vizuri, kutoka matokeo ya kazi za mabalozi wa mazingira.

Hivi karibuni, maskauti 300 kutoka shule nne za msingi jijini Dar es Salaam, walitembelea nyumbani kwa Baba wa Tafa, Mwalimu Julius Nyerere, kufanya usafi ufukweni.

Kazi hiyo iliofanyika kuenzi mchango wake kwa huduma za skauti nchini, pia siku ya kuzaliwa mwanzilishi wa skauti duniani, Baden Powel.

Carlos Mdemu kutoka Taasisi ya Kijamii ya Masuala ya Mazingira inayojulikana kama 'Nipe Fagio'ameiambia Nipashe kwamba, waliamua kushiriki kampeni ya kusafisha fukwe ya makazi ya Mwalimu Nyerere, ili kukifundisha kizazi kijacho maana ya usafi katika maeneo yao.

Mdemu anafafanua azma nyingine, ni kusafisha mazingira baharini na kuwaelimisha aina za taka zinazooza na zisizooza, pia madhara yake kwa viumbe baharini na afya ya binadamu.

"Lengo kuu tunataka wajue taka zisizooza kama vile chupa, mifuko ya plastiki hasa ya rambo zina madhara gani kwa viumbe wa baharini, kwa sababu mfuko wa plastiki wa rambo unachukua miaka 500 hadi 1000 kuoza," anasema.

"Tunawafundisha kusafisha fukwe za bahari ili kuokoa maisha yetu na viumbe wetu baharini,"anasema Mdemu na kufafanua:

"Lengo la zoezi hili ni kudumisha moyo wa kujitolea kwa Skauti na vijana kwa ujumla kwani baba wa Taifa aliwahi kusema "It can be done play your part (Inawezekana, Timiza Wajibu wako)."

Kiongozi wa skauti hao, Cuthbert Safari, anasema waliamua kufanya usafi ufukweni kwa Mwalimu Nyerere, kwa sababu alikuwa karibu sana na jumuiya skauti.

Vilevile, walienda kujifunza elimu ya mazingira na kufundisha wanafunzi wa skauti elimu hiyo, ili watoto wawe mabalozi wa usafi wa miaka ijayo.

"Hii ni mara ya kwanza kushiriki katika zoezi hili, tutakuwa tunafanya zoezi hili la usafi kwenye maeneo tofauti tofauti kila baada ya miezi mitatu," anasema.

### KITABU KIPYA

Walimtaka Mama Maria Nyerere, azindue kitabu kinachohusu vijana 'Mwenendo na Tabia Nzuri' kilichoandikwa na Mzee Biga Kaisi.

Cutherbert, anaushukuru mfuko uitwao 'Rejuvenation Fund' kwa kuwasaidia kuwapatia vifaa kwa ajili ya usafi ikiwemo chakula kwa

> "Kila mwananchi kupitia mradi huo atakuwa na wajibu wa kutenganisha taka nyumbani kwake, ili kuhakikisha inakaa sehemu yake, ili mwishoni zile taka zote zinazoweza kurejeshwa, zinapelekwa viwandani kutengeneza bidhaa nyingine na mabaki yasiyo na matumizi, yanapelekwa dampo."



ajili ya wanafunzi walioshiriki katika kampeni hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya familia ya Mwalimu Nyerere, mjukuu wake , Moringe Magige, anawashukuru skauti kwa kufanya usafi ufukweni hapo, kumuenzi babu yake kwa kwa mchango aliowapatia skauti nchini.

Huku akiomba udhuru wa bibi yake Mama Maria kutohudhuria hafla hiyo, Moringe alipokea nakala ya kitabu kwa niaba yake.

### MHAMASISHAJI

Ofisa Uhamasishaji kutoka taasisi ya Nipe Fagio, Wilyhard Shishikaye, anasema hivi sasa kuna ongezeko kubwa la watu jijini Dar es Salaam, ikilinganishwa na huko nyuma.

Anasema kuna wakazi wengi wanaoishi pasipo kujali taka wanazozizalisha ndizo baadhi zinazoshuhudiwa ufukweni mwa baharini.

"Ndiyo maana leo tulipokuwa tunafanya usafi na watoto wa skauti, tulishuhudia taka nyingi za plastiki, mifuko ya plastiki, chupa cha plastiki na kioo, vifuu vya nazi, pampasi, viatu, kandambili ambazo kwa ujumla wake zinachafua bahari," anasema.

"Mara nyingi tumekuwa tukifanya shughuli za usafi wa mazingira, usafi wa 'beach' (ufukweni) katika maeneo tofauti ya jiji la Dar es Salaam, kwa kushirikisha wananchi wanaoishi katika jamii husika.

"Pia, kushirikiana na vikundi mbalimbali vya kijamii kama vile; Jogging Clubs', vikoba, timu za mpira, shule, pia kushirikiana na wanafunzi wa shule mbalimbali binafsi na serikali.

"Kitu kilichotuvutia hadi kutoa elimu ya usafi wa mazingira kwa skauti, ni baada ya kuona Dar es Salaam imekuwa chafu zaidi," anasema Shishikaye, anayerejea

ripoti ya Jarida la Forbes, 2012, inayoitaja kuwa kinara wa uchafu kimataifa.

### MRADI MPYA

"Sisi kama 'Nipe Fagio' tuna vifaa vya kutosha kufanya usafi, wataalamu wa kutosha kuhusu masuala yote ya taka ngumu, pia tunatoa elimu kuhusu masuala yote ya taka ngumu," anafafanua Shishikaye, anayedai kuwa na mabalozi wataalamu na wasimamizi wa kutosha.

Anasema kuanzia mwaka huu, taasisi ya Nipe Fagio imepanga kufanya mradi unaoitwa 'Taka Sifuri' kwa miaka 10, unaomwajibisha mtu kuanzia uzalishaji, hifadhi na usafirishaji taka .

Lengo la mradi huo ni kupunguza taka zinazokwenda dampo kwa asilimia 80, ikizingatiwa Dar es Salaam ina dampo moja pekee.

"Kila mwananchi kupitia mradi huo atakuwa na wajibu wa kutenganisha taka nyumbani kwake, ili kuhakikisha inakaa sehemu yake, ili mwishoni zile taka zote zinazoweza kurejeshwa, zinapelekwa viwandani kutengeneza bidhaa nyingine na mabaki yasiyo na matumizi, yanapelekwa dampo.

"Mradi huu unarajia kuanza mwezi wa nne baada ya kupita mitaa yote ambayo mradi utatekelezwa na mpaka sasa, baadhi ya wanajamii tayari wamependekeza mitaa yao na tulishakutana nao.

"Kilichobaki ni kupata picha ya mitaa, ili kujua idadi ya wakazi, aina ya taka zinazozalishwa na mafunzo ya ukusanyaji taka uliyopo kwenye mitaa, anasema.

AFYA

# UNAIJUA NAWEZA?

## Mkakati unaosuka upya mwelekeo kukabilli magonjwa hatari nchini

**Na Mary Geofrey**

WIKI iliyopita mkoani Iringa, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma, walizindua jukwaa liitwalo 'Naweza.'

Hilo ni jukwaa la mawasiliano ya afya kwa watu wazima, linalolenga mabadiliko chanya ya tabia kwa jamii. Mtazamo uliopo ni kusaidia kufikisha taarifa zitakazowajengea uwezo Watanzania katika kubadili tabia zao kiafya.

Pia, linalenga kuimarisha afya ya kila mmoja, familia na jamii nzima, kumuwezesha Mtanzania ajitambue na awe na uwezo wake wa kujiwekea nia kuishi maisha bora zaidi.

Mradi huo unaendeshwa kupitia Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), chini ya mradi wa 'USAID Tulonge Afya' unaofikia tamati mwaka 2022.

Ofisa wa Wizara Programu ya uzazi Salama, wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, Martha Shakinyau, anasema jukwaa linalenga huduma jumuishi za afya kwa pamoja, katika kubadilisha tabia kwenye maeneo muhimu matano.

Anayataja kuwa ni maradhi ya: Ukimwi, Malaria, Afya ya Uzazi kabla baada ya kujifungua, Afya ya Mama na Mtoto na Kifua Kikuu.

Pia, linalenga mawasiliano ya kuhamasisha ubadilishaji tabia, kulingana na mahitaji na vipaumbele vya wakati husika, kama vile kipindi cha ujauzito au malezi ya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Anasema, watu wazima wanalengwa kupata habari na maarifa yatakayowawezesha kubadili tabia zao kiafya kwa wakati sahihi, ikiweka taratibu zinazokwaza mapokeo na mwendelezo wa tabia chanya zinazipotishwa na jukwaa.

Ili kufikisha ujumbe, Martha anasema jukwaa litafanya kazi kupitia mifumo yote ya mawasiliano, vikiwamo vyombo vya habari, uhamasishaji jamii, ana kwa ana, digitali na mitandao ya kijamii.

### KWANINI ILIANZISHWA?

Martha anasema mradi huo ulianzishwa kujenga na kuimarisha uzoefu katika mawasiliano nchini yanayobadili tabia ya jamii, ili kuiwezesha serikali kufanikisha mikakati ya afya, kulingana na vipaumbele vya kitaifa.

Anavitaja vipaumbele hivyo ni upunguzaji maambukizi vya Ukimwi, vifo vya uzazi na watoto wachanga, malaria na kifua kikuu.

Martha anasema, kampeni nyingi zilianzishwa kukidhi changamoto zilizopo kwa wakati husika, lakini zilikosa ufanisi kwa sababu ya kuingiliana kimaslahi, kwa sababu ziliwagusa walengwa wale wale kwa wakati mmoja.

Marha anasema, mradi huo mpya utaunganisha jitihada za wadau wanaotekeleza kubadili tabia katika jamii, ikijikita katika utoaji elimu na maarifa kwa jamii, familia na vikundi rika, ili kuwapa ari ya kuboresha afya na kuishi maisha ya furaha, yanayoratibiwa na jukwaa moja.

"Kila siku, jukwaa la 'Naweza' linazidi kujenga uaminifu kwa makundi muhimu tofauti, likiyawezesha kufikiwa na jumbe ama kazi mahsusi zinazolenga kila mmoja moja kwa moja," anasema Martha.




Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, akimuonyesha jarida mmoja wa maofisa walioshiriki uzinduzi wa jukwaa la Mawasiliano la Naweza uliofanyika mjini Iringa. **PICHA ZOTE: MARY GEOFREY.**

> Katika kukuza wigo wa jukwaa hili, nyenzo za Naweza zinapatikana kwa wadau wote watakaotaka kuzitumia kwenye miradi yao. Tunawakaribisha wote wanaotaka kuzitumia waje wazungumze nasi wakati wowote kuhusu fursa hizi au namna nyingine tunaweza kufanya kazi na wadau wa kuikuza Naweza,"



Ofisa wa Program ya Uzazi Salama wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Martha Shakinyau (aliyevaa nguo nyekundu) akifuatilia uzinduzi wa Jukwaa la Mawasiliano la Naweza, mjini Iringa, hivi karibuni.

### MIKAKATI

'Naweza' imejikita na vipaumbele vya mikakati ya kiafya ya serikali kwa karibu, ikitilia mkazo maeneo ya afya yanayoakisi malengo, mikakati na juhudi za serikali.

Martha anasema tabia chanya ambazo 'Naweza' inazipa kipaumbele, zinatokana na makubaliano ya wadau muhimu wanazoendeleza mikakati iliyoainishwa katika machapisho rasmi ya kitaifa, pia maamuzi ya kisera.

Martha anayataja maeneo yatakayowezeshwa na anachokitaja kuwa Jukwaa Mkakati wa Taifa ni kuboresha afya ya uzazi, kinamama, watoto wachanga na vijana nchini.

Pia, anataja eneo jingine ni Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi wa mwaka 2018 hadi 2020; na Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Malaria wa Mwaka 2014 hadi 2020.

Anasema Mkakati wa Taifa wa Tano wa Mwaka 2015 wa Kutokomeza Kifua Kikuu na Ukoma, nalo ni eneo watakaloligusa kwa kina.

### MAJUKUMU YAKE

Martha anayataja ni kuwapo majukwaa unganishi kama ilivyo Naweza, yakilenga maeneo tofauti ya afya kupitia mikakati shirikishi.

Anataja mbinu za mawasiliano ni kuwafikia watu walioko au makundi mahusus, kuyapa maelekezo na motisha zinazowalenga moja kwa moja.

Kwa mujibu wa Martha, jukwaa hilo lina njia mbalimbali za kuwafikia walengwa na mawasiliano ya kiafya chini ya jina moja Naweza kuanzia vyombo vya habari, uhamasishaji wa jamii, mawasiliano ya ana kwa ana baina ya mtu na mtu, digitali na mitandao ya kijamii.

Anasema, jukwaa hili linatofautiana na kampeni nyingine za afya ambazo hulenga maeneo mahusus ya kiafya huku shughuli zikifanyika kwa kipindi maalum.

"Vilevile Naweza ni tofauti na programu au miradi mingine ya afya, ambayo inahusisha shughuli nyingi na hutekelezwa kulingana na wigo wa kazi uliopangwa na mfadhili," anasema Martha.

### USHIRIKIANO ULIVYO

Martha anasema Naweza sio mbadala wa kampeni zilizopo za afya, isipokuwa inahakikisha programu zilizopo zinaendelezwa na kukuzwa zaidi.

Pia, kampeni ya Tuwavishe Salama iliyozinduliwa mwaka jana, inayowalenga watoa huduma za afya, watunga sera na wafanya maamuzi katika kuhakikisha wanatoa kipaumbele kwa ulinzi wa afya za kinamama na watoto wachanga.

Martha anaahidi kwamba Naweza itabeba kampeni nyingine ya 'Jiongeze' iunganishe jumbe zake za kuhimiza mabadiliko ya tabia ndani ya jamii chini, ya jukwaa moja na katika nyaraka zote zinazohusiana afya ya mama na mtoto.

### UKUZAJI JUKWAA

Martha anasema wadau na mashirika yaliyohusika kuunda jukwaa la Naweza, wana shauku ya mafanikio yake na ni fursa ya kuzungumza na watu binafsi, familia na kaya.

Anataja njia za kufikisha ujumbe ni kupitia nyenzo kama vile kadi mahususi za ushauri zinazotolewa na vituo vya huduma za afya, maigizo katika jamii, vipindi vya redio vya kila wiki vinavyowashawishi kukubali tabia zao kiafya.

"Katika kukuza wigo wa jukwaa hili, nyenzo za Naweza zinapatikana kwa wadau wote watakaotaka kuzitumia kwenye miradi yao. Tunawakaribisha wote wanaotaka kuzitumia waje wazungumze nasi wakati wowote kuhusu fursa hizi au namna nyingine tunaweza kufanya kazi na wadau wa kuikuza Naweza," anasema Martha.

### MKURUGENZI ELIMU

Kaimu Mkurugenzi wa Elimu ya Afya kwa Jamii, katika wizara yenye dhamana na afya, Dk. Amma Kasangala, anasema jukwaa hilo ni mkakati wa pamoja unaolenga kutumia mbinu shirikishi kuelimisha, lego kuu ni kubadili tabia na kuboresha afya.

Dk. Kassangala anasema, walengwa ni wenye umri kati ya miaka 18 na 45 na jukwaa la vijana ni kwa wenye umri wa miaka 15 hadi 24, eneo kuu la malengo ni: Malaria, kifua kikuu, mama na mtoto, huduma za afya ya uzazi kabla na baada ya Ujauzito, VVU na Ukimwi.

# Wanaunguzwa matiti wasivutie wanaume

**LONDON,** Uingereza

KUTOKANA na kukithri tabia ya kinamama kuunguza matiti yao kwa imani yasikue, Taasisi ya Elimu nchini Uingereza, sasa inashauri kuwapo elimu katika mtaala shuleni, kudhibiti matukio hayo.

Inaelezwa, vitendo hivyo vinahusisha kuunguza matiti ya wasichana kwa kutumia vitu vya moto, ili kuzuia yasikue haraka na kutowavutia wanaume.

Mbunge wa Chama cha Conservative, Nicky Morgan, anasema walimu wanapaswa kupewa elimu, kwa kuwa wana nafasi kubwa ya kuwaelimisha mabinti.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, nayo imesema walimu wana wajibu wa kutimiza lengo hilo.

**MWIKO KULIA**

Mama mmoja nchini Uingereza, mwenye asili ya Afrika Magharibi, ambako kuna asili ya mila na vitendo hivyo vya kuunguza matiti, anasema alianza kufanyiwa akiwa na umri wa miaka 10.

Anasema mama yake alimtamkia: "Kama hautayaunguza, wanaume wataanza kukufuata ili ufanye nao ngono"

Inaelezwa kuwa kimama amabao ndiyo hulifanya hilo, huunguza mabinti kwa kutumia mawe au vijiko, ambavyo baada ya kujipasha katika moto, wanavikandamiza kwenye matiti ya mabinti, kuhitimisha azma zao na hufanyika kila baada ya mezi kadhaa

"Maumivu yake huwa ya muda mrefu," anasema mama huyo na kuongeza: "Huruhusiwi hata kulia. Ikiwa utafanya hivyo, wanasema utailetea aibu familia, itatoa ishara kuwa wewe si msichana jasiri".

Kwa sasa mama huyo ana mabinti, anakiri kwamba mtoto wake mkubwa alipotimiza miaka 10, mama yake alipendekeza mjukuu wake huyo aunguzwe matiti.

"Nilisema hapana, hapana, hapana! Hakuna mtoto wangu yeyote atapitia nilichokipitia na kuniathiri mpaka sasa kutokana na niliyoyapitia," anasimulia mama huyo.

Anasema, aliondoka na kwenda mbali na familia yake kuwaweka mbali na madhara hayo, akiamini kuna makubwa, iwapo angewaunguza matiti bila ya ridhaa yao.

Inaelezwa utaratibu wake, wasichana huvaa vitambaa vinavyobana kuzunguka vifua vyao wakati wa kuunguzwa. Hadi sasa inaaminika takriban wasichana 1,000 nchini Uingereza wameshaathirika na 'uchomaji'matiti.

Aidha, kunaelezwa kuwepo elimu kuhusu ukeketaji dhidi ya wasichana, lakini ni wachache wanaofahamu kuhusu 'uchomaji' matiti.



Hii ndio hali halisi na vifaa vinavyotumika. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Mwanamke mwingine Nicky Morgan, anaesema alibaini kuungua matiti si kitu cha kawaida, alipojigundua kuwa na mwonekano tofauti na wenzake shuleni, hali iliyomuathiri sana kisaikolojia.

Nicky anashauri masuala ya 'uchomaji' matiti yanapaswa 'kudhibitiwa katika ngazi ya ukomeshaji kabisa".

Anasema, walio karibu na wasichana wanapaswa kufundishwa kutambua kuwa 'kuchoma' matiti kupo nchini Uingereza, hivyo wasichana waelimishwe hatua wanazopaswa kuchukua katika kujihami.

Mwanake mwingine anakiri 'alichomwa' matiti alipokuwa na umri wa miaka 13, mama yake alipogundua kuwa na mwekekeo wa uhusiano wa jinsia moja.

"Kwa mujibu wa mama, nilikuwa navutia kwa sababu ya matiti yangu, hivyo ikiwa atanichoma nitachukiza na hakuna atakayekuwa akinitamani," anasema.

Anarejea kumbukumbu kwamba, alichomwa matiti kwa kipindi cha miezi kadhaa ana akavalishwa kitambaa cha kubana sana kuzunguka kifua, hali iliyo na ugumu wa kupumua.

Miaka michache baadae, alipopata mtoto na mwanaume ambaye alilazimishwa kuolewa naye, anasema kukawepo shida iliyodumu kwa muda mrefu, anayoifafanua:

"Nilipata taabu sana wakati wa kunyonyesha. 'Nilihisi kama baadhi ya neva kuwa nimeharibiwa."

Hata hivyo, nchini hakuna sheria yeyote ya kupinga vitendo hivyo na Wizara ya Mambo ya Ndani, inaishia kueleza vitendo hivyo ni unyanyasaji dhidi ya watoto.

Angie Marriot, ni daktari mstaafu wa maradhi ya wanawake, anasema tatizo hili halikuwa linaripotiwa zamani, ila ni uhalifu unaofanyika kwa kificho na ni mara ya kwanza wamezungumza kilichowatokea na kueleza kuwa waliogopa kujitokeza kwa kuona aibu.

Anasema wanawake wanaogopa kuripoti kuwa walishawahi kuchomwa matiti, Simone hadi sasa bado anaugulia makovu aliyoyapata na anataka kutoa elimu kuhusu uhalifu huo.

"Ni udhalilishaji, inaumiza na kukuondolea utu wako, anasema na kufafanua: 'Huwezi kujihisi mwanadamu."

# Majaji: Umri wa ngono uwe miaka 16

MAHAKAMA ya Rufani nchini, imependekeza umri wa kuruhusiwa kujihusisha na ngono kitaifa, upunguzwe hadi kwa miaka miwili, iwe 16.

Kwa sasa, sheria zinaruhusu vijana wa miaka 18 na kuendelea ndio wana ruksa ya kufanya mapenzi.

Majaji watatu wa mahakama hiyo, katika maamuzi yao walipendekeza maboresho ya sheria na umri wa kuruhusiwa kufanya mapenzi ishushwe kutoka miaka 18 hadi 16.

Majaji hao wanapinga adhabu kali ya vifungo virefu jela wanayopewa wanaume, kwa kushiriki ngono na mabinti wakitumia mfano wa hukumu ya kesi waliotupa ya kifungo cha mika 15, alichopatiwa mwanamume aliyempa mimba msichana wa miaka 17.

Pia, wanasema baadhi ya wavulana na wasichana walio chini ya miaka 18, tayari wanajihusisha na uhusiano wa kingono.

"Magereza yetu yamejaa vijana wa kiume ambao wanatumikia vifungo virefu kwa kushiriki ngono na wasichana, ambao ridhaa yao ya kufanya matendo hayo haitambuliki kisheria, kwa sababu tawajafikia miaka 18," hukumu ya majaji hao imenukuu.

"Inawezekana hawajafikia umri wa utu uzima, lakini yawezekana tayari wameshafikia umri wa kuridhia kufanya ngono na wanaweza kuchukua hatua sahihi na za kiweledi kuhusu maisha yao na miili yao," anasema

Katika kesi husika, mshitakiwa Eliud Waweru, alifungwa baada kumtia mimba msichana ambaye aliyemaliza kidato cha nne.

Majaji wanasema, msichana huyo alilazimishwa kutoa ushahidi dhidi ya Waweru na wazazi wake, jambo ambalo aliliandika kwenye barua zake mbili na kutishia kujiua.

Waweru ambaye aliyekuwa anatumikia kifungo cha miaka nane, ameachiliwa huru Ijumaa iliyopita.





# Wasiosikia watishia kususia uchaguzi serikali mitaa

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MWENYEKITI wa Chama cha Viziwi Mkoa wa Mbeya, Tusajigwe Mwalwega, amesema endapo serikali haitatenga fungu maalum kwa ajili ya kuwatafuta wakalimani wa kuwasaidia viziwi kwenye mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu, hawatashiriki kupiga kura.

Akizungumza na Nipashe, Tusajigwe alisema licha ya serikali kuwa mstari wa mbele kutetea haki za watu walio kwenye makundi maalum, lakini imekuwa ikiwasahau pindi unapofika wakati wa uchaguzi.

Alisema katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu endapo hawatashirikishwa kwenye mchakato wa uchaguzi hawatashiriki na kwamba watakuwa wamenyimwa haki yao ya msingi kikatiba.

"Watu wenye ulemavu husani viziwi tumetengwa na serikali na jamii katika ngazi mbalimbali za maamuzi hata kwenye mikutano ya vijiji na mitaa hatupewi taarifa ya mambo yanayojadiliwa, ukifika wakati wa uchaguzi wanajiamulia wenyewe halafu wakihitaji kura zetu wanakuja kutubembeleza, sasa mwaka huu hatutafanya hivyo," alisema Tusajigwe.

Tusajigwe alisema ili kuondoa makandokando hayo serikali hasa watendaji wake wa chini kutekeleza wajibu wao bila ya upendeleo kwa kuhakikisha viziwi nao wanahusishwa katika shughuli mbalimbali za maendeleo.

Mratibu wa Shirika la Elimisha, Debora Mwanyanje, alisema ili kuleta usawa serikali kupitia wataalamu wake iweke utaratibu wa kuwatembelea na kutoa elimu ya masuala mbalimbali kwa viziwi.

Alisema elimu hiyo itawasaidia kutambua masuala mbalimbali na wajibu wao badala ya kulalamika au kutoa matamko.

Balozi wa kitongoji cha Nyibuko kilichopo Kata ya Mwakibete, Selina Lyapinda, alikiri viziwi kutoshiriki kwenye mikutano mbalimbali ya maendeleo wanayoitisha.

Alisema sababu ya kufanya hivyo ni kukosa gharama za kuwalipa wakalimani ambao watasaidia kuwafasiria viziwi hao, aliiomba serikali kutenga fungu la kuwalipa wakalimani ili viziwi nao washiriki kwenye mikutano.

# Kikwete akagua uwanja ujenzi wa chuo kikuu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Rais mstaafu Jakaya Kikwete ametembelea eneo la Tanganyika Parkers lililopo katika mji wa Mbalizi wilayani Mbeya, ambalo chuo hicho kimepewa ekari 3,000 kwa ajili ya kujenga chuo cha udaktari na kiwanda cha dawa.

Chuo hicho tawi la Mbeya ambacho kwa sasa kinaendelea kutoa taaluma ya afya kwenye majengo ya Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya kinaelezwa kukabiliana na changamoto ya ufinyu wa majengo kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi iliyopo.

Kikwete ambaye ni rais mstaafu, alisema serikali kwa kushikiriana na wadau kutoka mataifa mbalimbali wanakusudia kujenga chuo katika eneo la Tanganyika Parkers na kwamba kitakuwa na ubora wa mfano nchini.

Alisema atahakikisha ujenzi wa majengo hayo yanaendana na hadhi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kusisitiza kwamba ujenzi huo utakamilika kwa muda.

"Tuna mipango mingi ya kukuza na kupanua chuo chetu cha Dar es Salaam na miongoni mwa vipaumbele ni kwenye hili tawi la Mbeya tunakusudia kujenga chuo kikubwa ambacho kitabeba wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali nchini hususani kanda ya nyanda za juu kusini, lakini pia eneo tulilopewa tutajenga na kiwanda cha vifaa tiba," alisema Kikwete.

Kikwete alisema chuo hicho kitaendelea kutoa elimu bora na kuzalisha vijana mahiri na wabobezi ambao watahitajika kwenye soko la kimataifa la udaktari.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Bonaventure Rutinwa, alisema sababu ya kuanzisha chuo hicho ni kusogeza karibu huduma kwa wananchi zaidi ya milioni nane wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Profesa Rutinwa alisema mpaka sasa chuo hicho, kina jumla ya wanafunzi 1,146 na kwamba mafunzo yanayotolewa yanaanzia ngazi ya cheti na shahada.

"Tunajivunia uwepo wa masomo ya udaktari kwan kuwa tumeweza kupata madaktari bingwa 30 ambao wanatoa huduma katika Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya," alisema Profesa Rutinwa.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema ni heshima kubwa kwa mkoa kupewa nafasi ya kujenga chuo kikubwa cha afya.

Chalamila alisema chuo hicho kitazalisha madaktari ambao watasaidia kutoa huduma za afya katika zahanati, vituo vya afya na hospitali zote za mkoa wa Mbeya na kusaidia kukabiliana na changamoto ya uhaba wa madaktari.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NIC Tanzania Ltd, Mick Karima (kushoto), akizungumza na wanafunzi wa shule za sekondari za Tambaza na Kisutu Wasichana, waliofanya ziara ya siku moja ya mafunzo ya kibenki katika benki hiyo, iliyopo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Butiku ataka teknolojia itumike kuisaidia serikali

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MKURUGENZI wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, amewataka Watanzania kutumia elimu na teknolojia ili kuisaidia serikali kufikia uchumi wa kati kwa kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa nchini.

Butiku alitoa kauli hiyo akiwa mkoani Mbeya, kwenye mdahalo uliohusu viongozi na maendeleo yenye tija ambapo mada ilikuwa ni uongozi shirikishi kwa kuzingatia taratibu za kitaasisi pamoja na wajibu wa viongozi katika kuhamasisha maendeleo kwa wananchi.

Alisema ili kufikia mpango wa serikali wa kuelekea uchumi wa kati, kila mwananchi anapaswa kutumia elimu na teknolojia kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa nchini.


Butiku alisema teknolojia ya kisasa ambayo itatumika kuongeza thamani ya uzalishaji mazao itakuwa ni msaada kwa taifa kukuza uchumi, lakini pia kujivunia kutengeneza rasilimali zake. "Tunapaswa kutimiza azima ya nchi kuelekea uchumi wa kati kwa vitendo na sio maneno ili tufanikishe hilo inahitajika elimu juu ya matumizi mapya ya teknolojia ambayo yatasaidia kuongeza thamani ya uzalishaji wa mazao yetu na bidhaa," alisema Butiku.

Butiku alisema Taasisi ya Mwalimu Nyerere ambayo ilianzishwa kwa lengo la kukuza uwajibikaji, uadilifu na uzalendo imekuwa mstari wa mbele katika kuishauri serikali kwenye masuala mbalimbali ya maendeleo.

Aidha, alisema imekuwa ikizalisha vijana wanaofundishwa uzalendo, uwajibikaji na uadilifu ili kukabiliana na vitendo vya rushwa wanapowatumia wananchi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya ambaye alikuwa mgeni rasmi katika mdahalo huo aliwaeleza watendaji mbalimbali kutoka halmashauri na wilaya zote kuwa ili kuenzi na kudumisha yale aliyoacha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere kila kiongozi akatae rushwa kwa vitendo na siyo mdomoni.

Alisema kuna baadhi ya viongozi ambao wanasimama majukwaani na kuwaeleza wananchi kuwa wanakataa rushwa, lakini kiuhalisia hawako hivyo aliwataka kuwa wazalendo na kusimama kwenye misingi ya utumishi wa umma.





## Halmashauri yamwaga mikopo kwa wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu,**
SINGIDA

HALMASHAURI ya Ikungi mkoani Singida, imetoa mikopo ya Sh. milioni 85.9 kwa vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu ili kuwawezesha kupambana na umaskini.

Taarifa iliyotolewa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ikungi, Justice Kijazi, ilisema mikopo hiyo imetolewa kuanzia Julai 2018 hadi sasa.

Alisema imewezesha vikundi hivyo kufanya shughuli za maendeleo ambazo zinawasaidia kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini wa kipato na hivyo kuboresha maisha yao na kuchangia pato la taifa.

Kwa mujibu wa Kijazi, mikopo ya wanawake Sh. milioni 49 kwenye vikundi 27, vijana wenye vikundi tisa jumla ya Sh. milioni 29 na wenye ulemavu vikundi vitano Sh. milioni 7.2.

Alisema kati ya vikundi vya vijana kimoja kinamiliki kiwanda cha chaki kimepewa Sh. milioni 15, na kwamba shule zote 110 za wilaya hiyo zimetakiwa kununua chaki kutoka kwa kikundi hicho.

Kijazi alisema mikopo hiyo imeelekezwa kwenye vijiji na kata mbalimbali kwa vikundi ambavyo vimejikita kwenye kuweka na kukopa, ufugaji kuku, ujasiriamali na biashara, ushonaji na biashara ndogondogo. "Mikopo tunayowapa haina riba na inatolewa kwa mwaka mmoja, vikundi vinavyopata mikopo mikubwa vinapewa muda wa miezi mitatu wa kujipanga, wastani wa watu kwenye vikundi ni kuanzia saba isipokuwa vikundi vya vikoba vyenye watu 30," alisema.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii, Haika Massawe, alisema alisema changamoto kubwa ni uhitaji mkubwa wa mikopo wakati fedha inayopatikana ni kidogo, baadhi ya vikundi kutokuwa na miradi endelevu, pamoja na urejeshaji usioridhisha hasa kwa vikundi vya vijana.

Alisema vikundi vinavyoshindwa kurejesha mikopo hiyo vingi ni vya vijana na kwamba baadhi wamefikishwa mahakamani ili kuweka makubaliano ya kurejesha. "Mikopo imesaidia wanavikundi kugharamia huduma za kijamii kama afya na mahitaji ya shule kwa watoto wao," alibainisha Haika.

# Yatima waiomba serikali kuwamulika wanaotupa watoto

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

SERIKALI imeombwa kuwachukulia hatua wazazi ambao wamekuwa wakiwatupa watoto na kusababisha wingi wa watoto wa mitaani.

Ombi hilo lilitolewa jana na watoto wanaolelewa na kituo cha Rahmani Orphanage Center kilichopo Chang'ombe jijini Dodoma, wakati wakitoa shukrani zao baada ya kupokea misaada mbalimbali kutoka Jumuiya ya Waislamu ya Ahmadiyya kanda ya kati.

Mtoto Saluma Halfani alisema serikali inapaswa kutowafumbia wazazi hao ambao wamekuwa wakiisababishia serikali kubeba mzigo wa kuwalea watoto wakati wazazi wao wapo.

Alifafanua kuwa watoto wengi wanaolelewa kwenye vituo asilimia kubwa hawana wazazi baada ya kutelekezwa.

"Kitendo hiki ni cha kikatili na pia serikali na jamii imekuwa ikiingia gharama kubwa ya kutuhudumia kiafya na hata kielimu," alisema mtoto Kulwa Juma.

Kwa upande wake, mwanzilishi wa kituo hicho cha Rahmani, Rukia Hamisi, alisema kuwa changamoto kubwa iliyopo kwenye vituo vya kulelea watoto ni ukosefu wa wazazi wenye watoto hao, ambao kwa asilimia kubwa waliwatupa na wengine kuwakimbia kutokana na hali ngumu ya kimaisha.

"Baadhi ya wazazi kwenye kituo changu hiki sina kabisa na mawasiliano na wazazi wa watoto hao mnaowaona hapa karibu walio wengi watoto hao walitupwa na miongoni mwao tuliletewa na Ustawi wa Jamii ili tuwalee, hivyo tunaomba vyombo husika kuwachukulia hatua kali wazazi hao wenye tabia ya kikatili na manyanyaso," alisema.

Naye Shekhe wa Jumuiya ya Ahmadiyy, Khawaja Muzafar, alisema jumuiya imekuwa ikitoa misaada yake ya kibinadamu ikiwamo ya kuvisaidia vituo vya kulelea watoto wanaoishi katika mazingira magumu na wale yatima ambao wamekosa wazazi kutokana na shida mbalimbali.

Awali Rais wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya mkoani Dodoma, Twaha Nyange, aliomba taasisi zingine kusaidia watoto hao wanaoishi kwenye vituo mbalimbali kutokana na changamoto wanazokabiliana nazo.



Spika wa Bunge ambaye ni mlezi wa CCM Mkoa wa Kusini na Kaskazini Unguja na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, Job Ndugai, akicheza ngoma za utamaduni wa watu wa Mkoa wa Unguja, wakati akikagua ngoma hizo katika Ofisi ya CCM Mkoa wa Kaskazini Unguja juzi, mjini Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 94% wananchi wafikiwa huduma ya mawasiliano

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

ASILIMIA 94 ya wananchi wamefikiwa na huduma ya mawasiliano nchini, huku minara 530 ikisimikwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mhandisi Isaack Kamwelwe, wakati alipokuwa akifungua Baraza la Wafanyakazi wa wizara hiyo sekta ya mawasiliano.

Mhandisi Kamwelwe alisema mbali na hilo sekta hiyo imewezesha taasisi mbalimbali kutumia mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kukusanya mapato na kutoa huduma ndani ya serikali na wananchi.

Pia serikali kupitia sekta ya mawasiliano imekamilisha uandaaji wa mkakati wa taifa wa usalama wa mtandao.

Alisema katika kuhakikisha sekta ya mawasiliano inakua, serikali inashirikiana na taasisi mbalimbali zinazojihusisha na shughuli za mawasiliano zikiwamo sekta binafsi na wadau wengine katika kuendeleza kukuza sekta hiyo.

Alisema hadi sasa kuna laini zaidi ya milioni 45 za simu za mkononi na watumiaji wa intaneti wapatao milioni 23.

Aidha, serikali kupitia sekta hiyo imeendelea kuhamasisha matumizi sahihi ya huduma ya mawasiliano katika kudhibiti uhalifu mitandaoni.


Aliongeza kuwa serikali imekabidhi mtandao wa TTMS ambao utawezesha kukusanya mapato kutoka kwa watoa huduma za mawasiliano.

Naye Kaimu Katibu wa wizara hiyo, katika sekta ya mawasiliano Dk. Jim Yonazi alisema lengo la mkutano huo ni pamoja na kujadili mipango ambayo inatarajia kutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020.

Alisema kwa kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano na mifumo ya kielektroniki ya Tehama inafanya kazi ndani ya serikali pamoja na kwa mwananchi mmoja mmoja.

Dk. Yonazi alisema katika mwaka wa fedha wa 2019/2020, Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano, sekta ya mawasiliano iliidhinisha kutumia jumla ya Sh.18,856,423,000.

Alifafanua kuwa kati ya hizo Sh. bilioni 3.9 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na bilioni 1.9 ni za mishahara ya wafanyakazi, wakati bilioni 1.9 ni matumizi mengine.





Mafundi wakijenga miundombinu kwa ajili ya maabara ya Shule ya Sekondari Nyanja, iliyoko katika Kata ya Bwasi, Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara juzi. Shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 510. **NA MPIGA PICHA WETU**

# Spika Ndugai akumbusha wana CCM ushindi 2020

**Na Mwandishi Wetu,**

ZANZIBAR

MLEZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Kaskazini Unguja kichama, Job Ndugai, amewataka wana CCM wa Mkoa huo kutambua kuwa njia pekee ya kulinda Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha CCM inashinda na kubaki madarakani kwa kila uchaguzi wa dola.

Alisema kila mwanachama atumie nafasi yake kuhakikisha CCM inaendelea kustawi kisiasa, kiuchumi na kijamii na kukubalika kwa wananchi wote.

Kauli hiyo aliitoa katika ziara yake ya kujitambulisha na kuimarisha chama katika mkoa huo anaoulea akiwa ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa.

Ndugai alisema kuwa suala la ushindi wa CCM siyo mzaha bali ni jambo linalotakiwa kupewa kipaumbele kwa lengo la kulinda heshima, hadhi na urithi uliotukuka wa waasisi wa Muungano na Mapinduzi ya mwaka 1964.

Alisema kitendo cha CCM kukosa jimbo moja la uchaguzi ni sawa na kusaliti juhudi za viongozi waliokomboa nchi kutoka kwenye kiza cha ukoloni, utumwa na udhalilishaji.

Alieleza kuwa ni lazima viongozi waliopewa dhamana na CCM katika mkoa huo wafanyekazi kwa bidii na kuufuta upinzani ndani ya eneo hilo ambalo ni ngome ya CCM.

Ndugai ambaye pia ni Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alisema hatokuwa tayari kufanya kazi na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa mkoa huo ambao watakuwa wazembe katika ulezi wake. Alisema kuwa katika ulezi wake hatoweza kukubali kufanya kazi na wanachama hao na kwamba atakuwa mkali zaidi.

Aidha, alisema kuna baadhi ya watu hao wamekuwa wakibebwa, huku wakishindwa kufanya kazi ipasavyo ya kuisaidia chama na hatimaye kusababisha kuangusha utendaji wa CCM katika maeneo ya mkoa huo.

"Lazima chama kiwe na wanachama wenye nidhamu, lakini nitakuwa mlezi wa tofauti na mazingira ya Zanzibar nitakuwa mkali kidogo na niwaahidi kufanya kazi kwa ukaribu zaidi," alisema.

Alieleza kuwa katika nafasi yake ya kuwa mlezi atahakikisha anaendelea kuimarisha mkoa huo wa Kaskazini kuwa ngome ya CCM ili kushika nafasi za ngazi za udiwani, ubunge na uwakilishi.

"Nilipoambiwa kuwa ni mlezi wa chama katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na Kusini Unguja huku Zanzibar, moyo ulidunda kidogo nikasema nitaweza kweli kufanya kazi wakati siasa za huku nitofauti na za Bara, lakini nimejionea nitaweza," alisema.

Alisema kuwa kwa upande wa wabunge na wawakilishi ambao wanatoka katika maeneo ya mkoa huo, wanapaswa kutekeleza ahadi za utekelezaji wa ilani ya uchaguzi wa CCM na kwamba kufanya hivyo ndio njia pekee ya kuirejesha CCM madarakani.

Hata hivyo aliwataka wazazi na walezi wa mkoa huo kujenga utamaduni wa kuwaruhusu vijana wao wachangamkie fursa mbalimbali za kimaendeleo zilizopo katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara na Afrika Mashariki.

Aliwataka baadhi ya viongozi na wanachama ambao bado wanaendekeza makundi yasiyofaa ya kukigawa chama waache na badala yake washikamane kuleta maendeleo endelevu ndani ya taasisi hiyo.

Naye Mwenyekiti wa Mkoa huo, Iddi Ali Ame, alisema kaskazini ni ngome ya CCM na kwamba watahakikisha hawapotezi jimbo hilo kuanzia ngazi ya udiwani, uwakilishi hadi ubunge.

"Bado tunasafari ndefu tunatakiwa tukiimarishe chama kwa vitendo katika kutatua kero za wananchi na mambo tulioyaahidi katika utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya mwaka 2015," alisema.

# Mikakati yawekwa kupunguza vifo vya watoto

**Na Rahma Suleiman,**

ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Kinga na Elimu ya Afya Zanzibar, Dk. Fadhil Mohd Abdalla, amesema Serikali ya Zanzibar inaendelea kuweka mikakati ya kupunguza vifo vya watoto wachanga chini ya mwezi mmoja vinavyotokana na maambukizi ya wagonjwa ya watoto.

Aliitaja mikakati hiyo kuwa ni pamoja na kuhakikisha huduma za maradhi ya maambukizi yanayowasumbua watoto ndani ya wiki ya kwanza tokea kuzaliwa zinatolewa katika vituo vyote vya afya badala ya hospitali kuu pekee.

Dk. Fadhil alitoa kauli hiyo alipokuwa akifungua mafunzo ya madaktari wakufunzi kutoka nchi za Afrika Mashariki na Kati yaliyofanyika mjini Zanzibar.

Alisema Zanzibar imepiga hatua kubwa katika kupunguza vifo vya watoto wenye umri wa mwaka mmoja hadi mitatu, lakini vifo vya watoto wachanga wa siku saba za mwanzo tokea kuzaliwa bado imekuwa ni changamoto.

Mkurugenzi huyo alisema wizara itaendelea kufundisha madaktari wa vituo vya afya msingi ili kuhakikisha kila kituo kinaweza kutoa tiba ya maambukizi.

"Lengo ni kuhakikisha dawa za maambukizi zilizokuwa zikitolewa hospitali kuu sasa zinasambazwa katika vituo vya afya ili kupunguza vifo vya watoto wachanga," alisema Dk. Fadhil.

Naye Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Ofisi ya Brazzaville Congo, ambaye ni mtaalamu wa afya ya watoto wachanga, Dk. Assumpta Muriizhi, alisema kinamama wanapitia kipindi kigumu katika kipindi cha miaka miwili baada ya kujifungua kutokana na kupambana na afya ya mtoto ambaye hawezi kujieleza.

Alisema wapo baadhi ya wazazi hawaoni umuhimu wa kuwapeleka watoto wao hospitali wanapopata maambukizi jambo linalosababisha kuathirika zaidi na hatimaye kupoteza maisha.

Aliwashauri kinamama wanapogundua watoto wao wachanga wanasumbuliwa na maradhi, kuwaharakisha mapema katika vituo vya afya kupata huduma ya awali kabla ya kuwapeleka hospitali kuu iwapo matatizo yataongezeka.

Alisema hakuna umuhimu mkubwa kwa watoto wachanga kuwaanzisha huduma za afya katika hospitali kuu hasa kwa Zanzibar ambapo vituo vya afya vinapatikana kila sehemu.

Mkutano huo umewajumuisha madaktari wa wataalamu wa watoto wachanga kutoka Zambia, Zimbabwe, Msumbiji, Kenya, Uganda, Tanzani Bara, Zanzibar na maofisa wawakilishi wa mashirika ya kimataifa ya WHO na UNICEF.

# Wanaume wadaiwa kukacha upimaji VVU

**Na Mwandishi Wetu,**

ZANZIBAR

WATU wanaoishi na virusi vya Ukimwi wamesema ushiriki wa wanaume kupima afya zao kwa hiari ni mdogo hali ambayo inasababisha kuongezeka kwa maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Hayo yameelezwa na Mratibu wa Huduma na Tiba kwa wanaoishi na VVU, Maryamu Ali Khamis, wakati akitoa mada kwa waandishi wa habari katika semina ya kuwajengea uwezo kuripoti habari za Ukimwi, semina ambayo imeandaliwa na Kanisa la Anglikana Zanzibar.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 47.2 ya wanaume ndio waliojitokeza kupima virusi vya ukimwi kwa mwaka 2017, wakati wanawake ni asilimia 52.7.

Alisema bado wanaume ndio vikwazo katika huduma hizo kwa sababu hawajawa na utayari wa kupima afya zao kwa hiari.

Alieleza kwamba sababu nyingine inayochangia wanaume kukataa kupima afya zao kwa hiari ni hali ya unyanyapaa iliyojengeka kwa jamii.

Akizungumza katika semina hiyo, Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana, Michael Hafidh, aliwataka waandishi wa habari kutoa elimu kwa wanaume kupima afya zao ili kuweza kujikinga na maambukizi ya virusi vya ukimwi.

Alisema kuwa waandishi wa habari wana nafasi kubwa katika kutoa elimu ya masuala mbalimbali kwa sababu kazi zao zinauwezo wa kufika mbali na kusikilizwa.

Aidha, aliwataka wanaume kutokuwa waoga kwenda kupima afya zao ili kuweza kupunguza maambukizi ya virusi vya ukimwi.

Kwa upande wake Mratibu wa Huduma za Ushauri Nasaha na Upimaji wa VVU Zanzibar, Tatu Bilal Ali, alisema serikali imeandaa mikakati mbalimbali ya kukabiliana na ugonjwa huo ikiwamo utoaji wa ushauri nasaha kwa jamii, kuheshimu haki na maadili ya kitabibu na kuepuka kumpima mtu virusi bila ya ridhaa.

Alisema pia imekuwa ikitoa taaluma ya njia bora za kujifungua na unyonyeshaji pamoja na ulezi mzuri wa mtoto ili kujikinga na virusi vya Ukimwi.

HABARI KIMATAIFA

# Jeshi latoa tamko kumtaka Bouteflika ajiuzulu

**ALGIERS,** Algeria

MKUU wa majeshi Algeria, Jenerali Ahmed Gaid Salah, ametaka mchakato wa kikatiba uanzishwe kumtangaza Rais wa nchi hiyo, Abeldaziz Bouteflika hana uwezo wa kuiongoza tena nchi hiyo.

Kauli ya Jenerali Salah imetolewa baada ya maandamano ya umma yaliyodumu kwa zaidi ya mwezi mmoja yakimtaka Rais Bouteflika aondoke madarakani baada ya kuiongoza Algeria kwa miaka 20.

Akizungumza kupitia televisheni ya Algeria, Jenerali Salah alisema hilo ndilo litakuwa suluhisho pekee la kuleta utulivu wa kisiasa nchini humo.

"Nchi yetu imeshuhudia maandamano ya amani, watu wakitaka mabadiliko ya kisiasa. Hivyo nawaomba wote tuonyeshe uzalendo kwa maslahi ya taifa letu. Suluhisho litakalosaidia kupatikana kwa utulivu wa kisiasa ni kupitia katiba ambayo tunaiheshimu. Suluhisho ni kutumia kifungu cha 102 cha katiba ya Algeria," alisema Jenerali Salah.

Kiongozi huyo wa kijeshi alisema chini ya kifungu hicho, Baraza la Katiba linaweza kuamua kwamba rais ni mgonjwa mno na hawezi kutekeleza majukumu yake na ameliomba Bunge la Algeria kumtangaza Bouteflika kuwa ni mtu asiye na uwezo tena.

Kulingana na katiba ya Algeria, iwapo ombi hilo litakubaliwa kwa wingi wa theluthi mbili na wabunge wa nchi hiyo, Spika wa Bunge atachukua madaraka ya serikali hadi uchaguzi wa rais utakapofanyika.

Wakati hayo yakijiri, kiongozi wa chama cha Democratic National Rally, Ahmed Ouyahia ambaye aliwahi kuwa Waziri Mkuu wa nchi hiyo alimtaka Rais Bouteflika kujiuzulu.

Chama hicho ni moja kati ya vyama vinavyounda serikali ya muungano inayotawala Algeria na ambacho kina ushawishi mkubwa na kimekuwa kikimuunga mkono Boutelfika kwa muda mrefu.

Alisema chama hicho kinamtaka kiongozi huyo ajiuzulu kulingana na kifungu cha 102 kilichopo kwenye aya ya nne ya katiba ya Algeria, ili kuruhusu kipindi cha amani cha mpito.

Baadhi ya waandamanaji walitoa wito wa kutumika kwa kifungu cha 102 kwa lengo la kumuondoa Bouteflika madarakani, tangu Februari 22, yalipoanza maandamano ya kila Ijumaa ya kuupinga utawala wa wake.

Maandamano hayo yamekuwa yakiungwa mkono na chama cha RND pamoja na Chama tawala cha National Liberation Front, FLN.

**DW**



Wahamiaji haramu wakiwa katika meli Bahari ya Mediterania wakisafirishwa kuelekea nchi za Ulaya. **PICHA: REUTERS**

# Tume Comoro yamtangaza Azali kuwa Rais

**MORONI,** Comoro

TUME ya Uchaguzi Visiwa vya Comoro, jana ilimtangaza Azali Assoumani kuwa Rais wa nchi hiyo, baada ya kupata ushindi wa asilimia 66.77 ya idadi za kura zilizopigwa.

Assoumani alimshinda mpinzani wake, Mahamoudou Ahamada aliyeshika nafasi ya pili baada ya kupata asilimia 14.62 ya idadi ya kura zilizopigwa.

Lakini kabla ya matokeo hayo kutangazwa, vyama vya upinzani nchini humo vilikwishayapinga ukidai kuwa upigaji kura uliandamwa na kasoro nyingi ambazo ziliripotiwa tume ya uchaguzi.

Ahamada alitoa wito kwa wananchi wa Comoro kusimama kidete na kuyapinga matokeo hayo na kuitaka jumuiya ya kimataifa kutoutambua ushindi wa Azali.

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi, Rais Assoumani alikiri kutokea kwa kasoro wakati wa upigaji kura siku ya Jumapili.

"Ni kweli makosa yalifanyika, lakini tunafurahi kwa sababu hali ingeweza kuwa mbaya zaidi. Tunajipongeza na kumshukuru Mungu na Wakomoro," alisema Azali na kuongeza kuwa.

"Kama nilivyosema, kipindi kigumu zaidi kiko mbele; ni kujenga nchi na namwalika kila mmoja kushiriki."

Zoezi la kuhesabu kura lilikumbwa na mivutano ambayo ilihusisha matumizi ya nguvu za dola na maandamano ambapo watu 12 walijeruhiwa baada ya Jeshi la Polisi kutumia risasi kuwazuia wafuasi wa wagombea wa upinzani katikati ya Jiji la Moroni.

Mgombea urais aliyeshika nafasi ya tatu, Mwinyi-Baraka Said Soilihi, alisema hayatambui matokeo hayo pamoja na mchakato wote wa uchaguzi.

"Kwetu sisi kilichofanyika ni mapinduzi badala ya uchaguzi. Mapinduzi yaliyopangwa na Azali na timu yake kwa kulishirikisha jeshi. Tuliwaona wanajeshi wakibeba visanduku vya kura katika vituo vingi, hususani katika visiwa vya Anjouan na Moheli," alisema Soilihi.

Wapinzani wakuu wa Rais Azali, akiwamo Ahmed Abdallah Sambi walizuiliwa na mahakama kuu kugombea kutokana na tuhuma za ufisadi.

Mkurugenzi wa kampeni wa Rais Azali, Houmed Msaidie alitupilia mbali ukosoaji wa wapinzani na aliwashutumu kuwa na nia ya kuweka mazingira ya hofu ili kuhujumu uhalali wa mfumo wa uchaguzi, amewashauri walio na malalamiko kuyapeleka katika taasisi zinazohusika.

Rais Azali aliingia madarakani kwa mara ya kwanza kupitia mapinduzi ya kijeshi mwaka 1999, baadaye alishinda uchaguzi wa rais ulioandaliwa mwaka 2002 na wa mwaka 2016. **DW**

## KWA UFUPI

### Rais Tshisekedi kufanya ziara Marekani

**KINASHASA,** Congo

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Felix Tshisekedi, anatarajia kufanya ziara mjini Washington Marekani Aprili mwaka huu.

Kwenye ziara hiyo, Rais Tshisekedi anatarajia kukutana na Waziri wa Mambo ya Nje Marekani, Mike Pompeo, wanatarajia kujadiliana kuimarisha uchumi na usalama, pamoja na namna ya kupambana na mlipuko wa ugonjwa wa ebola mashariki mwa Congo.

Msemaji wa Pompeo, Robert Palladino alisema Rais Tshisekedi atatembelea Washington kuanzia Aprili 3 hadi 5, pamoja na kukutana na Pompeo, na maofisa wengine wa juu wa utawala wa Rais Donald Trump.

Alisema haijajulikana kama Rais Tshisekedi atakutana na Rais Trump.

"Tunaungana na matakwa ya Rais Tshisekedi ya kutaka kujenga uhusiano thabiti kati ya Marekani na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo," Palladino aliwaambia waandishi wa habari.

Alisema suala la kupambana na mlipuko wa ugonjwa wa ebola Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kulikogubikwa na vita litakuwa ni moja ya mambo yatakayojadiliwa.

**VOA**

### Wanafunzi waliokamatwa Burundi waachiwa

**BUJUMBURA,** Burundi

WAZIRI wa Sheria nchini Burundi, Aimée Laurentine Kanyana, amesema Mahakama Kuu nchini humo imewaachilia huru wanafunzi watatu wa kike ambao walikamatwa wakishutumiwa kuichafua picha ya Rais wa nchi hiyo, Pierre Nkurunziza kwenye vitabu vyao vya shule.

Wanafunzi hao walishikiliwa kwa muda wa wiki mbili kwa shutuma za kumtusi Rais Nkurunziza, ambapo baadaye kulizusha kampeni mitandaoni za kutaka wasichana hao waachiliwe, kampeni iliyokuwa na jina #FreeOurGirls, watu wakituma picha kwenye mitandao ya kijamii.

Waziri Kanyana alisema wasichana hao wenye miaka 15, 16 na 17 wameachiwa huru kwa muda.

"Tunawataka wazazi kuboresha elimu ya watoto wao. Tunawakumbusha watoto kuwa wanapaswa kuheshimu mamlaka na kuwa umri wa kuwajibishwa ni miaka 15," alisema Kanyana.

Wanafunzi hao walikamatwa walipokuwa katika shule ya ECOFO iliyopo katika Mkoa wa Kaskazini wa Burundi wa Kirundo Machi, 12 mwaka huu.

Awali walioshtakiwa walikuwa wanafunzi saba, lakini wanne wakaachiliwa huru. Watatu hao walikuwa wanashikiliwa kwenye Gereza la Wanawake la Mkoa wa Ngozi.

Mwaka 2016 shule mbalimbali mjini Bujumbura na mikoani, watoto kadhaa walikamatwa wakihusishwa na matukio ya aina hiyo, Shirika la Kutetea Watoto FENADEB lilikuwa mstari wa mbele kuwatetea watoto hao.

Mashirika ya kutetea haki za watoto nchini Burundi yameshauri uchunguzi wa kina ufanyike kabla ya kuwakamata watoto hao ili kubaini ni kwa nini matukio kama hayo yanajitokeza.

**BBC**

## IFM kujenga tawi Simiyu

**Na Happy Severine,** SIMIYU

CHUO cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kimeahidi kujenga tawi jipya wilayani Bariadi mkoani Simiyu katika Kata ya Sapiwi, Tarafa ya Dutwa ili kusogeza huduma ya elimu karibu na wananchi.

Akizungumza jana na viongozi wa Mkoa wa Simiyu baada ya kutembelea eneo la ujenzi, Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Tadeo Satta, aliwahahakikishia viongozi hao kujenga tawi hilo ili kuwasogezea huduma wananchi wa mkoa huo.

Aidha Satta, aliwashukuru viongozi wa Mkoa wa Simiyu kwa kutoa eneo la ekari 20 bure na kuahidi kushirikiana na Serikali ya Mkoa ili kuhakikisha ujenzi unakamilika kwa wakati.

Profesa Satta pia alisema watashirikiana katika hatua zote ikiwamo upimaji wa eneo hadi ujenzi na ukamilishaji wa majengo ya chuo.

Awali akizungumza na viongozi hao Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, alisema serikali mkoani humo iko tayari kushirikiana na viongozi wa chuo hicho kwa kutoa wataalam watakaosaidia katika usimamizi wa upimaji huku akiwashauri ujenzi wa majengo ya chuo hicho ufanyike kwa kutumia mfumo wa 'Force Account' ili kupunguza gharama za ujenzi.

Alisisitiza kuwa mfumo huo utapunguza gharama kwa kuwa hautumii wakandarasi badala yake ujenzi utafanywa na mafundi wa kawaida wakisimamiwa na wahandisi wa ujenzi mkoa na halmashauri.

Mtaka amemhakikishia makamu huyo kuhusu upatikanaji wa wanafunzi kwa kuwa hadi sasa mkoa huo bado una vyuo vichache vya elimu ya juu, huku akibainisha serikali imeshatoa ardhi bure kwa ajili ujenzi wa matawi ya vyuo mbalimbali vya elimu ya juu.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, Jumanne Sagini, alisema wanaendelea kushawishi taasisi nyingi za elimu ya juu kujenga matawi yake mkoani Simiyu ili kutoa nafasi kwa wana-Simiyu kupata elimu ya juu itakayochangia kuleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi, kijamii na kifikra.

# Wanawake watakiwa kuchunguzwa mabusha

**Na Boniface Gideon,** TANGA

WANAWAKE wameshauriwa kwenda kwenye vituo vya afya wanapoona dalili za uvimbe sehemu za siri, kwenye matiti na mikono kwa kuwa dalili hizo ni uwezekano wa kuwa na magonjwa yasiyopewa kipaumbele kama matende, mabusha na minyoo.

Akizungumza wakati wa kuwajengea uwezo walimu wa walimu, mratibu wa magonjwa yasiyopewa kipaumbele Jiji la Tanga, Dk. Nassoro Said Nassoro, alisema wanatarajia kulifanya zoezi hilo katika awamu mbili kwa mwezi Machi na Aprili kwa kutoa dawa za minyoo shule zote za msingi 103 za Tanga.

"Hata mwanamke anaathirika na magonjwa haya ya mabusha na matende, wanapofika hospitali tumeona kuna changamoto ya wagonjwa wanawake ambao tayari wameshaathirika na ugonjwa huu," alisema.

Alisema wanawake wenye tatizo hilo wapo majumbani kwa kushindwa kujieleza kuwa na tatizo na kuwaasa wanapoona dalili za uvimbe sehemu za siri wajitokeze kupata tiba.

Aliwasisitiza wakazi wa Tanga kuacha dhana potofu ya kuwa ukinywa dawa hizo kuna hatari ya kupoteza nguvu za kiume, kuwa jambo hilo si kweli kwa kuwa dawa hizo zimekwisha pimwa na kuthibitishwa na wataalamu kwa kiwango cha juu.

"Napenda kuwatoa hofu wakazi wa Tanga kwamba dawa hizi hazina madhara yoyote ni nzuri na zina faida kubwa kwa jamii kwa sababu zinatengeneza nguvu kazi na kuwapa afya njema watoto wetu waweze kuhakikisha hawadumai na wanakuwa na uwezo mzuri wa kusoma na kuzingatia masomo yao," alisema.

Halmashauri ya Jiji la Tanga imesema inatarajia kutoa dawa kwa jamii za magonjwa yasiyopewa kipaumbele na imelenga kutoa dawa za minyoo, mabusha na matende.

Dk. Nassoro alisema mgonjwa mmoja asipokunywa dawa kuna uwezekano mkubwa wa kueneza ugonjwa huo kwa watu wengine na kuwaasa wazazi, walezi na walimu kuhakikisha watoto wanajitokeza kwa wingi wenye umri wa kwenda shule ambao wapo nyumbani na waliopo shuleni kufika katika shule iliyo karibu kunywa dawa hizo.

Katika hatua nyingine Dk. Nassoro alisema lengo kubwa ni kuhakikisha kila mkazi wa Tanga anapata dawa hizo ili ifikapo mwaka 2020 ugonjwa huo uwe umekwisha kabisa.

Alisema malengo ya kidunia ni kuhakikisha ifikapo 2030 magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele yawe yametokomezwa kabisa duniani.

Kwa upande wake Mfamasia Msaidizi wa Tanga Jiji, Ally Hamza, alisema wametoa elimu kwa walimu watakaotekeleza utoaji wa dawa kwa magonjwa hayo na kwamba bado kuna wagonjwa wengi ambao hawajabainika kutokana na kutofika vituo vya afya.




Daktari bingwa wa magonjwa ya macho, Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha IMTU ambaye ni Daktari Mshauri Mualikwa wa Hospitali ya Macho ya Kimataifa (The International Eye Hospital), Dk. Luke Siyame, akimfanyia uchunguzi wa macho, Happynes Kumburu kando ya Mkutano wa Utafiti wa Afya na Sayansi wa Afrika Mashariki ulioanza jana, jijini Dar es Salaam katika Ukumbi wa Mikutano Mwalimu Nyerere. **MPIGAPICHA WETU**

# Vodacom sasa kuzifikia ofisi za nyumbani, SME, kampuni kubwa

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA jitihada za kuhakikisha biashara zinaenda na mabadiliko ya masoko ya kisasa, Kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania PLC, jana, imezindua kitengo kwa ajili ya kushughulikia huduma zinazoendana na mahitaji ya wateja wake wanaofanya biashara kuanzia kampuni ndogo-ofisi ndogo za nyumbani (Soho's), wafanyabiashara wa kati (SMEs) na kampuni kubwa.

Taarifa iliyotolewa na Vodacom Tanzania PLC, jana ilisema lengo kuu la huduma hiyo ni kuwawezesha kufanya biashara kwa ufanisi zaidi, kuhimili ushindani, kujenga mtandao wa kibiashara na kuwawezesha kupata huduma zote za kurahisisha biashara zao bila kuhangaika na masuala yaliyo nje ya biashara zao za msingi.

"Ulimwenguni kote kumetokea mabadiliko ya njia za kufanya biashara kutoka njia za zamani kwenda njia za kidijitali, kutumia mitandao na teknolojia za kisasa kama cloud, tunatarajia wateja wetu kwenda sambamba na mabadiliko haya ili kufanya biashara zao kwa ufanisi na kuhimili ushindani katika masoko nasi tunaamini ni wabia wao muhimu katika kuleta ufumbuzi wa kufanikisha biashara zao," alisema Hisham Hendi, Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania PLC.

Kampuni kubwa kama benki na sekta ya umma zinatafuta ufumbuzi wa ubunifu ambao utarahisisha shughuli za uendeshaji, kuhimili ushindani na kuhakikisha mali zake ziko salama.

Msukumo wa kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda umesaidia kuanzishwa kwa biashara ndogo na za kati ambazo uendeshaji wake kwa ufanisi unahitaji huduma za ubunifu wa kiteknolojia za kisasa ili kuzipunguzia gharama za uendeshaji.

"Vodacom ina dhamira ya kufanikisha ukuaji wa biashara nchini Tanzania kupitia ubunifu wake wa huduma za teknolojia ya kidijitali za kuwarahisishia wafanyabiashara kufanikisha malengo yao na kujiandaa kwa siku zijazo na ndio maana tumewaletea huduma hizi," Hendi alisema.

Biashara zenye ukubwa wa kati kama asasi zisizo za kiserikali (NGO's), ambazo zimejipanga kuendesha shughuli zake kwa njia za kisasa na ambazo zinatoa kipaumbele kutumia teknolojia za kisasa, zitafaidika na huduma kama IoT (Internet of Things), SIM Manager na utumaji wa ujumbe wa maneno kwa watu wengi kwa wakati mmoja (bulk SMS).

Kwa upande wa biashara ndogo na ofisi ndogo za nyumbani (Soho's), zitanufaika kwa kubana matumizi na kujenga mtandao wa biashara kupitia huduma ya M-Pesa, huduma za kurahisisha biashara na utumaji wa ujumbe wa maneno kwa watu wengi kwa pamoja wataweza kubadilisha biashara zao na kuzifanya kukua zaidi.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 27/03/2019

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumapili tarehe 28/03/2019 kampuni ya **OSAKA COMPANY LIMITED** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **CHALINZE** kupitia VIGWAZA gari hilo lenye namba za usajili:

   **T567 AUX/T695 BFS**


2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   - Urefu - mita 22.00
   - Upana - mita 2.84
   - Kimo - mita 5.20

3. Gari litasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215143902

### CHETI KIMEPOTEA



**ABDUL-SWAMAD M. KHAMIS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba P0391-0730 kilichotolewa na HAILE SELASSIE SEKONDARI mwaka 2004.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: CD/IR/RB/2012/2019.**

115141702

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGORO.**
**MAOMBI NA.19 YA MWAKA 2019.**

**KULWA DIONIZI LUSANA...............MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**

1. **NATIONAL MACROFINANCE BANK PLC**
2. **LJ INTERNATIONAL LIMITED**
3. **MAJIGE SIMON MZULUNGI**
4. **NATIONAL BANK OF COMMERCE............WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**MAJIGE SIMON MZULUNGI...........MJIBU MAOMBI**

Popote Ulipo Unaarifiwa Ufike ktk baraza la ardhi na Nyumba la wilaya ya Morogoro tarehe 29/04/2019 mwenyewe binafsi au mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautaudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa mkono wangu leo tarehe 25 Mwezi MARCH,2019.

215142902

### VYETI VIMEPOTEA



**MWANAIDI MGAYA** anatangaza kupotelewa na **CHETI CHA UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU** chenye namba AC No: 22435 kilichotolewa na **CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA TAWI LA MTWARA** mwaka 2011. Cheti cha **STASHAHADA YA UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU** chenye namba DC No: 0017191 kilichotolewa na **CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA TAWI LA MTWARA** mwaka 2013-2014.

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: MAG/RB/7781/2019.**

1151423O2

### CHETI KIMEPOTEA



**LYDIA MICHAEL SHILLA** anatangaza kupotelewa na CERTIFICATE OF BACHELOR OF SOCIAL SCIENCE DEGREE kilichotolewa na UNIVERSITY OF CAPE TOWN kilichopo NCHINI AFRIKA KUSINI mwaka 2012.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi:**

**Taarifa ya polisi: OB/RB/2951/2019.**

115142402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA:56..2019**
**Mdai: SALOME SAIMON MBIRO**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: JOYCE LEONARD MABULA**

Kwa:
JOYCE LEONARD MABULA
MKITI RUGEMEREZA

Ombi la Mdai:
SALOME SAIMON MBIRO
Madai ya: PESA SHILINGI 850,000/= NA GHARAMA ZA KESI ERV.

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 04 mwezi 04 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 27 mwezi 03 mwaka 2019.

215142802

**MARMO CIVIL & BUILDING ENGINEERING**
**IYUNGA INDUSTRIAL AREA,**
**TEL : + 255 25 2562017/18**
**MBEYA.**

INATANGAZA KUPOTELEWA NA BLUE KADI YA PIKIKPIKI YENYE USAJILI WA NAMBA T 728 CFB ILIYOTOLEWA NA TRA.

KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ANAOMBWA KUTOA TAARIFA KITUO CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI :
**MB1/RB/297/2019.**

215143602

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BENNY RUMISHAEL** MAKUNDI anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 622 BRY MITSUBISHI** FUSO. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **RHE/RB/435/2019.**

115142202

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BONART RAYMOND** ISHENGOMA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 595 DCC SUZUKI CARRY.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/4641/2019.**

115142102

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BARIKIEL DAVIS MTUI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 592 DJV** MITSUBISHI CANTER. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KMR/RB/2212/2019.**

115142102

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BW. APOLEI WILBOAD** anatangza kupotelewa na Kadi ya gari la Shirika la MEDICAL MISSIONARY OF MARY yenye namba za usajili **T832ACU** aina ya Mitsubishi, Chassis namba **C1044VKJ400144** na Engine namba **4056CB5760.**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. **KTS/RB/827/2019.**

115143302

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**HEDEB KHAMIS HEDEB** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Mitsubishi ROSA. yenye namba za usajili **T680 BNC. CHASSIS** Namba. **BE632G00592** na ENGINE Namba. **4M51EAA0592** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa **Polisi.TAN/RB/559/2019.**

115141602


## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

**Nipashe**

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# WAKALA

## wa Pogba ataka mshahara wa Euro milioni 16

**LONDON,** England

WAKALA wa Paul Pogba, Mino Raiola, atataka kumfanya mshindi huyo wa Kombe la Dunia kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa mshahara mkubwa zaidi duniani kama kiungo huyo ataondoka hapo Manchester United kipindi cha majira ya joto.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 anaingia kwenye awamu ya pili ya mkataba wake wa sasa hapo Old Trafford akiwa amerudi kwa mara ya pili akitokea Juventus mwaka 2016 kwa ada ya thamani ya pauni milioni 94.5.

Lakini sasa Pogba anazivutia klabu kubwa Ulaya baada ya kuwa na wakati mgumu mwanzo pale Manchester United, ambako alikuwa hana uhusiano mzuri na kocha Jose Mourinho.

Klabu za Real Madrid na Juventus ndizo zinazoongoza kuinyatia saini ya Pogba kipindi hiki cha majira ya joto na Gazeti la Tuttosport limedai kwamba Raiola ameziambia klabu zinazomwania kuwa zitaingia gharama ya kumlipa mshahara wa Euro milioni 16 kwa mwaka kama ataondoka Old Trafford.

Hiyo itamfanya Pogba kuwa mbele ya Gareth Bale (Euro milioni 14) ama Sergio Ramos (Euro miloni 11) ambao ndio wanaolipwa zaidi pale Real Madrid, huku Cristiano Ronaldo akiwa analipwa zaidi ya hapo kule Juventus.

Tuttosport limeongeza kwamba, Juventus wanaweza kuumudu mshahara huo, ingawa Pogba anafikiria zaidi kwenda Real Madrid ambako ameitaja kama klabu ya ndoto zake.



# JUVENTUS:

## Ronaldo fiti kuivaa Ajax

**TURIN,** Italia

CRISTIANO Ronaldo alikuwa na maumivu madogo kwenye paja wakati wa mchezo wa Ureno wa kufuzu Euro 2020 dhidi ya Serbia Jumatatu, Juventus imethibitisha.

Ronaldo alitolewa uwanjani dakika ya 31 kwenye mchezo uliopigwa jijini Lisbon baada ya kuumia wakati akiuwahi mpira.

Baada ya mchezo huo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alisisitiza kwamba hakuumia kwa kiwango kikubwa na kwamba ana matumaini ya kuwa fiti kwenye mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Juventus itacheza na Ajax kwenye mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Aprili 10, mwaka huu, na Ronaldo aliwaambia waandishi wa habari: "Najua kwamba nitaweza kurudi uwanjani baada ya wiki au wiki mbili."

Juve sasa imethibitisha kwamba alikuwa na maumivu kidogo kwenye paja na atarudi uwanjani mapema.

Taarifa ya klabu hiyo katika tovuti yake ilisema: "Cristiano Ronaldo alifanyiwa uchunguzi baada ya mchezo wa Ureno na ilionyesha kwamba hakuumia kwa kiwango kikubwa paja lake la mguu wa kulia.

"Hali yake itaimarika ndani ya wiki moja au mbili zijazo na atakuwa fiti kurudi uwanjani."

Juventus ambao ni vinara wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, watawavaa Empoli, Cagliari na AC Milan kabla ya kwenda Amsterdam kucheza na Ajax.

# Barca kukamilisha usajili wa De Ligt

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, amefanya mazungumzo na maofisa wa Ajax wiki hii kwa ajili ya kujadiliana mpango wa kumsajili beki, Matthijs de Ligt (pichani chini), mwishoni mwa msimu huu.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, tayari wameshakamilisha usajili wa mchezaji mwenza wa De Ligt, Frenkie de Jong, lakini sasa Barca wanataka kumaliza haraka makubaliano na beki huyo wa kati wa Ajax mwenye umri wa miaka 19.

Habari zinadai kwamba, Bartomeu, aliongozana na ofisa mtendaji wa Klabu, Oscar Grau, walisafiri hadi Uholanzi ambako kulikuwa kunafanyika mkutano wa Chama cha Klabu za Ulaya, na baadaye wakapata muda wa kuzungumza na Ofisa Mtendaji wa Ajax, Edwin van der Sar juu ya De Ligt.

Barcelona tayari imeshaweka wazi kwamba inataka kumaliza haraka mazungumzo na Ajax, huku De Ligt mwenyewe akibainisha kwamba yupo tayari kukamilisha usajili wa kutua hapo Camp Nou kabla ya mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Juventus.

Barcelona inaendelea kukijenga kikosi chake, huku tayari ikiwa na uhakika wa saini za Luka Jovic na Matthijs de Ligt pamoja na nyota wengine Ousmane Dembele, Phil Coutinho, Arturo Vidal, Malcom, Arthur, Clement Lenglet na Frenkie de Jong ambao wamesajiliwa kwa kipindi cha miezi 18 iliyopita.

"Jina langu linatokea kwenye vyombo vya habari, lakini kwa sasa akili yangu ni kucheza tu," amesema De Ligt, akinukuliwa na Sport.

De Ligt amechezea mechi 42 akiwa na Ajax msimu huu.



# EMERY atoa mbinu kwa Arsenal kumaliza 4-bora

**LONDON,** England

UNAI Emery (pichani chini), amewapa changamoto Arsenal kuonyesha kiwango kama walivyocheza dhidi ya Manchester United kwa kipindi chote kilichobaki cha msimu huu ili kuweza kumaliza kwenye nne-bora Ligi Kuu England.

Arsenal ilijivuta juu ya kikosi cha Ole Gunnar Solskjaer baada ya kuifunga United mabao 2-0 kwenye mchezo uliopigwa Uwanja wa Emirates Machi 10, mwaka huu.

Huku Tottenham wakiwa nafasi ya tatu wakiwapita 'Washika Bunduki' hao pointi moja na Chelsea ikiwa nafasi ya sita, hivyo kuna ushindani mkubwa wa kuwania nafasi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Emery anajiamini kwamba timu yake ina uwezo wa kumaliza ligi ikiwa nafasi ya nne, lakini pia wana kibarua cha kushinda kwenye Kombe la Europa, kwani watacheza dhidi ya Napoli kwenye hatua ya robo fainali.

Akizungumza baada ya ushindi wa 3-2 katika mchezo wa kirafiki dhidi ya Al-Nasr kule Dubai Jumanne, Emery alisema: "Ni majukumu yetu, lakini tunajua kwamba tuna kazi ya kufanya. Tumejiandaa kuhakikisha tunashinda na kumaliza nafasi nne za juu.

"Sasa zimebaki mechi nane ligi kumalizika, tunahitaji kucheza kama tulivyocheza dhidi ya Manchester United. Tunajua kwamba tupo kwenye wakati mgumu kwa sababu tunakabiliwa na mechi dhidi ya timu kubwa."





# VAN GAAL:

## Man ya Solskjaer kama ya Mourinho tu

**LONDON,** England

KOCH wa zamani wa Manchester United, Louis van Gaal, amesema staili ya uchezaji wa klabu hiyo haijabadilika chini ya Ole Gunnar Solskjaer.

Wakati vyombo vya habari vikiripoti siku ya Jumatatu kuwa Solskjaer anatarajiwa kukabidhiwa jumla kuinoa United kwa mkataba wa muda mrefu, Van Gaal ameibuka na kusema hakuna mabadiliko ya kiuchezaji ndani ya timu hiyo.

Solskjaer mwenye umri wa miaka 46, ameshinda jumla ya michezo 14 kati ya mechi 19 tangu kukabidhiwa timu hiyo Desemba mwaka jana akirithi mikoba ya Jose Mourinho aliyetimuliwa.

Van Gaal, ambaye naye alipitia wakati mgumu akiwa Old Trafford kama ilivyo kwa Mourinho, amesema kuwa Solskjaer amefanikiwa, lakini anaamini aina ya uchezaji ndani ya klabu hiyo ya kupaki basi haijabadilika.

"Kocha aliyenifuatia baada yangu mimi ambaye alikuwa Mourinho alibadilisha staili," alisema kocha huyo raia wa Uholanzi akinukuliwa na BBC.

"Kwa sasa kuna kocha ambaye anapaki basi na kucheza mashambulizi ya kushitukiza, lakini tofauti kubwa iliyopo kati ya Mourinho na Solskjaer ni kwamba Solskjaer anashinda.

"Mimi siko pale, lakini hali inaonekana imetulia kwa sasa na mazingira yamekuwa mazuri. Ukweli ni kwamba Solskjaer amembadilisha, Paul Pogba katika eneo alilokuwapo mwanzo na kumuweka sehemu muhimu zaidi.

"Lakini namna Manchester United inavyocheza kwa sasa ni tofauti na ilivyokuwa ikicheza chini ya Sir Alex Ferguson. Inacheza mpira wa kujilinda na kushambulia."

Van Gaal anaamini kuwa Solskjaer anayo nafasi ya kusonga mbele kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na pointi ya kuzingatia ni kwamba kama atafanikiwa kwenye hilo itamdharaulisha Mourinho.

"Anaweza kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa sababu anacheza mfumo wa kujilinda ambao ni ngumu sana kufungwa iwe unapenda hilo ama hupendi na ni matokeo ya kazi ya Mourinho."

United imezidiwa pointi mbili na Arsenal yenye alama 60 inayoshika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, huku ikitarajiwa kukutana na Barcelona hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwezi ujao.

# Ramos amkana Zidane Madrid

**MADRID,** Hispania

SERGIO Ramos amesema sio yeye aliyeamua Zinedine Zidane arudi Real Madrid, kauli hiyo ilikuja wakati nahodha huyo wa Hispania alipoutoa ushindi wa Jumanne kwa kocha wa timu ya Taifa, Luis Enrique.

Zidane aliteuliwa tena kuwa kocha wa Madrid baada ya kuiongoza kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya tatu mfululizo msimu uliopita.

Jose Mourinho alikuwa akihusishwa na mpango wa kutua kwa miamba hao wa mji mkuu wa Hispania, hata hivyo, kulikuwa na uvumi ukidai kwamba, Ramos alikuwa nyuma ya maamuzi ya kumrudisha Zidane baada ya kufukuzwa kwa Santiago Solari.

Akizungumzia kuhusu kurudi kwa Zidane baada ya mchezo wa Hispania kuifunga Malta 2-0 kwenye mechi ya kufuzu kwa michuano ya Euro 2020, Ramos aliwaambia waandishi wa habari: "Mabadiliko yanaweza kuleta hali chanya, tulikuwa na wakati wa kufurahisha chini ya Zizou na ni furaha tena kurudi nyumbani.

"Kurudi kwake imekuwa habari njema kwa wachezaji wote, hayakuwa maamuzi yangu kumleta tena hapa, hata kama watu wanafikiri hivyo.

"Mimi ni nahodha na huwa natoa mawazo yangu kama nikiombwa; siwezi kulazimisha, au kufanya ninachotaka."

Alvaro Morata alifunga mara mbili kwenye ushindi huo wa Malta, ambapo Hispania ilimkosa kocha wake, Luis Enrique kutokana na matatizo ya kifamilia.

Robert Moreno ndiye alikuwa kwenye benchi kuiongoza Hispania badala ya Enrique na nahodha Ramos aliutoa ushindi huo kwa kocha huyo wa zamani wa Barcelona.

"Licha ya kukosekana kwa kocha, tulijiandaa vizuri," alisema Ramos.

Ramos alicheza mechi yake ya 164 kwa Hispania, akikaribia rekodi ya Iker Casillas ambaye amemzidi mechi tatu tu.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




## BOATENG AKATAA BASI LA MESSI, APANDA LA ZLATAN

●●● Afuta pia nukuu yake ya zamani alipofunguka kuwa ni shabiki wa Madrid na kumuelezea Ronaldo kama mchezaji bora duniani...

**BARCELONA,** Hispania

KEVIN-PRINCE Boateng, ameshangaza wengi baada ya kuweka wazi kuwa Zlatan Ibrahimovic ndiye mchezaji bora zaidi aliyewahi kucheza naye huku kiungo huyo akimweka kando nyota na mchezaji mwenza wa Barcelona, Lionel Messi.

Boateng amecheza pamoja na wanasoka mbalimbali wakubwa duniani, lakini Ibrahimovic ndiye anayeonekana bora zaidi kwa nyota huyo wa zamani wa kimataifa wa Ghana.

Ibrahimovic na Boateng walicheza pamoja AC Milan, na wawili hao walisaidia miamba hiyo ya Serie A kutwaa ubingwa msimu wa 2010-11.

Alipotakiwa kutaja mchezaji bora aliyewahi kucheza naye, Boateng aliiambia Barcelona TV katika mahojiano ya swali na jibu: "Zlatan Ibrahimovic."

Jibu la Boateng lilikuja kama mshangao, haswa ukichukulia ukweli kwamba anacheza na mshindi mara tano wa tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ['Ballon d'Or'] na mfungaji kinara wa wakati wote wa Barca, Messi.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 32, ambaye alikamilisha uhamisho wake wa kushtukiza wa mkopo wa kujiunga na Barca Januari mwaka huu, alilazimika kufuta madai yake ya zamani ya kuiheshimu Real Madrid na Cristiano Ronaldo baada ya kutua hapo Camp Nou.

Boateng alimsifu Messi kama mchezaji bora "katika dunia hii na duniani kote" wakati wa uwasilishaji wake rasmi baada ya nukuu yake iliyopita akifunguka mwenyewe kwamba ni shabiki wa Madrid na kuelezea Ronaldo kama mchezaji bora duniani.

Messi amefunga mabao 39 katika mashindano yote msimu huu, wakati Boateng amecheza mechi tatu tu tangu achomoke Sassuolo na kujiunga na Barca kwa mkopo.

## KWA UFUPI

### RASHFORD KUMRITHI SUAREZ BARCA

BARCELONA inavutiwa kumsajili mshambuliaji wa England na Manchester United, Marcus Rashford lengo likiwa ni kumuandaa kumrithi Luis Suarez. Mkataba wa straika huyo mwenye umri wa miaka 21, unamalizika mwaka 2020. **(Mundo Deportivo - in Spanish)**

### HUDSON-ODOI HAUZWI - CHELSEA

CHELSEA haitamuuza winga wa England, Callum Hudson-Odoi, 18, hata kama atakataa kusaini mkataba mpya , wakati huu Bayern Munich na Manchester United zikijiandaa kutoa ofa majira ya joto. **(Times)**

### UNITED YAMFUATILIA SALIBA

MANCHESTER United inamfuatilia beki wa St-Etienne, Mfaransa William Saliba, 18. **(Le 10 Sport - in French)**

### OZIL, MKHITARYAN SOKONI ARSENAL

ARSENAL ipo tayari kuwauza kiungo Muarmenia Henrikh Mkhitaryan, 30, na Mjerumani Mesut Ozil, 30, wakati ikijaribu kupunguza mzigo mkubwa wa mishahara. **(Mirror)**

### TIERNEY, BARELLA LULU ARSENAL

ARSENAL itatumia fedha itakazopata kwa kuwauza wachezaji wake, kuwanunua beki wa Celtic, Mscotland Kieran Tierney, 21, na kiungo wa Cagliari, Mtaliano Nicolo Barella, 22. **(Metro)**

### MOURINHO AITAJA LYON, MONACO

KOCHA wa zamani wa Chelsea na Manchester United, Jose Mourinho, 56, amezitaja klabu za Ligue 1 Ufaransa, kama sehemu ijayo atakayoweza kufanya kazi. **(L'Equipe)**

### STERLING AMA HAZARD MADRID

REAL Madrid inaweza kumnunua mshambuliaji wa Manchester City na England, Raheem Sterling, 24, badala ya kiungo wa Chelsea na Ubelgiji, Eden Hazard, 28, kwa mujibu wa straika wa zamani wa Blackburn, Chris Sutton. **(Mail)**

### JUVE, ARSENAL MBIO MOJA

ARSENAL na Juventus ni miongoni mwa klabu zinazovutiwa kumsajili beki wa kushoto wa Benfica, Alejandro Grimaldo wa Hispania. **(Calcio Mercato)**

### CASILLAS SASA KUZEEKEA PORTO

KIPA Mhispania Iker Casillas, 37, amesaini mkataba mpya wa mwaka mmoja na Porto na kueleza atastaafia soka lake la kulipwa katika klabu hiyo ya Ureno. **(Sky Sports)**

### RAKITIC ANUKIA SOKONI BARCA

BARCELONA inaweza kuamua kumuuza Ivan Rakitic, 30, majira ya joto, wakati huu Manchester United na Inter Milan zikimfuatilia kiungo huyo wa kimataifa wa Uswisi. **(ESPN)**

### GRIEZMANN ALIA KULISHWA MANENO

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid, Antoine Griezmann, amesema "analishwa" kuhusu tetesi za mustakabali wake wa baadaye. Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 28, amekuwa akihusishwa na kujiunga na Barcelona na Manchester United. **(Univision - in French)**

### LIVER KUIBOMOA NORWICH

LIVERPOOL inajiandaa kulipa pauni milioni 10 ili kumsajili beki wa Norwich City, Muingereza Ben Godfrey, 21. **(Football Insider)**

### MORENO KUTIMKIA BARCA

BEKI wa kushoto wa Liverpool, Alberto Moreno, 26, anajiandaa kushtukiza majira ya joto kwa kujiunga na Barcelona. Mhispania huyo alijiunga na Liverpool mwaka 2014. **(Liverpool Echo)**

## Watoto mazingira hatarishi waiita TFF

**Na Mary Geofrey**

VIJANA wanaoishi katika mazingira hatarishi jijini Dar es Salaam, wameliomba Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuwasaidia kuendeleza vipaji vyao ili kutimiza ndoto zao za kuwa wachezaji bora ndani na nje ya Tanzania.

Wito huo ulitolewa jana na vijana hao katika mchezo wa bonanza la kutafuta timu bora ya Mkoa wa Dar es Salaam lililoshirikisha timu nne za watoto wanaoishi katika mazingira magumu wa Feri, Kigamboni, Ubungo na Kariakoo.

Akizungumza na waandishi wa habari katika viwanja vya Jakaya Mrisho Kikwete Youth Park (JMK Park) katika mchuano huo ulioandaliwa na kituo cha kulea watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi cha Dogodogo Centre, Simon Zuber (19), alisema wanahitaji kuungwa mkono na TFF.

Alisema Dogodogo Centre wamewasaidia kuwaunganisha, kuunda timu na kuanzisha mashindano hayo, hivyo TFF wanatakiwa kuunga mkono kusimamia vipaji hivyo na kuvilea kuhakikisha havipotei.

"Tunachoiomba TFF watusaidie kufikia ndoto zetu, mchezaji akishaibuliwa akaonekana ana uwezo mzuri wa kucheza mpira ni vema sasa wakamlea, kumkuza na kuhakikisha anafikia ndoto yake ya kuwa mchezaji bora wa kimataifa ikizingatiwa kuwa sisi ni watoto wa mitaani ambao hatuna wasimamizi," alisema Zuber.

Jumanne Khamis aliiomba TFF pia kuwadhamini katika mashindano hayo kwa kuwapatia vifaa vya michezo kama mipira, viatu na jezi.

Kwa upande wake kocha wa timu hiyo, Ally Ditufi, alisema wamekuwa wakiwafuata watoto hao mitaani na kuwaundia timu katika maeneo yao na baadaye kushiriki katika bonanza la kutafuta timu ya mkoa.

"Tunawafuata mitaani na tunaanza kucheza nao huko huko hadi hapo tunapokuwa tumekamilisha timu kama hivi tunafanya bonanza hili ambalo limejumuisha timu nne. Wachezaji ambao tutawaona wana viwango vya hali ya juu, tutawasajili kucheza timu ya mkoa," alisema.

Alisema bonanza kama hilo wanafanya mara tatu kwa mwaka na lengo ni kuinua vipaji vya watoto wa mitaani, kuwaepusha na kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya na kujitambua kupitia michezo.

# TIMU SHIRIKI CASTLE LAGER AFRICA 5S HADHARANI WIKI HII

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya Castle Lager Africa 5s yameshika kasi baada ya jumla ya timu 48 kati ya 60 zinazotarajiwa kuingia katika kinyang'anyiro hicho kwenye raundi ya kwanza kufikiwa na promosheni maalum inayoshughulikia mchakato huo kutoka Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) kupitia bia yake ya Castle Lager.

Mashindano hayo ya soka yanayohusisha uwanja mdogo na wachezaji watano watano kila upande, yanafanyika kwa mwaka wa pili jijini Dar es Salaam yakishirikisha takriban baa 60 kutoka katika wilaya zote tano.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, Meneja wa Bia ya Castle Lager, Pamela Kikuli, alisema, tayari mchakato wa kutafuta timu shiriki za fainali za mashindano hayo kupitia timu za promosheni kwenye baa mbalimbali za jijini Dar es Salaam umeshaanza na baa 48 zimeshafikiwa, ambapo wiki hii watakamilisha kwa kuzifikia baa 12 ili kukamilisha 60 kwa raundi ya kwanza.

"Tutarudi tena kwa raundi ya pili katika hizo baa kuhakiki timu zao na baa 32 zitakazokuwa zimeongoza kwa mauzo zitakuwa zimefuzu rasmi kuingia kwenye fainali ya bonanza kubwa litakalofanyika viwanja vya Leaders jijini Dar es Salaam," alisema Kikuli.

Aidha, Kikuli aliwashukuru wakazi wa jijini Dar es Salaam kwa kuitikia wito kwa kuwa mwamko wa mwaka huu ni mkubwa ukilinganisha na mwaka jana, kwani kila baa miongoni mwa zilizoingia kwenye mchakato zinashauku ya kutaka kushiriki mashindano hayo yanayofanyika nchini kwa mara ya pili, chini ya udhamini wa bia ya Castle Lager, lakini pia yakifanyika nchi mbalimbali barani Afrika.

"Mwaka jana tulifanya mashindano haya kwa mara ya kwanza na kupata mwakilishi aliyeshiriki katika michuano ya kimataifa ya Afrika, iliyofanyika nchini Zambia kwa kuzikutanisha timu za Afrika Kusini, Zimbabwe, Swaziland Lesotho na wenyeji Zambia.

"Mwaka huu, tunatarajia kuwa na mashindano bora zaidi yatakayotusaidia kupata washindani na mabalozi wazuri katika michuano ya kimataifa itakayofanyika nchini.

"Mchakato wa kupata timu zitakazoshiriki katika bonanza hilo umeboreshwa zaidi mwaka huu, ambapo washiriki watapatikana kupitia promosheni zitakazofanyika katika baa mbalimbali jijini Dar es Salaam.

Lengo ni kuwafikia wanywaji wa bia ya Castle Lager ikiwa ni pamoja na kuwapa fursa ya kutimiza ndoto zao.

Timu za promosheni zimekuwa zikipita baa mbalimbali kwa ajili ya kutoa maelekezo kwa wateja kwa namna ambayo wanaweza kushiriki katika uundaji wa timu zao.

Ili kuingia 32 bora, moja ya kigezo muhimu ni kufanya mauzo mengi ambapo kutakuwa na makasha maalumu katika baa husika kwa ajili ya kukusanyia vizibo baada ya mteja kununua bia ya Castle Lager.




Meneja wa Bia ya Castle Lager, Pamela Kikuli, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi. **MPIGAPICHA WETU**

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.Yanga | 28 | 21 | 4 | 3 | 45 | 19 | 67 |
| 2.Azam | 28 | 17 | 8 | 3 | 46 | 18 | 59 |
| 3.Simba | 21 | 17 | 3 | 1 | 45 | 7 | 54 |
| 4.Lipuli | 31 | 11 | 11 | 9 | 26 | 26 | 44 |
| 5.Kinondoni MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 6.Mtibwa Sugar | 29 | 12 | 5 | 12 | 30 | 23 | 41 |
| 7.TZ Prisons | 30 | 9 | 11 | 10 | 24 | 25 | 38 |
| 8.Coastal Union | 30 | 8 | 14 | 8 | 27 | 30 | 38 |
| 9.Mbeya City | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 10.Alliance | 30 | 9 | 10 | 11 | 23 | 30 | 37 |
| 11.Mwadui | 31 | 10 | 6 | 15 | 35 | 39 | 36 |
| 12.Kagera Sugar | 29 | 8 | 12 | 9 | 23 | 27 | 36 |
| 13.JKT Tanzania | 31 | 8 | 12 | 11 | 18 | 26 | 36 |
| 14.Mbao | 30 | 9 | 9 | 12 | 19 | 29 | 36 |
| 15.Stand Utd | 31 | 10 | 6 | 15 | 29 | 40 | 36 |
| 16.Ruvu Shooting | 31 | 8 | 11 | 12 | 27 | 37 | 35 |
| 17.Singida Utd | 30 | 8 | 9 | 13 | 20 | 31 | 33 |
| 18.Ndanda | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 19.Biashara Utd | 29 | 7 | 9 | 13 | 21 | 29 | 30 |
| 20.African Lyon | 31 | 4 | 10 | 17 | 19 | 39 | 22 |

# Majaliwa mgeni rasmi Sokoine Marathon 2019

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mashindano ya riadha ambayo yameandaliwa kumuenzi aliyekuwa Waziri Mkuu katika serikali ya awamu ya kwanza, Hayati Edward Moringe Sokoine.

Mashindano hayo yanatarajiwa kufanyika Aprili 6, mwaka huu, jijini hapa na yataanzia katika eneo la Clock Tower, kuzunguka barabara kadhaa na yatamalizikia kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Kumbukumbu ya Sokoine, ambaye aliwahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Lembris Kipuyo, alisema jana kuwa mashindano hayo yatahusisha mbio za nusu marathon (kilomita 21), kilomita tano na nyingine maalumu kwa ajili ya watoto.

Kipuyo alisema mashindano hayo ambayo yameandaliwa na familia ya marehemu Sokoine yanajulikana kwa jina la Sokoine Memorial Marathon na yatakuwa yakifanyika kila mwaka.

"Haya mashindano yanafanyika kama sehemu ya maandalizi ya maadhimisho ya kumbukumbu ya kifo cha marehemu, Edward Sokoine, na yatafanyika nyumbani kwake Monduli Juu, Aprili 12, mwaka huu," alisema Kipuyo.

Alisema pia kutakuwa na ibada maalum ya kumbukumbu ya miaka 35, imeandaliwa katika kijiji cha aliyekuwa kiongozi huyo wa nchi na inatarajiwa kuhudhuriwa na wageni kutoka sehemu mbalimbali nchini.

Kwa upande wake, Katibu wa Chama cha Riadha Mkoa wa Arusha, Alfred Shahanga, alisema wanatarajia mashindano hayo yataungwa mkono na viongozi mbalimbali wa serikali, siasa na dini.

Shahanga alisema mwanariadha atakayeibuka mshindi wa kwanza katika mbio hizo atapata zawadi ya fedha taslimu ambazo zimeandaliwa na familia na kwa upande wa watoto watapata zawadi kwa ajili ya matumizi ya shule.

# Michezo

Alhamisi Machi 28, 2019

Nipashe


## Boateng akataa basi la Messi, apanda la Zlatan



HABARI UK. 30

## Uchaguzi Yanga sasa kumenoga

**Na Mwandishi Wetu**

MCHAKATO wa uchaguzi wa Klabu ya Yanga ya jijini Dar es Salaam sasa utaanza upya baada ya viongozi wake wawili kutangaza kuachia ngazi nafasi zao rasmi hapo jana, imeelezwa.

Awali Kamati ya Uchaguzi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ilikuwa inasimamia mchakato wa kufanya uchaguzi mdogo wa kujaza nafasi nne ambazo ni ya Mwenyekiti na wajumbe watatu wa Kamati ya Utendaji ya klabu hiyo.

Viongozi waliotangaza kujiuzulu jana ni pamoja na Kaimu Mwenyekiti, Samuel Lukumay na Mjumbe wa Kamati ya Utendaji, Hussein Nyika ambaye pia alikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano na bosi mkuu wa Kamati ya Usajili.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Ally Mchungahela, alisema tayari ameshapata taarifa za kujizulu kwa viongozi hao wawili na anapenda kutangaza rasmi kwamba uchaguzi wa Yanga sasa utakuwa ni uchaguzi mkuu.**

Mchungahela alisema anaamini "vikwazo" ambavyo vilikuwa vinachangia kutekeleza majukumu katika kamati yake sasa havitakuwapo kwa sababu ya hali halisi iliyopo klabuni hapo.

"Uchaguzi wa Yanga sasa utakuwa ni wa jumla, namaanisha uchaguzi wa kuchagua viongozi wa kujaza nafasi zote, na kwa kifupi mchakato utaanza upya," alisema Mchungahela.

**LUKUMAY, NYIKA WANENA**

Licha ya kutangaza kujiuzulu, Lukumay na Nyika wameahidi kuendelea kushirikiana na wanachama wote wa Yanga ili kufanikisha timu yao kupata matokeo mazuri kwa sababu bado na wao ni wanachama wa klabu hiyo.

"Kujiuzulu kwetu haina maana tutakaa mbali na Yanga, tutaendelea kuwa bega kwa bega, tutashiriki katika mambo mengine, hata kabla hatujakuwa viongozi, tulishirikiana na wenzetu katika vitu vingi," alisema Lukumay.

Naye Nyika alisema kuwa anashukuru kuona wameiacha Yanga ikiwa inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara na vile vile ikiwa kwenye hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA.

UJUZI...



Mshambuliaji wa Brazil, Richarlison akionyesha ujuzi wake kwa kumiliki mpira hewani wakati wa mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Jamhuri ya Czech ambayo walishinda 3-1 wakitokea nyuma. Wafungaji wakiwa ni Gabriel Jesus (mawili) na Roberto Firmino. **PICHA: DAILY MAIL**

# SIMBA, TUYISENGE WAMALIZANA RASMI

### ●●● Yaizidi AS Vita ujanja, sasa kuunda kombinesheni hatari na Kagere baada ya...

**Na Somoe Ng'itu**

KATIKA kuhakikisha msimu ujao inakuwa imara zaidi na kufanya vema katika mashindano mbalimbali watakayoshiriki, uongozi wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam umefanikiwa kunasa saini ya mshambuliaji wa Gor Mahia ya Kenya, Jacques Tuyisenge.

Taarifa zilizopatikana jana jijini Dar es Salaam kutoka chanzo chetu cha uhakika ambacho hakikuwa tayari kutajwa gazetini, zimeeleza kuwa mshambuliaji huyo raia wa Rwanda alikuja nchini juzi na kusaini mkataba wa awali na Simba wa miaka miwili.

Chanzo chetu kilieleza kuwa Simba ililazimika kuwahi kumpa mkataba wa mshambuliaji huyo kwa sababu pia timu ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ilikuwa ikimtaka akazibe nafasi itakayoachwa na Jean-Marc Makasu ambaye ameshasaini mkataba na AS Berkane ya Morocco.

"Ni kweli Tuyisenge yuko nchini na muda huu (juzi usiku) ana kikao chake na viongozi wetu kimekwenda vizuri, yaani siku hizi hakuna siri, alifichwa lakini jamaa wamemuona," kilieleza chanzo chetu ambacho kinafasi ni kiongozi wa juu wa Simba.

Kiliongeza kuwa moja ya sababu iliyorahisisha Tuyisenge kutua Simba ni kutaka kukutana na "pacha" wake wa zamani ndani ya Gor Mahia na kwenye timu ya Taifa ya Rwanda (Amavubi), Meddie Kagere.

Taarifa zaidi kutoka Simba zimeeleza kuwa pia uongozi wa klabu hiyo uko katika hatua nzuri za kusaini mikataba mipya na washambuliaji wake, Emmanuel Okwi na Kagere ambao msimu huu wameisaidia sana timu hiyo hadi kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hata hivyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alipoulizwa na Nipashe alishindwa kusema lolote kuhusiana na usajili wa mshambuliaji huyo ambaye kwa sasa ameshaichezea Gor Mahia mechi 97, za mashindano mbalimbali.

Kwa sasa kikosi cha Simba kinaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuwavaa Mbao FC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro.

Simba inatumia Uwanja wa Jamhuri baada ya Uwanja wa Taifa kufungwa ili kupisha maandalizi ya fainali za Afrika za Vijana wa umri chini ya miaka 17 (AFCON U-17) zitakazochezwa kuanzia Aprili 14 hadi 28, mwaka huu hapa nchini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002